# UWASILISHAJI WA WAHUSIKA NA UHUSIKA WA KIMAZINGAOMBWE KATIKA RIWAYA ZA *WATU WA GEHENNA* (TOM OLALI) NA *BABU ALIPOFUFUKA* (SAID AHMED MOHAMED)

**ANNE CHELANGAT KENDUIYWA**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI KATIKA IDARA YA ISIMU, FASIHI NA MAWASILIANO**

**CHUO KIKUU CHA KABIANGA**

**FEBRUARI, 2022**

# UNGAMO NA IDHINISHO

## Ungamo la mtahiniwa

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa kwa shahada katika Chuo Kikuu chochote.

Kenduiywa Chelangat Anne

PGC/KIS/011/12

Sahihi: ………………………………  Tarehe: ………………………………….

## Idhinisho

Tasnifu hii imewasilishwa kwetu ili kutahiniwa kwa ushauri na idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kabianga.

Prof. Issa Mwamzandi

Sahihi: ……………………………  Tarehe: ………………………………….

Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Kabianga

Dkt. Emmanuel Kisurulia

Sahihi: ……………………………  Tarehe: ………………………………….

Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Kabianga

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa na kibali cha kuelimika. Pia kwa heshima na dhati ya moyo wangu natabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapenzi: Mama yangu marehemu Rael Chepkirui Koske na marehemu baba yangu Mwalimu Wilson Kipsongol Koske kwa juhudi zao za kunilea na kunisomesha kisha kunifanya niwe na kiu ya masomo ili niweze kufaulu maishani. Bila shaka nina imani Mwenyezi Mungu kwa rehema na mapenzi yake amewajaalia wawe miongoni mwa waja wa Peponi. Aidha naitabaruku kazi hii pia kwa wanangu Moses, Daniel, Mercy, Raymond, Juliet, Peter na Jacquelyn na mume wangu Bw. Stanley Kenduiywa. Ahsanteni kwa kunivumilia nilipochukua muda wenu mwingi kwa ajili ya masomo yangu.

## SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Maulana kwa uhai, neema na kibali chake masomoni. Utukufu na sifa ni kwake milele kwa sababu yeye hutoa vyote bure.

Pili, nawatolea shukrani zisizo na kifani wasimamizi wangu: Profesa Issa Mwamzandi na Dkt. Emmanuel Kisurulia. Sina lugha ya kuelezea msaada wenu wa maarifa, mapendekezo, maoni na mwongozo wa kila aina ambao ni wa thamani kubwa. Asanteni na Mungu awabariki.

Tatu, ni kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kabianga kwa ushauri na maarifa yao yasiyopimika hasa Dkt. Salim Sawe na Dkt. Alexander Rotich. Mungu awabariki.

Ninamshukuru mume mwandani wangu Bw Stanley Kenduiywa kwa mapenzi yake, msaada wa kifedha, ushauri na pia kunitia moyo wakati nilipokuwa nimekata tamaa. Baraka na mema yakuandame kila ulipo.

Shukrani zingine ni kwa wanangu wapendwa Moses, Daniel, Mercy, Raymond, Juliet, Peter na Jacquelyn. Ninawashukuru sana kwa kuwajibika kwenu kila wakati nilipowahitaji. Mungu awabariki na kuwaongoza katika shughuli zenu zote.

Mwisho, ni shukurani zangu zisizo na ukomo kwa wanafunzi wenzangu walioniauni darasani, Bi Mercy Moraa na Bw Ezekiel Kurgat. Nawatakia mema maishani.

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu uchunguzi wa uwasilishaji wa wahusika na uhusika wa kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* ya Tom Olali na *Babu Alipofufuka* ya Said Ahamed Mohammed. Swala hili la uhusika na uhusika wa kimazingaombwe katika utafiti huu limechochewa na ukweli kwamba usawiri wa wahusika wa aina hii huzua hali ya utata kwa wasomaji. Baadhi ya wasomaji hujikuta wametanzwa na wahusika waliomo ndani ya riwaya na kuufanya uhusika wao usieleweke ipasavyo. Istilahi ya 'uhalisiamazingaombwe' mwanzoni ilitumika kurejelea fani ya uchoraji katika miaka ya 1920 baadaye ikatumika kufasili kazi za bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina, na halikadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel García Marquez wa Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Günter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia, na John Fowles wa Uingereza. Waandishi hawa wanafahamika kwa jinsi walivyoambatanisha mbinu za uchoraji na za uandishi katika kazi zao za fasihi katika ruwaza inayobadilikabadilika daima, huku wakiwasilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengee vya kifantasia na kindoto kwa kutumia mambo yaliyotokana na visaasili na hekaya. Tasnifu imechambua usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe katika riwaya hizi na jinsi unavyokuwa nyenzo ya kuwasilisha ujumbe wa kipekee wa waandishi walioteuliwa. Data imechanganuliwa na kuwasilishwa kwa namna ya maelezo. Hususani, matokeo ya kimaajabu na yasiyokuwa ya kawaida yanayohusu wahusika na uhusika wao yamenakiliwa na kisha kutolewa maelezo. Matokeo hayo yameelezwa huku yakiegemezwa na haja za waandishi za kuwasilisha ujumbe maalum waliounuia. Matokeo ya utafiti huu yanadhamiria kukuza na kupanua uelewekaji wa riwaya za kimazimgaombwe kwa jumla. Tasnifu imejaribu kujaza mapengo yanayoleta matatizo ya ufahamu wa kazi zilizoteuliwa. Katika kazi hizi matukio yanasawiriwa kiajabuajabu, ni ya kuogofya, kutisha na hayaeleweki kwa urahisi.Uhakiki wetu utawapa motisha wahakiki wengine kushughulikia zaidi wahusika, uhusika na uwasilishaji katika misingi ya umazingaombwe katika fasihi. Aidha, utafiti huu utawawezesha wasomaji kusoma upya kazi hizi za kifasihi na nyinginezo nyingi za karne ya ishirini na moja ambazo huwatanza wasomaji wanagenzi.

# ABSTRACT

This study focuses on investigating the presentation of ghost like characters in Watu wa Gehenna (Tom Olali) and Babu Alipofufuka (Said Ahamed Mohammed). The presentation in this study has been prompted by the interactive nature of the characters which creates a complexity for the readers in capturing the messages conveyed by the characters in these selected experimental novels. The term 'magical realism', originally used by painters in the 1920s, used to describe the literary works of Argentina's Jorge Luis Borges, as well as the works of writers such as Gabriel García Marquez of Colombia, Isabel Allende of Chile, Günter Grass of Germany, Italo Calvino of Italy, and John Fowles of England. These authors combine a specially formulated reality in an ever changing pattern, representing a series of detailed descriptions of fantasy and using fantasy elements such as myths and legends in their works. Their works presuppose that through magical transformations, the co-relation between magic and artistic expression is evident. When magical transformations are utilized in literary works, they foreground meaning. In essence, this is a form of defamiliarization or deviation from the usual mode, aimed at making society to examine itself more critically. The authors of these works use a variety of writing techniques to the point of making these novels challenging to read. Magical realism leaves a lot of readers in confusion. A mode that exists somewhere between fantasy and reality, many readers get mixed up with speculative fiction, urban fantasy, and much more. It can be unsettling, and some readers find it absolutely infuriating. It is in this context that the research seeks to analyze magical transformations in the above mentioned novels. The research will be mainly library based. The data will be analyzed and presented in the form of explanation. The findings of this study aim to promote and expand the understanding of novel and multimodal approaches. This research will inspire other researchers to study more effectively the diversities of characters and magical presentations on the basis of Magical Realism in literature.

# YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINISHO ........ ii
TABARUKU ........ iii
SHUKRANI ........ iv
IKISIRI ........ v
ABSTRACT ........ vi
SURA YA KWANZA ........ 1
UTANGULIZI ........ 1
1.0 Kitangulizi ........ 1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti ........ 1
1.2 Tatizo la Utafiti ........ 4
1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 4
1.4 Nadharia Tete ........ 5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........ 5
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 6
1.7 Hitimisho ........ 7
SURA YA PILI ........ 8
YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI ........ 8
2.0 Utangulizi ........ 8
2.3 Dhana ya Wahusika ........ 14
2.4 Dhana ya Uhusika ........ 16
2.5 Dhana ya Usawiri ........ 17
2.6 Dhana ya Mandhari ........ 17
2.7 Uwasilishaji wa Umazingaombwe ........ 19
2.8 Misingi ya Nadharia ........ 19
2.9 Hitimisho ........ 23
SURA YA TATU ........ 24
MBINU ZA UTAFITI ........ 24
3.0 Utangulizi ........ 24
3.1 Muundo wa Utafiti ........ 24
3.2 Uteuzi wa Sampuli ........ 25
3.3 Njia za Kukusanya Data ya Utafiti ........ 26
3.4 Uchanganuzi wa Data ........ 27
3.5 Uwasilishaji wa Data ........ 28
3.6 Maadili ........ 28
3.7 Hitimisho ........ 29
SURA YA NNE ........ 30
UWASILISHAJI WA WAHUSIKA NA UHUSIKA WA KIMAZINGAOMBWE ........ 30

4.0 Utangulizi ........................................................................................................................ 30
4.1 Swala la Wahusika, Uhusika na Mandhari ................................................................................ 31
4.1.1 Wahusika, Uhusika na Mandhari ya Kimazingaombwe katika *Babu Alipofufuka* .................. 32
4.1.2 Wahusika, Uhusika na Mandhari ya Kimazingaombwe katika *Watu wa Gehenna* ................ 46
4.3 Umazingaombwe katika Uwasilishaji wa Wahusika Wadogo .................................................. 85
4.4 Hitimisho ................................................................................................................................ 96
SURA YA TANO ............................................................................................................................ 97
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................................................. 97
5.0 Utangulizi ............................................................................................................................... 97
5.1 Muhtasari wa Tasnifu .............................................................................................................. 97
5.3 Kuafikiwa kwa Nadharia Tete ................................................................................................ 104
5.4 Mapendekezo ......................................................................................................................... 106
MAREJELEO ................................................................................................................................ 108

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Kitangulizi

Sura tangulizi katika pendekezo hili imejengwa kwa kuzingatia msingi wa utafiti huu ambapo tumeangazia usuli pamoja na tatizo la utafiti. Yanayoshughulikiwa pia katika sura hii ni madhumuni ya utafiti, nadharia tete na sababu za kuchagua mada. Aidha, ubainishaji wa upeo na mipaka ya utafiti umefanywa.

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Uwasilishaji ni dhana inayotumiwa kuelezea njia au mtindo unaotumiwa na wasanii wa fasihi katika upashaji wa ujumbe hadi uwafikie walengwa wao, yaani wasomaji (Wamitila 2003). Wahusika ni wenzo muhimu katika kufanikisha kazi ya msanii katika utanzu husika. Wahusika ndio kisemeo ambacho msanii wa kazi ya fasihi anakihitaji kutimizia lengo aliyonayo mawazoni mwake. Mtunzi huwachora wahusika wake kwa lengo la kuwasilisha maudhui ya kazi yake kwa jamii husika.

Katika fasihi, wahusika ni binadamu (watu) au viumbe inginevyo kama wanyama, au vitu vyengine vinavyowakilisha matendo ya kibinadamu ambavyo watunzi huvitumia kwa lengo kuu la kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Wamitila (2008) anasema kwamba, wahusika wowote wa kifasihi ni wenzo kuu katika kazi za kifasihi. Hii ni kwa sababu wao ndio wanaoendesha kazi zote za fasihi na kuzalisha matukio na masimulizi kulingana na mpangilio wa mtunzi. Wamitila anaendelea kuelezea kuhusu watenda kazi katika sanaa, akisema kuwa wahusika ni viumbe ambao majukumu yao ni kutekeleza shughuli alizonazo mtunzi mawazoni mwake. Wahusika hao wanasawiriwa kuchukua sehemu kubwa katika kazi

nzima ya kifasihi sifa zao zikiwatambulisha kulingana na maadili, itikadi na falsafa zao. Hivi ni kusema kuwa waandishi husawiri wahusika wao waambatishe mambo wanayoyasema katika mazungumzo na yale wanayoyatenda kulingana na matukio yao. Kwa hivyo msingi wa uhusika na uwasilishaji ndiyo kiini cha motisha na uhamasishaji wa wahusika hao katika riwaya za Kiswahili. Wajibu mkuu wa wahusika katika fasihi ni kuwasilisha ujumbe kwa kushirikisha matendo, hisia, mazumgumzo na mawazo ya mwandishi.

Mtazamo wa dhana ya wahusika unaweza kutofautiana kutegemea mtindo na utaratibu unaofuatwa au anaouchukua mhakiki au mwandishi katika uhusika na pia kulingana na nadharia ya fasihi inayohusishwa. Kwa mfano, mtunzi anasawiri wahusika wa kihalisia wawe na sifa nyingi zinazohusishwa na binadamu katika maisha ya kawaida katika jamii kisha kubuni wahusika wa kimazingaombwe na kuwahusisha kwa kiasi kikubwa na matukio ya kinjozi au wa kifantasia. Mtunzi pia anaweza kusawiri wahusika wowote kisha kuwaweka katika mandhari au mazingira ajabuajabu na hata kusababishwa wawe na sifa za ulimbwende wanaposhikamana na viumbe wasiokuwa wa kawaida. Njozi hutumiwa kutekeleza masimulizi katika kazi ya fasihi ambayo huonyesha na kufichua mambo anayoyawaza msanii kwa kiwango cha juu na kusababisha matukio ya kimazingaombwe.

Uhusika katika fasihi ni istilahi ambayo hutumiwa kuelezea mbinu na mikakati inayotumiwa na watunzi kuwasawiri wahusika katika kazi zao. Suala la uhusika huwa kipengele ambacho kinaonyesha jinsi matukio yanayopatikana katika kazi za kifasihi yanavyowaathiri wahusika. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa dhana ya uhusika ni umithilishaji wa matendo vya viumbe wanaopatikana katika kazi za kifasihi na vile vya viumbe katika ulimwengu razini. Njogu na Chimerah wanadai kuwa kilicho na uzito na maana kabisa katika fasihi ni

jinsi matendo au matukio yanayofanyika yaweze kuafikiana na kuathiri matukio ya aina mbalimbali ya wahusika kuambatana na malengo ya msanii husika. Kulingana na Wamitila (2003) athari hizo huwa na matokeo mengi tofautitofauti kuhusu utaratibu unaofuatwa au mikabala inayoenda sambamba na matukio yaliyojengeka kutokana na mbinu zilizotumiwa katika usawiri. Wamitila anafafanua saidi kuwa uhusika ni ile hali au sehemu inayochangiwa na wahusika katika kazi ya fasihi. Mchango huu unaweza kuonekana kupitia kwa mawazo yao, matendo yao, mazungumzo yao na hata kwa malengo yao yanayodhihirisha ufaafu wa kazi za watunzi katika fasihi husika.

Mfano ni katika matumizi ya majina au mbinu ya majazi katika kutekeleza kazi za kimazingaombwe katika fasihi. Majina hayo huwa ni msingi muhimu wa uhusika. Katika mbinu hizi, mtunzi anaumba wahusika na kuwapa majina ambayo yanafumbata tabia, sifa na matendo yao kisha kuwafanya wapatikane katika mazingira ya kifantasia. Kwa njia hii, msomaji lengwa huweza kuifahamu mienendo au wasifu wa wahusika kwa njia inayofaa. Hata hivyo, kuna udhaifu katika masimulizi ya kimazingaombwe na msimuliwa hulazimika kuridhika na maoni ya mtunzi ama achanganyikiwe huku akikosa kupata maana inayobebwa katika ujumbe. Hii ni kwa sababu watunzi hutumia mbinu chanagamano katika uhusika bila kuhusisha msomaji katika uamuzi wa wasifu wa mhusika. Ingawa hivyo, waandishi wanaofuata mkondo wa kimazingaombwe huwa na sababu maalum zinazochochea uteuzi wa wahusika na uhusika unaoelekea kuwatanza wasomaji. Tasnifu hii imechochewa sana na uteuzi wa wahusika na uhusika wa aina hii kama mbinu ya uwasilishaji wa ujumbe wa waandishi teule.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Baadhi ya riwaya zilizoandikwa kwa njia ya umazingaombwe hazina mshikamano, muungano wala muumano wa hadithi toka mwanzo hadi mwisho kutokana na mbinu za kimajaribio za uhusika. Usawiri wa aina hii husababisha tatizo kwa wasomaji katika kufahamu lengo linalodhamiriwa na kuangaziwa na wahusika katika uwasilishaji wa ujumbe riwayani. Utunzi huu wa kimajaribio unahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kubainisha sababu za kuwepo kwa umazingaombwe katika masimulizi na matukio yanayoelekezwa na waandishi katika fasihi za kimajaribio. Kuna mwachano mkubwa kati ya mambo ya kweli katika dunia halisi na ile ya kindoto katika fasihi za kimajaribio. Hiyvo basi inadhihirika kuwa kuna pengo kati ya mambo tunayoyajua katika uhalisia na yale ambayo hatuyaelewi katika ndoto lakini yanaonekana kana kwamba ni matukio halisi. Hivyo ndivyo tunavyowajua wahusika katika riwaya nyingi ambapo yale yanayotendwa na wahusika wa kijadi na waliowasilishwa katika mkondo wa kihalisia huwa wanashabihi hali zetu za kila siku katika jamii. Matumizi ya wahusika na uhusika usioweza kuyumkinika katika riwaya teule za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka* na sababu za kutumika kwake ni jambo lisilofahamika barabara. Utafiti huu, hivyo basi unaazimia kuchanganua vichocheo na sababu za kutumika kwa wahusika hao wa kinjozi kama njia ya uwasilishaji wa yaliyomo katika riwaya hizo.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni yetu katika utafiti huu ni kama yafuatayo:

1. Kubainisha jinsi vipengele vya uwasilishaji wa wahusika vinavyodhihirisha masimulizi ya kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka*.

2. Kuchunguza jinsi mbinu za uhusika katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka* zinavyomithilisha matukio na uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe.
3. Kuchanganua uwasilishaji wa wahusika ili kuainisha matukio na mandhari ya kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka.*

### 1.4 Nadharia Tete

1. Vipengele mbalimbali vya uwasilishaji wa wahusika vinadhihirisha masimulizi ya kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka*.
2. Mbinu za uhusika katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka* zinamithilisha matukio na uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe.
3. Uwasilishaji wa wahusika unaainisha matukio na mandhari ya kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka*.

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* zimeshughulikiwa katika kutafiti huu mintarafu ya jinsi wahusika na uhusika wao unavyojitokeza katika mandhari ya kimazingaombwe. Ni riwaya ambazo zimewekwa katika tapo la riwaya za kimajaribio ambazo zinakiuka kanuni za kijadi katika usawiri wa wahusika. Tumechagua mada ya utafiti huu ili tuchunguze jinsi watunzi wa riwaya hizi teule walivyotumia mbinu za kushangaza katika uhusika na muundo changamano wenye matukio na mandhari ya kimazingaombwe. Baada ya kutalii matini mbalimbali katika uchambuzi wetu, tumebaini kwamba hakuna mtafiti aliyewahi kufanya utafiti unaohusu uwasilishaji wa wahusika na uhusika wa kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka* licha ya kuwa ziko tafiti nyingi zilizofanywa juu ya wahusika katika tamthilia na riwaya kadha wa kadha.

Hivyo basi utafiti wetu unanuia kuziba pengo hilo lililoachwa na watafiti tangulizi pamoja na kuitikia mwito wa baadhi ya wasanii hao. Mfano wa wahakiki hao ni Nyabunga (2005) ambaye katika uhakiki wa *Bina-Adamu*! (2002) na *Musaleo*! (2004) za K.W. Wamitila anatoa pendekezo kuwa watafiti wengine washughulikie kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili na kuzihakiki kwa kutumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Kwa misingi hiyo, tumeona ipo haja ya kufanya utafiti wetu kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya kiuhalisiamazingaombwe.

Sababu nyingine ya kuteua mada hii ni kwamba utafiti huu umekuwa wa manufaa kwa wasomaji kwa sababu unalenga kuweka wazi uelewaji wa kazi za kimajaribio. Hii ni kwa sababu mada hii imetuwezesha kutafiti na kubainisha namna watunzi hao wanavyokiuka mbinu za kawaida katika utunzi wa kimapokeo na kuegemea mtindo wa kiajabu katika usawiri ili kuwasilisha ujumbe wao wa kidhahania. Usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe unawapa watunzi wa kimajaribio uhuru kuweka wazi umazingaobwe wa mambo mengi kwa azma ya kuwapa moyo na kuamsha ari za wanajamii kila wanapokabiliana na maswala wasiyoyafahamu vyema katika maisha yao ya kila siku. Suala hili ndilo lililotufanya tuamue kushughulikia mada hii kwa undani tukitarajia kwamba umesaidia kutoa taaluma ya fasishi linganishi hasa katika usawiri wa wahusika. Uchunguzi wa aina hii umeweza kubainisha namna ya kuchanganua uwasilishaji uliotofauti na ule wa kawaida katika fasihi za kijadi ili iwe nyongezo muhimu kitaaluma na kinadharia katika ngazi mbalimbali za kielimu na fani nyenginezo stahiki kwa walimu na wanafunzi vyuoni na kwengineko kwa jumla.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti wetu utashughulikia baadhi ya kazi za riwaya zilizoandikwa na Tom Olali na S.A. Mohamed. Hii ni kwa sababu waandishi katika fasihi za Kiswahili ni wengi na riwaya nazo

ni nyingi na wakati haukuturuhusu kuzichunguza riwaya zao zote. Said Ahmed Mohamed, kwa mfano, ameandika zaidi ya riwaya kumi zikiwemo *Nyuso za Mwanamke* (2010) , *Dunia Yao* (2006). Naye Tom Olali ni mwandishi chipukizi anayefahamika zaidi kutokana na uandishi wa riwaya ya *Mafamba* (2008). Uteuzi wa riwaya ya tasnifu umezingatia zaidi kipengele cha umazingaombwe na hasa unaohusu wahusika na uhusika wao – sifa ambazo hazijitokezi sana katika riwaya za awali za waandishi hawa.

Utafiti wetu umejikita katika riwaya mbili za kimajaribio ambayo ni *Watu wa Gehenna* (Tom Olali, 2012) na *Babu Alipofufuka* (Said Ahamed Mohamed, 2001) ambazo zimetutoshelesha kwa mahitaji ya utafiti wetu. Hii ni kwa sababu waandishi wa riwaya hizi mbili wamemezea mate mwelekeo wa umazingaombwe katika uumbaji wa wahusika wao na kutokana na hali hii, matarajio katika utafiti wetu yalifikiwa.

**1.7 Hitimisho**

Sura ya kwanza imejikita katika kujadili vipengele muhimu vya tasnifu hii ambavyo ni dira katika utafiti wetu wenye mada isemayo, uwasilishaji wa wahusika na uhusika wa kimazingaombwe katika Riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka*. Tumeshughulikia usuli wa suala la utafiti na kubainisha tatizo la utafiti wetu kisha kuangazia madhumuni pamoja na nadharia tete ambazo zitatuongoza katika kutafiti mada yetu. Vilevile, tumeeleza sababu za kuchagua mada ambayo tumeishughulikia katika utafiti wetu. Mbali na hayo, tumebainisha upeo na mipaka ya utafiti wetu katika sura hii. Tumekamilisha sura hii kwa kutaja misingi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe ambao tumetumia katika kuishughulikia uchanganuzi wa utafiti wetu. Sura ya pili inaangazia yaliyoandikwa kuhusu mada ya tasnifu na vilevile kufafanua nadharia iliyotumika.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imehakiki makala, vitabu na matini mbalimbali zinazohusiana na utafiti huu. Katika kutekeleza hilo, sura imeanza kwa kuangazia dhana ya umazingaombwe na uamilifu wake katika utunzi wa fasihi ulimwenguni. Aidha, swala la wahusika na uhusika wa kimazingaombwe umechunguzwa. Mwishoni sura hii imezingatia nadharia mahsusi iliyotumika, ya Uhalisiamazingaombwe, ili kuelewa namna waandishi walivyotumia maarifa haya ya kisasa kama nyenzo ya kuwasilisha ujumbe katika fasihi. Kwa misingi hiyo sura hii imejengwa kwa kurejelea kazi mbalimbali za waandishi tangulizi zenye uhusiano na mada husika ili kujenga ithibati na umakinifu wa kutimiza haja ya madhumuni na nadharia tete za utafiti wetu.

## 2.2 Dhana ya Umazingaombwe na Uamilifu wake katika Fasihi

Wataalamu mbalimbali wametoa fafanuzi tofauti tofauti kuhusu umazingaombwe. Katika fasihi, umazingaombwe ni dhana inayotumiwa na waandishi katika uhusika na kwa kusawiri wahusika kwa njia ambayo wanasababishwa kutekeleza matukio ya kiajabu. Akieleza kuhusu jambo hili, Mbatia (2002) anafafanua kuwa umazingaombwe ni nadharia mojawapo inaotumika kwa kiwango kikubwa katika kazi ya fasihi inayojengwa kutokana na matumizi ya mbinu changamano katika uhusika na usawiri wa wahusika.

Breton (1924) anaeleza kwamba utunzi wa kimazingaombwe ni uandishi katika fasihi unaohusu matumizi ya mbinu dhahania (kufikirika akilini) usioongozwa na kaida za kiutunzi za kijadi. Breton anaendelea kusema kuwa umazingaombwe ni mawazo ya vitu vilivyo kweli na vilevile visivyo kweli afikiriavyo mtunzi pamoja na kule kuchezea maneno kwa umakinifu kiasi cha kufanya yaliyomo akilini kudhihirika huku hadithi ya kushangaza ikiundika. Breton pia anaeleza kuwa uhalisiamazingaombwe hujikita katika kubainisha mtazamo wa hali halisi wa mtunzi wa kimajaribio na kueleza haja ya kifikra kupitia kwa mtazamo wa hali ya kinjozi na uhuru wa gezo. Msomi mwingine anayetoa mawazo yanayofanana na haya ya Breton ni Faris (1995) anayesema kwamba uhalisiamazingaombwe hulenga kukaidi mipaka ya uandishi wa riwaya za kawaida za kimapokeo na kwamba si hoja kujua mipaka hiyo imechukua mkondo upi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) uwasilishi katika sanaa za kimazingaombwe ni dhana inayotumiwa kuelezea njia ya kuwasilishia maana katika kazi ya kifasihi lengo likiwa kufikisha mawazo ya mwandishi hadi kwa wasimuliwa kwa kushughulisha wahusika wa aina mbalimbali wenye mawasiliano na matukio ya kiajabu. Mfano ni katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ambapo tunaelezwa kuhusu watu wanaokuwa na uwezo wa kubadilishwa na kufanywa kuwa tumbili jambo linalomfanya msomaji ajijengee picha akilini mwake na kutafakari umazingaombwe wa watu hao. Mambo ya aina hii katika fasihi huonekana yakiwa na ukubalifu fulani kuambatana na ubunifu wa kimiujiza ambapo lengo la mtunzi ni kupasha ujumbe wake kwa njia ya kipekee. Matukio ya wahusika hao wa kimazingaombwe husawiriwa kiajabuajabu kwa njia ya kuogofya au hata ya kutisha na kubabaisha msomaji. Hii ni kwa sababu si kawaida matukio haya kujitokeza kama yalivyo katika maisha yetu ya kila siku. Mtindo unaotumika katika uhusika na katika uwasilishaji wa ujumbe wa

kimazingaombwe huvunja sheria na kanuni ambazo zinatumika katika fasihi za kimapokeo au katika usawiri unaozingatia desturi ya kawaida katika jamii husika.

Jameson (1986) ameelezea kuwa umazingaombwe katika sanaa ni mvuto unaotanza (*strange attractiveness*) na unaovutia wasanii mbalimbali hasa katika nchi ambazo zilikuwa koloni za Wazungu. Hii ni kwa sababu kwa njia moja au nyingine mambo ya unyanyasaji jinsi yanavyodhihirika katika nchi zilizotawaliwa, yalisababisha wasanii nao waathirike kimawazo kutokana na athari za ukoloni. Jambo hili lilichangia wanafasihi wa kimajaribio kuelekea uigaji wa mitindo waliyoitumia Wakoloni hao katika fasihi zao. Mwelekeo huu umefaidi watunzi katika fasihi za kimajaribio kwa kuwawezesha kubuni na kusambaza ujumbe wao wa kimazingaombwe kwa dhati bila kudhalilika.

Abrams (1999) anaeleza kwamba nadharia ya uhalisiamazingaombwe ilibuniwa na Franz Roh aliyekuwa mhakiki wa sanaa. Franz Roh alitumia dhana hii ya uhalisiajabu katika kazi ya kifasihi kueleza na kuonyesha njia inayoweza kutumiwa katika kusawiri aina fulani ya wahusika wenye uwezo wa kutekeleza matukio ya kimazingaombwe.

D’Haen (2005) akiunga mkono uandishi huu wa kimazingaombwe anasema kuwa mwanzo kabisa, Franz Roh anayependelea hali ya kifantasia na ambaye aliamili kwa ukamili dhana ya umazingaombwe, alipata kuelekeza kazi yake ya usanii kwenye mkondo ambao unafanana na ule aliokuwa akiutumia katika kazi zake za uchoraji. Michoro yenyewe ilikuwa ya kawaida kama picha ya kamera lakini ambayo iliibua hisia za kushangaza na hata kuogofya na basi kusababisha kuwepo kwa umazingaombwe. D’Haen anaendelea kueleza kwamba usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe ni mkondo katika fasihi unaotumiwa

katika utekelezaji wa matukio ya usanii kulingana na mahitaji yanayoendelea kuenea katika jamii ya sasa hivi. D'Haen akiendelea katika ufafanuzi wake anaeleza kwamba uhalisia-mazingaombwe unabuni ulimwengu badilifu unaogeukageuka kuambatana na hali ya dunia ya kisasa katika jamii.

Uwasilishaji wa kiuhalisia au wa kijadi hufuatilia kanuni za kimapokeo ambazo hushabihi ukweli na wahusika hudhihirisha wasifu wa mwanadamu katika hali halisi kwa kuwa wanawakilisha mwanadamu wa kawaida jinsi anavyoishi katika mazingira halisi.

Wanauhalisia husisitiza matumizi ya mbinu za uhalisia hakiki katika usawiri na uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Wasanii wanaotumia uhalisia wanapendelea kuumba wahusika, mandhari na matukio ya kawaida au yanayoweza kuonekana wazi na kukubalika katika jamii husika. Kulingana na Njogu na Wafula (2007) uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri matukio na masimulizi ya kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha katika jamii. Neno uhalisia humaanisha kuwa watunzi katika sanaa wanabuni wahusika ambao usimulizi na matendo yao yanachochewa kuambatana na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka.

Hapo awali Wamitila (2003) alifasili kuwa riwaya za kimajaribio zinatia kiwewe kwa wasomaji jambo ambalo ni shida kufahamu malengo ya watunzi kutokana na masimulizi ya kutatanisha yanayotekelezwa na wahusika wa kimazingaombwe. Watunzi wa riwaya za kimajaribio wanaweza kutumia mbinu ajabuajabu katika uwasawiri wa wahusika na kusababisha uwasilishaji wa ujumbe kwa njia dhahiri au isiyokuwa dhahiri. Masimulizi

yanadhihirishwa na kuendelezwa kwa njia za kimazingaombwe zilizo tofauti na njia za kijadi.

Waandishi wengine hapa Afrika Mashariki ambao wamewahi kutumia mbinu za kimapokeo katika kazi zao za kisanii hapo awali, mwishowe walikiuka desturi za kijadi na wakajipata wakithamini uandishi wa kimajaribio. Mmoja wa wasanii hao akiwa Ngugi wa Thiong'o (2005) hasa katika riwaya yake ya '*Wizard of the Crow*' (2005) yenye masimulizi maajabu. Katika riwaya yake ya *Murogi wa Kagogo* (2004) tunapatana na matukio ya kimazingaombwe kwa mfano, Thiong'o anavyosawiri mhusika mmoja wa kifantasia wakati moja alipokuwa akiongea, sauti yake ilikuwa ikisikika ikitoka ndani ya kioo kwa njia ya kushangaza lakini mhusika mwenyewe haonekani. Wamitila pia katika riwaya zake *Bina–Adamu* (2002) na *Musaleo* (2004) amewasilisha kazi zake kwa njia ya kifantasia kimakusudi, kwa kutaka kuyaangazia upya mambo ya kijamii yanayofanyika kwa njia ya kiajabu.

Riwaya hizi za kimajaribio zinaasisi misingi mipya ya uhusika na usawiri na hata kubadilisha dhana nzima ya mhusika. Kwa mfano, kuna waandishi watangulizi wa uwanja huu wa utunzi mpya miongoni mwao ni Topan (1970) katika tamthilia ya *Aliyeonja Pepo* pamoja na Hussein (1971) katika tamthilia ya *Mashetani* waliobuni wahusika katika kazi zao kwa njia ya kimazingaombwe. Hata ingawa waliweza kubuni hali za kimazingaombwe, Nyabunga (2005) anasema kuwa watunzi hao wa kimajaribio walifanya hivyo kwa kuiga mitindo yao kutoka malighafi ya utamaduni wa kimarekani kusini na kiafrika ambapo inajulikana tangu kale kuwa dhana za miungu, mashetani, pepo na nyinginezo zimekuwepo katika jamii mbalimbali.

Hii ni ishara kuwa watunzi katika riwaya za kimajaribio wako huru kuteua mbinu zao za usawiri zinazoambatana na mawazo walizonazo katika mipangilio yao bila kujifunga kwa kanuni maalum za uandishi jinsi ilivyo desturi katika fasihi za kijadi. Wahusika wa kimazingaombwe ndilo kundi linalotawala riwaya nzima kwa sababu hata wengi wa wahusika wa kihalisia wanasawiriwa kutekeleza masimulizi yao katika mandhari ya kinjozi.

Riwaya hizi za kisasa pia hujulikana kama riwaya mpya za kimajaribio ambazo zinabuniwa kuashiria umazingaombwe ya matukio mbalimbali yanayopatikana katika jamii. Kulingana na Wamitila (2003) dhana "riwaya za kimajaribio" hutumika pia kuelezea riwaya za kimazingaombwe ambazo zinakiuka kanuni au desturi za kawaida katika uandishi wa riwaya za kimapokeo. Aidha Wamitila anafafanua kwamba riwaya mpya pia huitwa riwaya za kimajaribio ambazo zinashughulikiwa na wasanii wa usasaleo wakiwa na lengo la kubuni wahusika wenye ujumbe unaobeba matendo ya kushtua na kutia hofu. Anavyosema Wamitila, waandishi wa aina hii huwa na nia ya kujitenga na mitindo ya kijadi katika uhusika na uandishi wa riwaya.

Katika uhakiki wao wa tamthilia ya *Mashetani*, Njogu na Chimerah (1999) wanatuarifu kwamba Kitaru na Juma wamesawiriwa kucheza mchezo wa binadamu na shetani ili waielewe vizuri hali yao hususan mahitaji katika maisha ya kisasa na mabadiliko ya kiutadawazi. Mtunzi katika mchezo huu anaashiria hali ya kutoafikiana baina ya binadamu (Kitaru) na shetani (Juma). Kitaru akiwa ndotoni, anapatana na maisha ya kikweukweu huku akikumbana na mabishano, mikwaruzano na mikinzano ya kijamii. Kupitia ndoto mtunzi anamwezesha Kitaru kuifahamu mifumo mbalimbali ya kiuchumi na ya kijamii, jinsi inavyomwathiri yeye na jamii nzima. Jambo hili husukuma binadamu kufumbua macho kisha

kulenga kutafuta suluhisho kwa njia moja au nyingine ya kujaribu kutatua matatizo yake. Kutokana na mchezo huu, tunaona jinsi watunzi katika fasihi za kimajaribio wanatumia mbinu za kimazingaombwe kufunua na kuweka wazi mambo anayokumbana nayo binadamu katika jamii husika.

### 2.3 Dhana ya Wahusika

Wahusika ni viumbe wanaosawiriwa kutekeleza uigaji fulani katika kazi ya fasihi kulingana na mawazo ya mtunzi. Shughuli hasa ya mhusika katika sanaa ni kuwezesha uwasilishaji wa ujumbe wa mwandishi kufikia wasimuliwa lengwa. Hivyo basi wahusika ni watenda kazi katika fasihi na huwa vielelezo vya viumbe wanaopatikana katika mazingira yaliyobuniwa na mtunzi.

Mtazamo wa dhana ya wahusika huweza kutofautiana kutegemea utaratibu anaouchukua msanii katika utunzi na kulingana na uteuzi wake wa nadharia ya kazi ya fasihi inayohusika. Wasifu wa mhusika katika fasihi nao unategemea mkabala uliopo katika jamii husika. Utunzi unaoegemezwa katika mitazamo ya kimapokeo au kihalisia unasawiri wahusika kwa namna ambayo hisia zao zinafanana na hisia za mwanadamu wa kawaida katika jamii. Wahusika hao wa kihalisia kwa mujibu wa mtunzi, usawiriwa kwa kutumia nguzo za maisha halisi na kwa kutegemea kanuni za ushabihihikweli za kimapokeo.

Wamitila (2003) anafasili dhana ya wahusika kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi za kifasihi na ambao wanafanana na binadamu kwa kiasi kikubwa. Wamitila anasema kuwa wadhifa wa wahusika unategemea mkabala uliopo katika mpangilio wa mtunzi. Fasihi za kijadi ambazo zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinasawiri wahusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika jamii ya kawaida. Akiendelea

kufafanua, Wamitila anasema kuwa wahusika ni wenzo kuu katika fasihi kwa sababu wao ndio jira ya matukio yote yanayopatikana katika kazi ya fasihi husika.

Kuhusu wahusika wa kimazingaombwe, Alexander (1990) anasema kuwa mbinu zinazotumiwa katika uhusika unaohusisha umazingaombwe wa wahusika huwa kielelezo cha jinsi nadharia ya kiusasaleo inavyotuelekeza. Alexander anasisitiza kuwa wakati umefika kufikiria upya mwelekeo katika fasihi utakaoafiki mahitaji ya kisimulizi katika maisha ya jamii ya kisasa ambayo hayafikiwi tena kupitia fasihi za kimapokeo. Alexander anasema kuwa ni bora pia kuangazia njia mwafaka ya kuelezea maana ya mambo kadhaa yanayounganishwa katika uwasilishaji wa kimazingaombwe inayoleta utata kwa wasimuliwa katika kushika ujumbe lengwa.

Wahusika wa kihalisia kulingana na Abrams (1999), wanaumbwa na kupewa sifa zinazohusishwa na binadamu katika maisha ya kila siku katika jamii husika kisha kuna wahusika dungudungu ambao wanahusishwa na matukio ya kinjozi. Abrams anasema kuwa wahusika wa aina hii wanasawiriwa na kuwekwa katika mazingira ya kimuujiza kisha kupewa sifa za kimazingaombwe na kufanywa kwa kiwango cha juu waingiliane na viumbe wenye maumbo na matukio changamano. Mtunzi anatumia njozi kueleza au kusawiri fasihi ambayo hudhihirisha uwasilishaji wa kiajabu wenye matukio ya kuogofya yasiyokuwa ya kawaida katika jamii.

Njozi ni dhana muhimu katika kazi za kimajaribio na hutumiwa kueleza fasihi ambayo huonyesha uwazaji wa kiwango cha juu cha matukio ya kimazingaombwe. Dhana ya njozi huweza kujumlisha bunilizi za kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kazi za kifantasia

zinazohusishwa na matukio pamoja na mandhari ya kiajabu. Kulingana na maelezo haya, inabainika kuwa kuna makundi mawili makuu ya wahusika, wahusika halisi na wahusika wa kimazingaombwe. Kuna tofauti kubwa kati ya wahusika wa kimapokeo (wa kijadi) na wale wa kimajaribio unaotokana na namna watunzi katika fasihi wanavyotumia mbinu ajabuajabu katika uhusika, usawiri na katika uteuzi wa mandhari katika kazi zao. Watunzi katika fasihi za kimazingaombwe wanasawiri wahusika katika kikundi hiki cha kifantasia kiwe ndicho kinachotawala kazi nzima katika sanaa za kimajaribio.

## 2.4 Dhana ya Uhusika

Uhusika ni kipengele cha msingi katika fasihi kwa sababu ndicho kinachofafanua kila tukio pamoja na mhusika na maendeleo yake jinsi anavyochorwa katika fikra za mtunzi. Njogu na Chimerah (1999) wanafasili dhana ya uhusika wakisema kuwa uhusika ni umithilishaji wa matendo ya viumbe hadithini na vile vya viumbe katika dunia razini. Matukio ya viumbe hao husababishwa kuambatana na mazingira ya ubunifu.

Uhusika wa jadi umejengwa kupitia usawiri wa wahusika kwa msingi wa uhalisi wa kijamii ambapo wahusika wanawakilisha binadamu katika ulimwengu halisi. Wahusika wa jadi au wa kimapokeo wanakaribiana na binadamu wanaopatikana katika ulimwengu halisi. Katika uhusika wa kimajaribio matendo ya wahusika yanasababishwa yawe na maingiliano baina wao wenyewe na mandhari yao, ambayo yanaweza kuwa halisi au yawe ya kimazingaombwe.

Gromov (2002) anafafanua kuwa uhusika katika fasihi za kisasa hutumia mbinu za kuubuni ukweli wa mambo katika maisha kwa njia tofauti ya kusawiri wahusika wa kimazingaombwe. Gromov anaongeza kusema kuwa umazingaombwe ni chombo cha kisasa

kinachotengwa katika fasihi kuzungumzia maswala ya kiusasaleo yanayoshughulikiwa na wasanii wa kimajaribio. Jambo hili limewawezeshea wasanii hao maafikiano stadi na uhuru wa kutumia mbinu zao za kimazingaombwe katika utunzi wao. Watunzi hao wa kimajaribio wamefanikiwa kutekeleza usawiri na usimulizi mwafaka katika jamii ya usasaleo bila kulazimika kuzingatia desturi za uandishi wa fasihi za kijadi.

### 2.5 Dhana ya Usawiri

Msokile (1993) anafasili dhana ya usawiri kama tendo la kimakusudi linalotekelezwa na mtunzi katika fasihi kwa kutumia maneno kuchora picha ama kuunda taswira inayoiga maisha fulani kwa kuzingatia misingi ya namna ya kuishi katika jamii inayohusika. Kulingana na BAKIZA (2010), usawiri ni kitendo cha kuunda sura ya mtu, kitu au jambo akilini kisha kuwasilisha ujumbe huo kupitia maandishi.

Katika kuhitimisha, usawiri wa wahusika katika fasihi ni kitendo cha kuwabuni, kuwafafanua, kuwatambulisha na kuwajenga wahusika huku wakipewa hadhi na uwezo wa kuwasilisha ujumbe kupitia maneno na matendo yanayoambatana na maudhui aliyonayo mtunzi katika kazi husika, Ponera (2014).

Wamitila (2002) anafafanua kuwa mtunzi katika fasihi anaweza kutumia njia kadhaa tofauti katika kuwasawiri wahusika na ana uhuru katika uhusika wa kuteua na kutumia wahusika wa aina mbalimbali watakaoambatana na mahitaji ya kazi yake.

### 2.6 Dhana ya Mandhari

Wamitila (2003) anasema kuwa dhana ya mandhari hurejelea wakati na mazingira ya utendaji au usimulizi unaochorwa na mtunzi katika fasihi. Wamitila anaeleza upana wa dhana ya mandhari akisema kwamba mandhari katika fasihi si mazingira tu bali hurejelea mambo

mengi yakiwemo eneo, jamii, elimu, mila, desturi na itikadi. Wamitila anasisitiza kuwa mandhari pia huchangia katika kueleza masuala mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika katika sanaa na yanaweza kuhamishwa katika mazingira tofauti tofauti kulingana na muktadha lengwa.

Njogu na Chimerah (1999) wanafasili dhana ya mandhari wakisema kuwa mandhari ni makazi maalumu yanayojengwa na mtunzi kisha kuwaweka wahusika wake na kuwapa uwezo wa kutekeleza masimulizi na matukio mbalimbali ya kifasihi. Kwa hivyo mandhari ni mazingira ya wahusika pamoja na matukio yao na ni kipengele muhimu katika kazi za kifasihi ambacho kinadhibiti wahusika hao.

Pamoja na juhudi kubwa zilizofanywa na wasanii tangulizi katika kazi za kimajaribio, inabainika kuwa matukio na masimulizi katika kazi zao hayajaweza kuashiria malengo tuliyonayo katika utafiti wetu. Ni kwa sababu hii Hough (1962) anasema kuwa hakuna kazi yoyote ya uhakiki iliyokamilika wakati mmoja na ikawa ndio ukomo wa utafiti. Hough anasisitiza kwamba utafiti hutegemea historia na mazingira ya kijamii katika kila kipindi kipya cha historia. Kama tunavyofasiri maandishi mapya, ndivyo fasihi za wakati uliopita zafaa kufasiriwa upya jinsi zinavyobadilika na kuchukua mwelekeo mpya.

Utafiti wetu umehitaji kutathimini umazingaombwe katika uwasilishaji wa wahusika, uhusika na kwa uteuzi wa mandhari katika riwaya za kimajaribio za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka*. Hivyo basi kutokana na maelezo hayo, tunakusudia kuchambua masimulizi ya aina mbalimbali ya wahusika waliosawiriwa kusababisha uwasilishaji wa kimazingaombwe kwa kuzingatia misingi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe.

## 2.7 Uwasilishaji wa Umazingaombwe

Mbatiah (2002) na Wamitila (2003) wanasema kuwa uwasilishaji wa umazingaombwe ni namna fulani ya kueleza uhalisi unaotuzunguka kwa njia mpya huku watunzi kukita hadithi zao katika ajenda za kijamii ya kisasa ambazo zinaathiri maoni ya kiutandawazi katika mataifa mbalimbali na viongozi wao.

Kuibuka kwa uwasilishaji wa kimazingaombwe katika riwaya za kimajaribio kumeibua pia hali borongo katika jamii kutokana na mitazamo ya wasomaji mbalimbali wakosao kupata masimulizi kwa njia wazi huku wakishindwa kuamini ama kutoamini mambo wanayoyasoma. Mambo hayo ni kama vile uchangamano wa matukio ya ufu, uhai, uchawi na wakati nyingine kukosekana kwa mipaka wazi kati ya mandhari au matukio halisi na yale ya kimazingaombwe.

Chanzo cha baadhi ya mambo hayo ya umazingaombwe hasa ni watunzi kadhaa kukiuka matumizi ya mitindo ya uandishi katika fasihi za kijadi. Hii ni kwa sababu ya utunzi huu wa kiuhalisia kutoweza kuwapa wasanii hao uwezo wa kubuni wahusika wanaoweza kutekeleza uwasilishaji wa kimazingaombwe na kuafikia malengo waliyonayo mawazoni mwao.

## 2.8 Misingi ya Nadharia

Tumetumia nadharia ya Uhalisiamazingaombwe katika uchanganuzi wetu. Nadharia hii pia hujulikana kama uhalisiajabu. Walibora (2010) akiunga mkono Abrams (1999) anaelezea kuwa dhana ya umazingaombwe hapo mwanzoni ilitumika katika sanaa za uchoraji tu. Badaye wasanii katika fasihi waliweza kuambatanisha sanaa za uandishi na zile za uchoraji kwa mpangilio wenye utaratibu maalum kulingana na hali katika jamii inayobadilikabadilika

kila uchao. Sanaa za uchoraji wakati huo zilitumika katika kupasha habari fulani katika jamii kupitia michoro ya kifantasia ambayo watu hutazama na kupata habari lengwa.

Roh (1925), mwanzilishi wa nadharia hii, anasema kuwa umazingaombwe ni uwasilishishaji wa ujumbe wenye uwezo wa kubainisha na kufichua hali ya uajabu unaoashiria miujiza iliyomo kwenye uyakinifu wa maisha ya kila siku katika jamii husika. Katika hali hii, watunzi wa kimazingaombe husawiri wahusika waweze kutekeleza na kuweka wazi matukio ya kimazingaombwe yanavyodhihirika katika jamii. Jambo hili huingiza wasomaji katika ulimwengu wa kinjozi huku wakichanganyikiwa bila kupata masimulizi kwa ukamilifu.

Kwa muhtasari Roh anasema kuwa umazingaombwe ni uwasilishi wa ujumbe unaodhihirisha hali ya kimazingaombwe ilivyo rohoni au mawazoni mwa mtunzi kwa kuwasawiri wahusika kubainisha na kung’amua mambo ya kifantasia na kisha kudhihirisha mambo hayo katika uwasilishaji wao. Katika hali hii, umazingaombwe unaowakilishwa kama uhalisi unaotuingiza katika ulimwengu wa kinjozi. Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa Franz Roh alitumia mtindo wa kimazingaombwe katika muktadha wa kisanaa akiwa na nia ya kudhihirisha uwepo wa usawiri wa aina fulani ya uajabu uliomo kwenye uhalisi uliozoeleka katika jamii.

Khamis (2005) anazungumzia uwezekano katika riwaya za kisasa kuchukua kwa kiwango kikubwa sura mpya wenye umazingaombwe katika usawiri wa wahusika. Khamis anazidi kueleza kuwa kuna mvuto wa mbinu za kimajaribio kama inavyobainika katika riwaya za kisasa. Allende (1985) naye akiangazia jamii inayopitia mabadiliko katika maisha aliandika kazi zake za kwanza kwa kutumia mtindo huu wa umazingaombwe katika riwaya yake

aliposawiri mhusika kwa jina Rosa kwa njia ya kimazingaombwe. Rosa amesawiriwa kuwa na nywele za kijani kibichi na uso wenye rangi ya manjano tangu kuzaliwa kwake, jambo ambalo wakati ule lilikuwa la kiajabu lakini katika jamii ya kisasa labda si jambo la kimazingaombwe tena.

Mbatiah (2001) akielezea kuhusu umazingaomwe katika fasihi anafafanua kuwa dhana ya umazingaombwe inatumiwa kwa kiasi kikubwa kuelezea mkondo katika uandishi ambapo matukio ya uhalisiamazingaombwe yanaelezwa kwa njia linganifu kana kwamba ni mambo ya kawaida. Hawthorn (2001) na Wamitila (2008) nao wanasema kuwa matendo ya wahusika yanaweza kutuelekeza katika kuelewa hisia zao, kero zao, ndoto zao au hata udhaifu wao. Wasanii wanaotumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kimazingaombwe, nguzo au kiini cha wazo hutokana na maisha ya kawaida ya jamii inayohusika na pia kulingana na yaliyomo mawazoni mwa mwandishi. Watunzi wanaotumia mbinu za umazingaombwe katika kazi zao wana mitazamo na imani tofauti tofauti za kimsingi na kwa hivyo wanatumia sifa zinazobainisha kazi zao kulingana na imani ya kila mmoja wao.

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa umazingaombwe ni nadharia ambayo kwa kimakusudi inakiuka sifa za uhalisia ambazo zilikuwa zikitumiwa na wasanii wa nyakati za karne ya kumi na tisa katika fasihi za kimapokeo. Kwa muhtasari, sifa za kiuhalisia hujenga taswira katika fasihi inayoashiria matendo ya mwanadamu wa kawaida katika jamii halisi. Katika hali ya kimazingaombwe, matukio na masimulizi ya kiuhalisi na kinjozi huchanganyika. Hii ni kusema kwamba hakuna mipaka ya uhalisi na utohalisi katika fasihi za kimazingaombwe. Kwa mfano mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa kwa sababu

wana-uhalisiamazingaombwe wanajadili mambo mbalimbali yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila ya kujikita katika mazingira finyu kama vile ya jamii, taifa, nchi au bara fulani.

Katika fasihi ya kimajaribio wakati hufupishwa, mwanda hupanuliwa na uhusiano baina ya mahali au mandhari na wakati wa matukio huvunjwa. Mipaka ya kijadi baina ya nyakati pia huvunjwa kiasi kwamba matukio hayafuati kaida ya uhalisi wa kiwakati. Katika mtazamo huu wakati unafungamana na suala la njozi mara kwa mara. Katika hali hii, mtunzi katika usawiri huweza kueleza mambo yanayomkumba binadamu kabla ya kuzaliwa na baada ya kifo. Uwanda wa kisimulizi pia hupanuliwa na huweza kuhusisha hali katika ulimwengu halisi, ulimwengu wa kidhanifu au wa kinjozi na maingiliano kati ya aina hizo tofauti huvunjwa.

Warnes (2006) anasema kuwa waandishi wa riwaya za kijadi hapo awali hawakuikuza sana dhana ya uhalisiamazingaombwe. Huenda ikawa hii ni sababu ya Franz Roh (1925) kuaminika kuwa ni yeye aliyepata msukumo kuitumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe kama mwasisi wa istilahi hii. Aliamua kubadili mkondo kulingana na mtazamo wake wa kifasihi ili kuweko na mapatano ya mambo katika jamii ya kisasa inayokumbwa na mahitaji mbambali yanayotokana na maendeleo ya kiutandawazi.

Walibora (2010) anasema kuwa utunzi katika kazi za kimajaribio unawezesha usawiri wa wahusika kwa njia ya kiajabu unaokiuka mbinu za utunzi katika riwaya za kimapokeo. Walibora, akiwaunga mkono Khamis (2005) na Williams (1999) anasema kwamba uandishi wa kimajaribio unachukua mkondo katika sanaa za Kiswahili ambao unalenga kushughulikia mambo yanayojitokeza katika jamii ya sasa. Williams naye anaongeza

kusema kuwa mikakati ya kimajaribio katika fasihi hudhamiria kuakisi ukosefu wa uthabiti katika michakato ya kiutandawazi (ukiwemo uhalisiamazingaombwe) katika jamii. Aidha, kuibuka kwa riwaya za kimajaribio kumebadili hali iliyokuweko hata zaidi. Hivi basi, baadhi ya waandishi wa lugha ya Kiswahili kama vile Said Ahmed Mohamed na Tom Olali wameegemea mkondo huu wa kiuhalisiamazingaombwe katika usawiri wa wahusika katika kazi zao.

### 2.9 Hitimisho

Sura hii inashughulikia mapitio ya kazi tangulizi zinazoambatana na mada ya utafiti wetu. Tumejadili dhana ya mhusika na kufafanua kwa ufupi shughuli za wahusika katika fasihi za Kiswahili. Tumeangazia wahusika wa kimazingaombwe waliosawiriwa katika riwaya tulizozishughulikia. Tumefafanua wahusika hao hususan makundi na aina mbalimbali wanaopatikana katika sanaa za kimajaribio kisha kuchambua matini mbalimbali yaliyoadikwa na wasanii waliotangulia kuhusu fasihi za kimajaribio. Maandishi hayo ya awali yanatuwezesha kutambulisha upungufu ulioko katika fasihi za kijadi hasa katika uwasilishaji wa ujumbe. Jambo hili ndilo lililowafanya baadhi ya waandishi waliozoea mtindo wa uhalisia kuhamia utunzi wa kimazingaombwe katika uhusika na usawiri wa wahusika pamoja na uteuzi wa mandhari katika kazi zao. Hatimaye, tumechanganua uwasilishaji wa umazingaobwe unaotekelezwa na wahusika wanaopatikana katika riwaya zetu teule za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka.*

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inajikita katika ufafanuzi wa vipengele muhimu ambavyo vinahusu mbinu ambazo ni lazima tuzingatie kwa utaratibu uliorasmi. Mbinu za utafiti zitatuwezesha kujenga kazi ya utafiti wetu kwa njia halali na ithibati timilifu. Mbinu zilizoshughulikiwa ni pamoja na muundo wa utafiti, njia ya kukusanya data, uteuzi wa sampuli, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa data na maadili ya utafiti.

### 3.1 Muundo wa Utafiti

Enon (1998) amefafanua kuwa muundo wa utafiti ni njia na taratibu maalumu ambayo unapaswa kufuatwa na mhakiki au mtafiti wakati wa ukusanyaji wa data kulingana na aina ya utafiti wake. Kothari (2004) naye anafasili muundo wa utafiti kama jumla ya mbinu zinazotumika wakati wa kufanya uchunguzi wa jambo lengwa kwa kuzingatia hali ya umakini na mantiki wenye mtiririko wa fikra za mtunzi kwa lengo la kufanikisha kazi husika. Kothari anasema muundo ni umbo la utafiti na hujulikana pia kama usanifu wa utafiti na ni jumla ya taratibu, mpango na hatua maalum anazozifuata mtafiti anapoendelea na zoezi lake la kukusanya data kulingana na mada halisi ya utafiti wake.

Mbinu kuu iliyotumiwa ni uzingatiaji wa matini mbili za utafiti, yaani riwaya teule za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.* Kadhia kuu ilihusu kuzisoma na kuzipitia mara kadhaa kwa azma ya kubainisha namna waandishi walivyotumia fikra ya umazingaombwe, na hasa katika ujenzi na uwasilishaji wa wahusika muhimu wa riwaya hizo. Mapitio haya ya riwaya teule kishayalirutubishwa na mapitio ya ziada  kutoka maktabani na mtandaoni ambapo

matini kadhaa zinazohusiana na mada zilisomwa. Hivyo basi tumesoma kwa undani majarida, makala na tasnifu mbalimbali zitakazojadili vipengele vya uwasilishaji wa wahusika na uhusika wa kimazingaombwe.

### 3.2 Uteuzi wa Sampuli

Kwa kuzingatia mada, nadharia tete na malengo ya utafiti wetu, tumetumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Adam na Kamuzora (2008) wanasema kuwa mbinu ya usampulishaji lengwa pia inajulikana kama usampulishaji wa kimakusudi na ina manufaa makubwa katika fasihi kwa sababu mtafiti yuko huru kuchanganua na kupata data za uhakika tena kwa muda mfupi. Mugenda (1999) anaeleza kuwa mbinu ya uteuzi wa sampuli kimakusudi ni mbinu ambayo inawawezesha watafiti kuchukua data kutoka kwa watafitiwa kulingana na malengo na madhumuni ya utafiti wao. Aidha, Bryman (2004) anafafanua usampulishaji akisema kuwa uteuzi wa sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha watu, vitu au matini ili kitumike katika kazi za kiutafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa. Kothari (1990) anaeleza kuwa sampuli ya watafitiwa ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa za kundi zima ambalo huwawezesha watafiti katika fasihi kupata habari kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wao.

Babbie (1999) naye amefasili dhana ya sampuli kuwa ni kundi dogo la watafitiwa ambalo limechaguliwa katika kundi kubwa kwa lengo la kutoa data za kuwakilisha kundi zima. Babbie anaeleza kuwa usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti kimakusudi ambapo mtafiti huteua sampuli fulani ya vitafitiwa vyake akiamini kuwa sampuli hiyo ni sahihi na ndiyo itakayompa data sahihi za kuweza kuafiki malengo ya utafiti wake.

Mbali na *Babu Alipofufuka*, mwandishi Said Ahmed Mohamed ameandika riwaya kadhaa zikiwemo *Utengano, Asali Chungu, Tatat za Asumini, Dunia Mti Mkavu, Dunia Yao,* na *Nyuso za Mwanamke.* Tom Olali naye ni mwandishi chipukizi ambaye anafahamika katika ulingo wa uandishi wa riwaya kupitia riwaya yake ya awali ya *Mafamba.* Uteuzi wa riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* umefanywa kimakusudi kwa kuzingatia kipengele cha kupatikana kwa wingi wahusika wanaoshamiri sifa za umazingaombwe. Katika riwaya hizi, ndimo mnamopatikana wahusika wasioyumkinika katika maisha yetu ya kawaida. Kwa mfano, humu ndimo mnamopatikana wafu wanaoweza kudhihiri riwayani na mara wakapotea. Wafu hawa, tofauti na maisha halisi wana uwezo wa kujitokeza na kuwasemesha wahusika walio hai, tofauti na ilivyo katika maisha halisi.

### 3.3 Njia za Kukusanya Data ya Utafiti

Data za utafiti huu zitakusanywa kwa kutumia mbinu ya kimaktaba. Kulingana na Kothari (1990) dhana ya kukusanya data ni zoezi muhimu katika utafiti wowote ule wa kifasihi ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa anazozikusudia ili kufanikisha lengo la utafiti wake. Kothari anasema kuwa mbinu za kimaktaba zinalenga kutoa fursa kwa watafiti kuchanganua kwa kina kazi mbalimbali maktabani. Hiyvo basi tumekusanya data zetu kwa kutumia mbinu hii ya kimaktaba na usomaji matini wa riwaya zilizoteuliwa.

Upekuzi wa kina umefanywa kwenye tovuti mbalimbali mtandaoni. Tumesoma majarida na vitabu vyenye maandishi tofauti tofauti yanayohusiana na utafiti wetu ili tupate vigezo na habari muhimu kuhusu suala la uhusika na uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe. Riwaya zilizoteuliwa za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka* zitasomwa na data kudondolewa na kuchambuliwa kulingana na malengo ya utafiti.

Wahadhiri wetu pamoja na wanafunzi wenzetu walishirikishwa katika mijadala na tukaweza kupata ushauri wao kila ilipohitajika. Mkazo umewekwa kwenye vipengele vya usawiri na uhusika vinavyochochea uwasilishaji wa kimazingaombwe katika riwaya zilizoteuliwa. Data yote itachanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe.

### 3.4 Uchanganuzi wa Data

Mbinu ambazo tumeyotumia katika kuchambua data za utafiti wetu ni ile ya uchanganuzi matini ambapo data itapangwa kupitia njia ya kimaelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Kombo na Tromp (2006) wanasema kuwa uchanganuzi wa data ni mchakato wa uhakiki wa taarifa iliyokusanywa kwa kutoa maelezo yatakayoafiki malengo ya utafiti lengwa. Kombo na Tromp wanaeleza kwamba uchambuzi huu ni kitendo kilicho rasmi ambacho watafiti hukitumia baada ya kukusanya data za utafiti kutoka katika vyanzo husika kwa lengo la kuzichanganua ili kupima uhalali wa matini yatakayopatikana kwa mujibu wa mada ya utafiti.

Kulingana na Kothari (1990) uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu ya uchanganuzi wa data ambapo mtafiti huzichanganua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake. Tumechanganua vigezo vya uwasilishaji wa aina na makundi mbalimbali ya wahusika katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka.* Aidha katika uchambuzi wetu, tumezingatia matumizi ya sifa bainifu za nadharia teule katika kutathmini mbinu za usawiri wa wahusika tukihusisha malengo ya utafiti wetu. Kutokana na maelezo ya waasisi na wataalamu mbalimbali, utafiti wetu umeongozwa na mahitimisho yafuatayo mintarafu ya wahusika wa kimazingaombwe katika riwaya zilizoteuliwa:

1. Njozi katika fasihi za kimajaribio hufungamana na sanaa za kijadi kama vile visasili, yaani hadithi zinazoeleza asili ya watu fulani. Uwasilishaji wa wahusika wa

kimazingaombwe huzua hali ya kushtua, kushangaza na kuogofya wala hauna mtiririko kama ilivyo katika riwaya za kimapokeo.

2. Matukio ya uhalisia yanachanganyika na yale ya umazingaombwe hivi kwamba kutofautisha wazi ni vigumu. Matukio ya wahusika hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida na huwepo mvunjiko katika usimulizi. Watunzi huweza kujenga wahusika wenye nafsi mbili kwa kutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi na mtiririko wa urazini mawazoni mwao. Sifa wanazopewa wahusika hao hukuzwa kuashiria umazingaombwe.
3. Ndoto na uhalisi vinachanganyika. Ndoto ni fikra au mawazo ya kimazingaombwe yanayodhiririka katika ubongo wa mhusika. Malcolm (1959) anasema kuwa ndoto ni mtiririko wa mawazo dhanifu akilini ya mwa mtu ambaye yuko macho au amelala na husafirisha tabia na sifa zake. Malcolm anaeleza kuwa mawazo hayo huambatana na taswira za matukio, ukisiaji, maono, fikra za uwongo, malengo, matarajio na matamanio katika maisha ya anayeota na vilevile picha halisi ya mambo anayowaza kuonekana.

### 3.5 Uwasilishaji wa Data

Matokeo ya utafiti wetu yamewasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Maelezo haya yamezingatia ufafanuzi wa uwasilishaji wa wahusika, uhusika na mandhari ya kimazingaombwe kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Ruwaza maalum zinazojitokeza katika riwaya zote mbili zimepangwa pamoja na kujadiliwa katika mada kuu sa sura ya nne.

### 3.6 Maadili

Katika utafiti wetu tumeamili haki zote za kimaadili na kuzingatia misingi yote ya utafiti. Sture (2010) anafafanua kuwa dhana ya maadili ni miongoni mwa masuala muhimu ambayo

mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito mkubwa wakati wote wa utafiti wake. Sture anafasili dhana ya maadili kama mwenendo wa kuzingatia onyo au mafundisho mtafiti yeyote anafaa kutilia maanani kutoka mwanzo hadi kukamilisha na kuwasilisha matokeo ya utafiti wake.

Mathooko (2007) anasema kuwa maadili ni kaida ambazo zinaelekeza tabia zetu ziweze kuleta utangamano na maafikiano ya watu katika maisha ya kila siku katika jamii. Mathooko anaeleza kwamba dhana ya maadili ni uwajibikaji na uelekevu wa mienendo ya wote tunaotangamana nao katika kazi za utafiti kwa malengo ya kuwa na uhusiano na ushirikiano wa hiari. Anol (2012) anasema kwamba mtafiti yeyote anapaswa kutilia maanani maadili ya utafiti anaposhughulikia utafiti wake. Baadhi ya masharti hayo kwa mfano ni kupata idhini kutoka Chuo kikuu anachosomea mtafiti kabla ya kuenda nyanjani kukusanya data za utafiti.

### 3.7 Hitimisho

Vipengele vinavyozingatiwa katika sura hii vinahusu mbinu za utafiti. Imedhihirika kupitia kwa mifano iliyodondolewa kutoka kazi za waandishi tangulizi kwamba muundo wa kimaelezo umefaa katika kukusanya, kuchambua na katika uwasilishaji wa data za utafiti wetu. Uteuzi wa sampuli umezingatia mbinu za usampulishaji wa kimakusudi. Aidha sifa bainifu za maadili ya utafiti zimeagaziwa na ni wajibu wetu kuzidumisha.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI WA WAHUSIKA NA UHUSIKA WA KIMAZINGAOMBWE

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii utafiti wetu umebainisha vipengele vya uwasilishaji wa wahusika na uhusika wa kimazingaombwe kama vinavyojitokeza katika riwaya za *Watu wa Gehenna (2012)* ya Tom Olali na *Babu Alipofufuka (2001)* ya S. A. Mohamed. Tunanuia pia kuchunguza jinsi watunzi katika riwaya hizi teule walivyotumia mbinu za kiajabu katika usawiri unaohusisha ujenzi wa wahusika ambao wanaweza kubadilikabadilika na kuchukuwa nafsi zaidi ya moja na kutekeleza kazi tofauti tofauti katika uwasilishaji wa ujumbe. Katika kufanya hivi, tunachanganua umazingaombe katika masimulizi kwa kiwango cha wahusika na uhusika wao mandhari za kimazingaombwe ambapo matukio ya kinjozi yanadhihirika katika riwaya zilizoteuliwa.

Katika uchunguzi huu, tumebainisha dhima za wahusika wa kiajabu pamoja na sifa zao ambazo zinazowafanya waonekane viumbe wasio wa kawaida katika ulimwengu halisi na kwamba wahusika hao huwa nguzo kuu ya kuendeleza hadithi katika fasihi. Kulingana na Wamitila (2003), dhima ni dhana inayotumiwa kuelezea wajibu wa wahusika katika kazi za kifasihi. Wamitila anasema kuwa mtunzi katika sanaa anatumia mbinu yoyote katika kuwakilisha ujumbe wake kimakusudi ili kutimiza azimio lake kwa wasimulizi wake lengwa.

Kutokana na migogoro ya wahusika wanapotagusana na wahusika wengine, tumebainisha umaarufu na umuhimu wao kwa kuadabisha na kuonyesha sifa bainifu za kimazingaombwe na jinsi zinavyodhihirika katika riwaya zilizoteuliwa. Uhusika usiozoeleka unajengeka

kwenye uhalisiajabu ambapo uwasilishaji wa ujumbe unawakilishwa na aina mbalimbali ya wahusika wa kifantasia waliosawiriwa kisha kuwekwa katika mandhari ya kimiujiza.

Katika kuangazia kipengee cha mandhari, tumebaini mahali kama panapojengwa na watunzi na mnamotukia matukio ya aina yoyote yawe kihalisia au ya kinjozi. Tumeangazia pia njozi kama mandhari ambayo yamechukua kiwango kikubwa katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka*. Hatimaye, sura imeangazia wahusika mahususi wanaojitokeza katika riwaya teule na jinsi uhusika wao unavyoendeleza dhana ya umazingaombwe.

### 4.1 Swala la Wahusika, Uhusika na Mandhari

Mandhari au mazingira katika uwasilishaji ni mahali katika jamii wanamojikuta wahusika kulingana na mbinu za usawiri na mpangilio wa mtunzi. Katika kuzungumzia usawiri wa aina mbalimbali ya mazingira, Wamitila (2003) anaeleza kuwa mandhari ni sehemu au mahali ambapo wahusika hutekelezea matukio yao. Wamitila akifafanua zaidi, anasema kuwa dhana ya mandhari pia hutumiwa katika kuwakilisha wakati fulani ambapo kazi katika sanaa husimuliwa au matukio kufanyika. Hivyo basi, mandhari ni sehemu muhimu kabisa hasa katika uwasilishaji wa ujumbe wa wahusika wa kimazingaombwe.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa mandhari ni makazi maalumu yanayojengwa na mtunzi na mnamotukia matukio mbalimbali yanayotekelezwa na wahusika. Waandishi wanaozingatia mbinu za usawiri wa kimazingaombwe katika kazi zao, wanabuni mandhari ajabuajabu kisha wabuni wahusika wenye matukio ambayo hayafuati sheria zozote kama ilivyo kawaida katika fasihi za kimapokeo. Zaidi ya hayo, wasanii katika kazi za kimajaribio

hutumia mbinu za kinjozi katika usawiri wa wahusika wao ambazo zinafikiriwa akilini mwo bila kuzingatia utaratibu wowote wa fasihi za kijadi.

Kutokana na maelezo haya, tumepata kuwa mandhari katika kazi za kimaazingaombwe ni nguzo muhimu katika uhusika na kwamba mazingira hubuniwa ili kuwapa wahusika uwezo au jukwaa ambako wanaweza kutekelezea matendo yao ambayo yanafungamana na mazingira hayo. Ufahamu wa mandhari umetusaidia kuchanganua wahusika na hata kukagua picha inaypodhamiriwa kujengeka mawazoni mwa wasomaji kuhusu tabia zao, hisia zao, imani yao, na hata maumbile yao.

### 4.1.1 Wahusika, Uhusika na Mandhari ya Kimazingaombwe katika *Babu Alipofufuka*

Katika kuangazia umazingaombwe wa wahusika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* kunapatikana uwasilishaji wa wahusika unaofanyika katika mandhari yaliyochanganyika hivi kwamba kuna mandhari ya kiuhalisia na vilevile kuna mandhari ya kimazingaombwe ambapo kwa wakati mwingi ni vigumu kutofautisha au kubainisha mipaka ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa kinjozi.

Mandhari yenye matukio ya kustaajabisha husawiriwa ili kuwakilisha umazingaombwe wa aina fulani katika hali ya uwasilishaji wa kawaida lakini ya ajabu ni kwamba tunapata mambo yanayofanyika kinyumenyume. Kwa mfano, katika mandhari yenye watu matajiri tunamowaona wahusika wa tabaka la watu waliofukarika na wasio na mali wakichanganyika na wale wa kimwinyi ilhali katika mandhari ya kimaskini, kwenye watu waliodhalilika ndimo tunawakuta matajiri humo humo. Tunapata pia mchanganyiko wa wahusika waliosawiriwa wawe na uwezo wa kubadilisha nafsi zao mara kwa mara na kujiingiza

katikati ya wafanyi kazi wa nyumbani, walinzi na wengineo vilevile kuingia katikati ya matajiri huku wakitekeleza matukio ya kimazingaombwe bila kutambulika.

Katika uchanganuzi wetu, tuligundua kuwa kuna mandhari yaliyochanganyika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* hivi kwamba kuna mandhari ya kiuhalisia na ya kimazingaombwe, ambapo inakuwa vigumu kutambua na kubainisha mipaka ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa kimazingaombwe. Tumepata kujua kwamba watunzi hubuni mandhari ya kimazingaombwe ili kuwakilisha umazingaombwe fulani katika ulimwengu wa kawaida. Kwa mfano, mwanzoni mwa riwaya yanapatikana mandhari yenye masimulizi ya kiuhalisia ambapo mhusika K anaanza maisha yake katika mandhari halisi na kisha kubadilika na kuingia katika mandhari ya kinjozi, na kurejea tena katika mazingira halisi. Mandhari haya yameonekana yakibadilika vivyo hivyo kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Umazingaombwe wa wahusika katika riwaya nzima umedhihirika kufanyika mara kadhaa kuanzia wakati Mzuka, babu yake K, alipomwingilia na kumtatiza kwa kila hali katika maisha.

Tunampata mhusika K katika nyumba yake ya kifahari anafuga mbwa wake anayependa kumwita “Doggi.” Mhusika Biye pamoja na watumishi wengine wana jukumu la kumlisha mbwa huyo kwa kumpelekea chakula kila siku wakati wa jioni kwenye chumba chake. Katika mandhari haya yanayooneka kama ya kihalisia, matukio ya kustaajabisha yanafanyika, kwani kwa muda unaozidi mwezi mzima, chakula cha doggi kimekuwa kikitoweka kila mara anapoletewa na watumishi na anayeondoa chakula hicho hajulikani. Katika hali ya kimazingaombwe, babu Mzuka ndiye anayechukua chakula hicho cha doggi kimakusudi mara tu anapoletewa bila yeye kuonekana na mtu yeyote. Mzuka anakichukua chakula hicho

na kuwapatia majirani akisema haoni kuwa ni jambo la maana mbwa ale chakula kizuri huku watu wakilala njaa kijijini. Mzuka wakati huo huo amekasirika akinung'unika kuwa wakati wa akina babu yake, mbwa walikuwa wakipewa chakula tu kilichobakia baada ya watu wote kula na kushiba (uk.2).

Mhusika K anawalaumu watumishi wake akidhani wao ndio wanaofanya kitendo hiki cha kuchukuwa chakula cha mbwa wake. Ni jambo hili linalomfanya K kuwafuta kazi wafanyi kazi wake kila mara na kuajiri wengine wapya lakini hili halikuwa sulihisho kwani kutoweka kwa chakula cha doggi kukawa jambo la kuendelea. Riwaya, kwa njia ya kipekee inatumia tukio hili la kiajabu kukashifu matendo haya ya kibadhirifu ya kuwajali wanyama zaidi na pia kutoa funzo kwa viongozi waovu katika jamii wanaodhulumu wananchi maskini bila kujali hali yao ya kimaisha.

Mzuka, babu yake K, anasema kuwa viongozi hao wabaya pamoja na matajiri wengine katika jamii kama vile K anaowajali wanyama zaidi kuliko wananchi waliowapigia kura. Katika kumwaadhibu K, Mzuka anamtaabisha kwa kusababisha matukio ya kimazingaombwe kumsibu K akiwa pekee yake katika kasri lake. K anapatwa na kikohozi kikali kinachomghadhabisha, mara moyo kuelea, mara tumbo kumsokota likingurumanguruma na kutoa sauti ya mnung'uniko.

Baada ya mhusika huyu K kujizoazoa kwa muda msalani, anajipata ameenezwa uchafu kila mahali mwilini mwake na ghafla masikio yake yanazibwa na kicheko kizito kinachokuja kwa njia ya kitashtiti. Ni umazingaombwe kuwa kicheko anachokisikia kina sauti kama yake mwenyewe lakini anashangaa kinatoka wapi na ni vipi anaweza kujicheka mwenyewe (uk.8).

Matukio mengine mengi ya kimazingaombwe yalizidi kumwandama kila mara hasa anapokuwa katika hali ya wasiwasi au wakati ameshikwa na hamaki.

*Babu Alipofufuka* inatumia wahusika wa kimazingaombwe kukashifu ubinafsi wa viongozi wanaofayia watu rabsha na kutojali kuondoa uovu ulioenea kote katika jamii. Watu wanaowakilishwa na mhusika K ndio wanaosababisha uozo huu wanapopandishwa vyeo au wanapopata nafasi za uongozi. Ndivyo Babu Mzuka anamaka akishangaa na kujiuliza ni kwa nini K, mjukuu wake, aweza kuketi katika meza moja na viongozi ambao miaka michache iliyopita ilikuwa mwiko kukaa nao, (uk.9-12). Babu Mzuka anapewa uwezo huu wa kupenya kila mahala ili aweze kuelezea hadhira baadhi ya matukio ya faragha ambayo katika muktadha wa maisha halisi ingekuwa muhali kuyajua. Uozo wa mjukuu wake K unabainika kutokana na uhusika wa kimazingaombwe aliopewa babu Mzuka.

Jumba au kasri la K linaweza pia kutazamwa kama sehemu ya uhusika ambao riwaya inautumia ili kutufunulia mengi kuhusu K. Jumba hili linabainika kuwa jumba la kidhahania na limo tu katika fikra za K. Kasri hili ni la kimazingaombwe na lina mabawa kama ndege inayoweza kubeba abiria. Ni kasri kubwa zaidi lenye vyumba vingi mle ndani yake. Babu Mzuka kwa mshangao anamwuliza K ni kwa nini mtu awe na jumba kubwa lenye vyumba vingi zaidi ya mia moja ilhali akijaaliwa na Mungu aweze kuishi muda mrefu, anaishi miaka themanini au tisini tu (uk. 15). Katika dunia halisi, tunawapata marafiki zake K wakilikejeli jumba hilo hilo bila hata kumheshimu K. Kasri hili limetumiwa kuwakashifu viongozi kama K wanaomiliki majengo ya kifahari huku wananchi wasiojiweza katika jamii wakiishi katika makazi yaliyo duni na mazingira yenye umaskini mwingi (uk. 15). Aidha, jumba hili linaweka wazi ulafi na uchoyo wa viongozi wanaofurahia kujilimbikizia mali ambayo kamwe hawataweza kuifaidi maishani mwao. Haya yanathibitishwa na kuwepo ndani ya

kasri wafanyi kazi wa vyeo mbalimbali wakiwemo madereva, walinzi wa kasri, makarani, wapishi, pamoja na wanofanya usafi. Ni ajabu kwamba mhusika K hata huchanganyikiwa na kushindwa kutambua kila mmoja wao mpaka pale anapomhitaji mmoja wao na kulazimika kutumia kompyuta (uk.16).

Tunaona pia mandhari ya kimazingaombwe yanavyojitokeza wakati mhusika K anapojitayarisha kuondoka kwenda hotelini katika gari lake la kifahari likiendeshwa na dereva wake Mzula. Hapo tukio la kimazingaombwe linatokea wakati K alipotaka kuingia ndani ya gari. Gari hilo linaibuka kwa ghafla likitoa sauti kama ya radi kisha kupotelea hewani. Ni umazingaombwe pia wakati walinzi wa K wanapochimbuka kutoka ardhini walikokuwa wamefukulika na kujitokeza juu kwa kasi mara tu waliposikia gari likingurumishwa (uk.17-18).

Wakiwa katika gari lake wakienda Kasino, K na dereva wake Mzula wanakutana na matukio ya kimazingaombwe tena. Umazingaombwe unatokea ambapo kioo kilijitokeza na kuwatenganisha wakiwa ndani ya gari lao kisha milango ikafunguliwa huku gari likienda bila mpangilio wowote na pasipo na aliyetaka kutoka nje ya gari. K anagundua kuwa dereva wake amegeuzwa tayari kuwa nyani huku akiendesha gari kwa njia ya kimazingaombwe kwani anatumia miguu yake ya nyuma kuendesha gari akiwa amekaa kama popo. K anashangaa na kukosa kuyaamini matukio hayo (uk.18-20).

Tumepata kujua ya kuwa tangu babu Mzuka aingie katika maisha ya K, hajawahi kumtoka na amekuwa akimwandama kila mahali kucha kutwa akisababisha mkururo wa mikasa ya kumgandamiza. Mzuka amechukua muda wake kumueleza K kwamba hali yake imechukua mkondo mpya wakiwa pamoja na kwamba amekuja karibu naye ili amsaidie kumtatulia

matatizo aliyonayo K. Mzuka anamwabia K kwamba angalijua angegeuza mienendo yake ili ajiepushe na hukumu inayomgojea, (uk. 21-23).

Wakiwa safarini wakitoka Kasino, babu Mzuka tena anamuonya K kuwa mabaya anayoyafanya katika jamii hayatapita bila yeye kumfanya alipe maovu yake hapa duniani akiwa hai. Babu Mzuka anaendelea kumfunulia macho K kuwa ni yeye anayesababisha maajabu yote anayoyaona yakimfanyikia kutokana na tabia yake mbaya angalau azinduke. K kusikia maneno hayo kutoka kwa babu yake, hakujiamini na hakujua kama yu macho au la. K hakujali wala kujirekebisha hata kidogo (uk. 22-23).

Magari yalikuwa yakienda mfululizo kwa mwendo wa kinyonga huku madereva wakishindwa ni nani aliye na idhini ya kupita ama ni nani anafaa ampe nafasi mwenzake. Watu nao waliokuwa wakitembea walikuwa mashakani. Walipokuwa wakizuiliwa kupita kwa sababu ya magari mengi na wingi wa watu, tukio la kimazingombwe linatokea katika mazingira haya ambapo K na dereva wake Mzula walijipata wakizungukwa na machokora wakiomba angalau thumni. Kulikuwa na vijana pia waliokuwa wameghadhibika huku wakifinyanga ngumi na kupigapiga gari kwa fujo. Wote wakiwa wamebanwa na mori na macho yao mekundu yalikuwa ni kama yanawaka moto wa makaa. Walikwako pia vimada waliokuwa wamevalia miniskati huku wakitembea asteaste na kujipodoapodoa walipokuwa wakipita mbele ya gari la K hukku wakimkonyeza kwa ishara za mapenzi. Gari lao nao lilizimika na lilisukumwa lakini wapi! Halikusonga mbele wala nyuma huku likilia kwa sauti kama ya kondoo badala ya kunguruma kama gari la kawaida.

Umazingaombwe pia unadhihirika wakati K anapowaza kuwa yeye ni kiongozi mkuu wa nchi. Kwa njia ya kidhania, K anafinya kidude fulani cha kisasa lililosababisha gari lake

liruke angani kama ndege ya kubeba abiria likiongozwa na mapikipiki ya polisi kutoka upande zote, nyuma, mbele na hata upande wa kushoto na wengine wakiwa upande wa kulia (uk. 25-28).

Mwandishi pia anatumia umazingaombwe huu kuonyesha jinsi hali ilivyo katika mataifa ya kiafrika ambayo umaskini umetanda na uhitaji walio nao ni mkubwa miongoni mwa wananchi wa kawaida katika jamii. Badala ya kutumia ujuzi na uwezo walionao kubuni njia za kuwawezesha kujitosheleza kiuchumi, viongozi wanaishi maisha ya ubwege huku wakiiga maisha ya Wazungu mawazoni mwao. Mambo hayo yote yanatokana na uongozi duni ambao daima viongozi hao waovu wanazinza vichwa. Kwa sababu ya utovu wa nidhamu katika uongozi na ugavi ovyo wa matumizi ya mali, kumekuwa na chuki kati ya viongozi. Kutokana na kule kutowahudumia wananchi vilivyo, K anawaona mahasimu wake wakimfuata japo hayo ni katika mawazo yake tu. Hawa ni wale wanaopinga uozo wa viongozi katika jamii. Mahasimu hao wa K wanaendelea kuongezeka maradufu na hivyo jambo hili linakuwa onyo kali kwa K kuwa hawezi kamwe kuukimbia ukweli wa mambo katika jamii.

Katika Kasino matukio ya kimazingaombwe yanafanyika pale K anapopepesuka na kuyumbayumba kwa mapozi na majivuno huku akijilazimisha kicheko cha kifahari. Anajitakia makuu huku akijaribu kuwa na moyo wa simba na kutaka kujitajirisha. Aidha K anaagiza vyakula vya ajabu vya wazungu vilivyo mawazoni mwake. Njia ya kukila chakula hicho pia ni kana kwamba mtu amelazimishwa kumega.

Mtunzi anasawiri mhusika Mzuka ambaye ni mhusika wa kimazingaombwe kwa sababu yeye ni mfu na kumtumia ajaribu kumkanya K kutokana na kujiweka kwake katika hali ya kuwa kama mtu ambaye amewekwa jela na kulazimishwa kufuata amri za wakoloni. Mzuka

amesawiriwa kama hasimu wa K kwa lengo la kubainisha namna mtu mweusi anavyofuatafuata mzungu tu kufikia kujisahau na hata kujidharau na kujiamini kwamba hafaa kuishi. K na viongozi wenzake wamekumbatia na kufungamana na utamaduni wa kigeni na kuiga kila kitu kutoka kwa Wazungu na kushiriki mambo yasiokubalika katika jamii yao (uk.38-45).

Umazingaombwe pia unaonekana wakati K anafika ofisini mwake ambapo tukio la ajabu linatokea. K alipigwa na bumbuazi asijue kuwa anachoshuhudia ni kweli au yuko ndotoni. Mara tu ofisi inapofunguliwa, K anapatana na watu dungudungu waliosawiriwa na kuwekewa mikono katika kila kiungo cha mwili wao huku wakivunjavunja kila kitu ofisini kwa njia ya kimiujiza. Kwa mfano badala ya mikono ya kawaida miwili, wako na mikono minne, kisha kuna mkono katika kila sikio, kwenye goti na kiunoni. K anawaona walinzi wa ofisi wakishughulika hapa na pale wakijaribu kuzuia uharibifu unaotendeka lakini viumbe wale wanageuka mvuke kisha wanatoweka machoni mwao. Wanajipata wakiwa na wasiwasi na kupasukwa na mioyo. Umazingaombwe ni kuwa wote waliokuwa pamoja na K, wakiwemo walinzi wa serekali yake, hawakuwaona mahasimu hao wa K kwani matukio hayo yote yamo mawazoni mwa K tu (uk.68-69).

Mtunzi kwa kutumia uhalisiamazingaombwe huu, anadhihirisha kuwa uovu unapozidi katika jamii, mahasimu wa wa viongozi nao huongezeka kila uchao. Nia ya mahasimu hao ni kuwalipiza kisasi viongozi hao kulingana na uongozi wao duni na kwa kuwacha wananchi katika jamii wakiwa hawana asili wala fasili. Umazingaombwe unajitokeza tena katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, wakati K anasawiriwa kujipata gerezani mawazoni mwake akiorodheshewa mashtaka tata (uk.73-75). Baadhi ya mashtaka hayo ni kama yafuatayo:

- Mfumo makini wa kilimo uliofisidiwa kwa ajili ya viongozi fulani kujipatia sifa na kushiriki ufisadi na kuitiza hongo.
- Uozo wa maadili ambapo watoto wanafanyishwa kazi za mkono na kupewa elimu ya jembe miaka yote badala ya elimu kamili itakaowafaidi katika maisha.

Umazingaombwe unatokezea pia pale ambapo mhusika Mzuka anasawiriwa kupatikana kwa njia ya kimazingaombwe katika mazingira ya kimiujiza pasipo ardhi ambapo watu huelea angani. Mzuka aliandamana na K ili aweze kusomeshwa hali ya maisha huko. K anapopinduka na kutazama nyuma yake anajipata ni yeye tu aliye mwanadamu kamili. Aliwaona viumbe wa umbo la kushtua. K anajipata akivuliwa miwani kisha akafaanyishwa mambo ya kustaajabisha na yasiyoweza kuelezeka (uk.82-86).

K, kwa njia ya kimazingaombwe, anageuzwa na kuchukua nafsi nyingine inayomwezesha kuingia kwenye ulimwengu wa kiajabu na kufanyishwa umazingaombwe bila kuwa na uwezo wa kujikinga. Anakutana na watu raia lakini ambao wananung'unika kuhusu utawala mbaya wakisema kina K wakiwemo viongozi wengine wanajifanya joka la mdimu na hawawashughulikii. Watu hao wanapitapita mbele yake na mara wanatoweka. Mara K anawasikiza wakiongea lakini hawawaoni. K anahisi kama wamechukua huko miaka zaidi ya elfu moja katika safari hii ya kuchosha na isiyo na mwisho kiasi cha K kujipata hana damu tena (uk.88-99).

Ni ajabu pia K alipokutana na mhusika Mussa lakini Mussa hakuweza kumtambua kwa sababu amevaa kinyago cha kuvaliwa usoni yaani figu ili asitambulike wazi. Kwa kutumia hali ya kinjozi, mwandishi anaangazia uozo wa uongozi duni katika jamii na kumulika jinsi

viongozi wanavyopuuza jukumu lao la kuleta maendeleo vijijini na kupotelea huko mijini wakila raha (uk.96).

K anaguswa fahamu na anajirejelea na kuhisi makosa yake. Amesawiriwa aweze kufikiria jinsi alivyowahi kusaidiwa siku moja akiwa kwenye shida lakini akasahau hata kutoa shukrani badala yake akamdhuru zaidi yule aliyekuwa amemsaidia. Jambo hili linaelezwa vyema na hadithi ya ngamia na msafiri jangwani:

> *Niruhusu nitie kichwa tu, haya! Msafiri anakubali. Niruhusu niingishe shingo tu, vyema! Msafiri anamwitikia. Niruhusu nitie kifua tu, sawa! Msafiri anamkubalia. Niruhusu niingishe miguu tu, hewalla! Msafiri aridhika. Niruhusu nitie mkia tu, ndiyo! Lo! Kahamanika msafiri, kapigwa teke na kasalia kukula baridi nje ya hema* (uk 98-99).

Mwandishi anatumia hadithi hii kutoa funzo na kuonyesha vile baadhi ya wanadamu wanavyokosa shukrani hata wakisaidiwa wanapokuwa taabani. Mara tu wanapopata msaada na kufanikiwa, huwasahau na hata kuwadharau waliowasaidia bila kufikiri kuwa wanaweza kuwahitaji siku nyingine tena. Mtunzi analinganisha tukio hili na viongozi wanaotoa ahadi zisizo za kweli lakini wanapopata kuingia madarakani, wanawasahau watu waliowachagua na kuwasaidia kupata uongozi.

K anabadilishwa tena kisha anarudishwa katika mandhari yale yale alimotoka. Hapa anapatana na mhusika Maajuza ambaye ni mfu wa nyanya yake. Maajuza anawasimulia wajukuu wake hadithi, K akiwemo. Anawaambia kuwa, simulizi za kale zilikuwa zikifundisha kuwa watu wakifa roho zinatoka ndani ya miili yao na hapo ndio mwisho wa maisha yao ya kawaida lakini watu hao waliokufa hugeuka kuwa pepo wanaoishi bado katika dunia nyingine mpya na ambao wanaweza kusikika lakini ni vigumu waonekane kwa macho ya mwanadamu aliye bado hai. Ajabu ni kwamba wao huathiri maisha ya binadamu wote

katika jamii, matajiri kwa maskini. Maajuza anaendelea kuwasimulia kuwa mizuka katika hali ya kimazingaombwe ina uwezo wa kuwasiliana na watu walio hai wakiwa wanalala usiku kwenye ndoto au wakati wowote wakiwa katika ndoto macho na inaweza kusababisha balaa kwa watu binafsi katika ukoo fulani, au hata katika jamii nzima.

Maajuza akisisitiza, anasema kuwa makungu haya ambayo ni ya kimila hujia watu katika maumbo mbalimbali kwa mfano kama paka nyeusi, nyoka kama vuvi, mijusi, vinyonga, na katika ulimwengu wao kuna giza totoro. Jambo hili ndilo ambalo linawakosesha utulivu na linawafanya waghadhabike na kuamsha taharuki katika mioyo ya wanadamu. Taharuki hizi ndizo ambazo huwaogopesha na hivyo huwafanya kuchukua jukumu la kuwafanya watu walio hai kuingiliana na kuwashirikisha katika kusafisha dhambi na mara dhambi zinaondolewa. Vijijini, matendo yao hufunuliwa na kumulikwa kiajabu kwa mwanga unaong'aa kote hata kwa watu walio wangali hai. Wakati Maajuza anaposema kuwa wanaofanya mambo maovu huandamwa na pepo wasioonekana wakitaka kulipiza kisasi, K anachukuliwa papo hapo akiwa mzimamzima na kudidimizwa kwenye ardhi ya saba. Huko ndiko anakoshuhudia ukweli wa hadithi hii ya Maajuza (uk. 117-120). Tunaona matukio ya kimazingaombwe yanayotokana na masimulizi haya ambayo hayafuatiliki kama ilivyo katika maisha ya kawaida.

Katika ulimwengu wa kawaida inajulikana kuwa watu waliofariki hawana uwezo wa kuwa hai tena wala kuwa na uwezo wa kuingilia maisha ya watu walio hai katika jamii. Ingawa hivyo, mtunzi anatumia umazingaombwe huu ili aweze kusababisha msomaji kusafirishwa kimawazo kwenye safari ya hali na matukio yaliyo na uimara wa hoja. Mwandishi hapa anajenga kimakusudi wahusika wenye nafsi zaidi ya moja. Akiwa katika nafsi iliyo halisi,

kwa mfano, K anashindwa kuamini mambo yanayohusu hali ya mizuka lakini katika nafsi nyingine akiwa amebadilishwa na kugeuzwa na kufaywa achukue nafsi ya mzuka anajipata kuyaelewa matukio haya ya kimazingaombwe bila tashwishi.

K akiwa safarini anashangaa kupitishwa katika nchi zenye majina yaliyosawiria kwa mlinganisho wa mawazo ya mtunzi kama vile nchi za Kataa na anashangaa na kujiuliza kama ni kukataa ama ni kukataliwa. Jina jingine ni nchi ya Amani na K hapa anajiambia kuwa angependa kuwa na makao hapo. Kufikia nchi ya Nusunjia na nyinginezo, ndipo anapatwa na uoga akijua kwamba Nusunjia huenda ukawa mwisho wa safari yao. Baada ya muda kidogo, K anaona umati mkubwa na kila mtu alikuwa akiabudu sanamu wenye sura ya mnyama fulani kutoka nchi za ngambo asiyejulikana na huenda ikawa mnyama huyo ni pepo. Majina haya hayakutumika kisadfa bali ni njiaya riwaya ya kuelezea namna wakoloni wanavyotumia hila za kuwazuga watawala weusi. Safari hii ya K inaashiria namna watawala hawa Waafrika wanavyozugwa kiakili kwa kufundishwa namna ya kuwazuga watawaliwa ili wakose kujiamini hata pale inapobainika wazi kuwa kile wanachokiona ni kitu cha sawa. Watawaliwa wanafanywa wakose kujiamini. *Babu Alipofufuka* inatumia matukio haya ya kiajabu kuonyesha na kudhihirisha athari za utandawazi katika barani Afrika. Hii ni kwa sababu watu katika jamii mbalimbali za kiafrika wanaiga karibu kila kitu kutoka Wazungu huku wakipuuza mambo mengi ya maana katika utamaduni wao hata kuwa na uwezekano kuwa wameanza kuabudu miungu yao. Mwandishi anasisitiza kuwa viongozi wetu wa Kiafrika hawathamini vitu vyao vya kiasili hata kidogo kwa sababu wakoloni waliwagaragaza hadi akili zao kugandamizwa.

Umazingaombwe unapatikana pia wakati mhusika K anaporejeshwa na babu Mzuka akimsababisha apitishwe baharini ambapo kuna mahakimu. Hii ni kwa sababu kulingana na

Mzuka, K ni lazima apatiwe hukumu bila kuhurumiwa. Mzuka anamwambia K kuwa, hana la kuchagua wala cha kuamua kwani maamuzi ni kwa mahakama ambako ataishia korokoroni. Mhusika K, kutokana na kiburi chake, anaendelea kukataa mashtaka akikosa kutambua kuwa panzi huingia kwa kujilinganisha na moto. Mzuka kwa kujaribu kumfanya K aogope mahakama, anamfanya aona viumbe wa kimazingaombwe. K anashangaa kuwaona watu watano ambao ni wa umri mkubwa na wenye ndevu nyeupenyeupe lakini umbo la watu hao sio kama la wanadamu wa kawaida. Mzuka anamwambia K kuwa hao wazee ndio mahakimu wanaosubiri kusikiliza mashtaka ya viongozi waovu katika Gehenna.

Mwandishi, kwa kutumia mahakama na mahakimu wa kimazingaombwe, anadhihirisha kuwa hukumu ni jambo la lazima kwa viongozi ambao juhudi zao haziafikiani na mahitaji ya wananchi katika jamii na wanaokosa kuwajibika kwa njia ipasavyo katika kutekeleza shughuli zao vilivyo wanapowahudumia raia wa kawaida. Babu Mzuka anasema hata wakifa viongozi hao, lazima wataabike hadi kizazi chao pia kilipizwe kisasi hata kama ni kupitia kwa watoto wao wenyewe ama jamaa yao. Mzuka anamuelezea K kuwa hata kukikosekana kumwadhibu yeyote katika jamaa yao, basi hata vivuli vyao vitahukumiwa kwani hiyo ndiyo kanuni iliyowadia. Babu Mzuka anamwambia K kuwa yeye akiwa babu yake, amefika ukingoni kwa kufanya bidii kumwelekeza na kwamba amemaliza kazi yake ya kujaribu kumwadhibu vilivyo na kwamba kilichosalia sasa ni kumwachilia apewe adhabu ya kumtosha (uk.143-144).

Umazingaombwe unadhihirika pia wakati wanasheria huko mahakamani wanapomlisha K kiapo cha mchanganyiko wa vitu vingi vya ajabu. Baadhi ya viungo hivyo ni pamoja na karafuumaiti na vipande vya unyoya na mangisi kukiwemo nyama ya kinyaunyau na mizizi ya mimea aina mbalimbali ya makaburini. Pamoja na hivyo viungo pia ni kalatusi na

magamba ya samaki aina mbalimbali (uk.133-145). Kiapo hiki ni jumla ya mbinu za kikatili wanazofundishwa watawala weusi ili wasijali ukatili wao pindi wanaposhika hatamu za uongozi. Kiapo anacholishwa K kina viungo vya kuogofya ingawa hatimaye anavila.

Mwandishi anatumia kauli alizowekewa K bayana kutoa ushahidi kuwa kuna ukweli wa yale yaliyosemwa na hata yaliyoshuhudiwa akifanya kwa kula yamini. Tumefahamu kuwa mwandishi kwa kupitia kiapo cha aina hii ametoa dhihirisho kuwa K na viongozi wengine wengi wamefanya makosa katika jamii na hata nchi nzima kulingana na maovu waliyoyatenda ambayo bila shaka yameathiri watu na hata kwa wanyama na mimea ya aina mbalimbali. Madhara haya yako kweli kwa mfano, misitu inapokatwa ovyo ovyo, chechemi ya maji huathirika na hapo watu pamoja na wanyama katika mazingira wanakosa maji.

Ajabu ni kuwa mhusika K baada ya kula kiapo, macho yake yanafunguka na kuweza kuaona jinsi mambo yamezoroteka katika jamii kupita kiasi. Mfano ni kiwango ambacho barabara zimeharibika. Hali ya maisha ya watu ni mbaya. Vijana chipukizi wametorokea nchi za ngambo na waliosalia ni wazee waliomaliza kula chumvi kitambo.

Katika mawazo ya K, umazingaombwe bado unadhihirika kwani anaona watu hao wasio na umbo la binadamu wa kawaida wakionekana wakitafuta kitu kisichoonekana wala kutambulika ni nini wanachotafuta. Wanatafutatafuta tu na nyuso zao zinaonyesha kukata tamaa. Hawana anayewapa msaada hata wakiomba. Ulimwengu wote umejumuika kuwadharau kwa sababu wanawakaghadhabisha hata kwa kuwatazama tu (uk. 146- 147).

Mhusika K mwishowe anarejeshwa katika ulimwengu halisi na kufikishwa kwenye kasri lake. Anakutana na doggi wake na mara moja anafurahi na kukumbatiana naye wote

wakitokwa na machozi ya furaha tele tele. Kidogo tu K ananyambulika na kutururika moyo na kukosa kufanikiwa kupata wa kumpa sauti. Bila kuambiwa anajipata akijiambia kuwa wakati wa kufunga jamvi umefika. K amenyang'anywa mamlaka yake yote na watumishi pamoja na walinzi wake wote wametolewa. Anapojaribu kukimbilia usaidizi huko Kasino hapati wa kumkaribisha tena. Hapa sasa K akigitagita, anawakumbuka wanawe, Kidawa na Bamkubwa na mkewe Kikuba ambaye tayari wameshageuka kuwa wendawazimu kutokana na shida mbalimbali baada ya kutupiliwa mbali na K kwa miaka yote akiwa uongozini. Katika hali halisi K anajipata mashakani kwenye njia panda huku mawazo yakimzidi. Mwishowe K anajinyonga. Anapokufa anajipata amedidimia kwenye makazi mahalum huko ahera. K akiwa pepo, anajaribu kuwafikia watoto wake lakini wapi! Haikuwezekana tena na akasalia akitamani kuwa na uwezo kama ule wa babu yake Mzuka (uk. 165-168).

### 4.1.2 Wahusika, Uhusika na Mandhari ya Kimazingaombwe katika *Watu wa Gehenna*

Katika kuangazia uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*, imebidi tuangalie masimulizi mbalimbali na mandhari ambayo mwandishi Tom Olali amebuni na kutumika katika kazi yake ya usanii. Tumechanganua umazingaombwe wa wahusika na uhusika wa kifantasia katika aina mbalimbali za mazingira ya riwaya. Amesawiri wahusika wake watekeleze matukio ya kifantasia ambayo yanaingiliana vizuri na uteuzi wa mandhari yaliyoyaumba akiashiria kuambatisha hali ya kimazingaobwe unaopatikana katika jamii na uovu wa viongozi wanaojitakia makuu bila kujali matatizo ya wananchi ihali wao ndio wanaotegemewa kutatua shida hizo na kuleta suluhisho katika jamii.

Wasomaji wa kazi hii wamechorewa taswira ya kimazingaombwe na ya kutatanisha kupitia mandhari ya jahanamu ambapo watu wanahukumiwa. Mtunzi anayapatia makazi haya jina

“Gehenna” yaani eneo ambalo kuna moto mkali usiozimika na kuufanya kama mahali pa kuadhibu na kupatisha taabu au maumivu makali kwa watu walioshiriki matendo maovu wakiwa hai katika jamii, (uk.1-8).

Kwa kutumia mbinu za kimiujiza zisizoeleweka, Olali anaumba wahusika wake wa kimazingaombwe na kuwaweka katika mazingira tata ya kifantasia na kisha kuwapa matukio ya kustaajabisha na ambayo yanadhihirisha umazingaombwe na uovu katika jamii. Uovu huo unatekelezwa hasa na viongozi walioshiriki matendo mabaya katika jamii na mwishowe wanaadhibiwa kwa kugeuzwa watu ambao mazingira yao ni gereza lile la Gehenna milele.

Olali, pia amesawiri na kutumia mandhari haya ya kimazingaombwe kwa mfano gereza lenye moto unaowaka daima ukichoma na kutaabisha watu bila kikomo. Anadhamiria kujulisha jamii kuwa ni haki yao wakatae kudhulumiwa na kulazimishwa kutoa hongo kila mara wanapohitaji msaada wowote kutoka kwa serikali. Mtunzi anatumia hali hii pia kama njia ya kuleta onyo kwa viongozi hasa wa kisiasa wanaotenda matendo mabaya yanayosababisha mahangaiko mabaya kwa wananchi wa kawaida katika jamii. Kwa njia hii anawahakikishia wananchi hao kuwa hukumu ni lazima kwa wale wanaoshiriki maovu hasa viongozi kwa kutojitolea katika kuwafanyia watu kazi na kwamba mwishowe watapata adhabu kali kwa kutowajibika vilivyo.

*Watu wa Gehenna* imewasilisha ujumbe wake kwa kumsawiri mhusika wa kimazingaombwe, Eks na kumwezesha kuwa na nafsi tatu na kumpa uwezo wa kugeuza nafsi yake na kuilekezea kwa mhusika tofauti. La ajabu ni kuwa nafsi yake Eks inazungumza naye kana kwamba ni watu wawili wanaozungumza kisha nafsi yake ya tatu inawacheka na kukejeli wenzake na hapo kumkasirisha Eks. Wanabishana huku wakipigiana kelele na kwa hali

inayonsikika kama ya kawaida lakini watu humuona mtu mmoja (Eks) akifanya mambo hayo ya kimazingaombwe peke yake huku wakitafakari na kuulizana kama Eks amepatwa na kichaa (uk.9-14). Ni umazingaombwe pia Eks anaposawiriwa na mtunzi kuwa na uwezo wa kujigeuza kuwa sauti zinazosikika zikiongea lakini watu wenyewe wanaozungumza hawaonekani (uk.8-15).

Uchunguzi katika utafiti huu pia umedhihirisha kuwa mtunzi amesawiri uwepo wa umazingaombwe na uhalisia katika uwasilishaji kupitia mchanganyiko wa wahusika wa kimazingaombwe na wale wa kiuhalisia. Kwa kutoa mfano, hali ya kiuhalisia inaonekana wakati Eks anasawiriwa kama mhusika mmojawapo wa wafanya kazi katika kiwanda cha kutengeneza saruji. Akiwa kazini katika kampuni hii, alipatwa na magonjwa yaliyosababishwa na hali mbaya kimazingira pamoja na kemikali katika kiwanda hicho. Eks anaathirika kiafya na hata akawa na upungufu wa akili na akaugua ugonjwa wa mapafu na matatizo ya figo. Eks akawa na maumivu mengi akawa amelemazwa kabisa (uk. 14-15). Kupitia ujumbe huu, mtunzi anaonyesha hapa kuwa waajiri wengi katika jamii huwatumia wafanyikazi kwa lengo la kupata faida kubwa bila ya kujali maslahi ya wafanyakazi hao kiafya.

Kutokana na matukio haya, mwandishi anatumia wahusika wa kimazingaombwe na mandhari halisi kuangaza jinsi wafanyi kazi wanavyoteswa na kuhangaishwa na baadhi ya makampuni na kuwa muda si mrefu wanapatwa na matatizo ya kiafya wakiwa kazini. Tunaona pia uwasilishaji katika mandhari ya kimazingaombwe, wakati nafsi ya Eks inamlazimisha ajitoe uhai. Kabla ya kukata roho, nafsi yake inamwambia kuhusu matendo yake yaliyodhuru wananchi. Baada ya kuulizwa swali ambalo hakuweza kulijibu, Eks papo hapo anafariki. Baada ya miaka kadhaa Eks anafufuka na kurudi katika maisha yake ya kawaida.

Eks sawa na Babu Mzuka wa *Babu Alipofufuka* anapewa uwezo wa kuweza kuwasiliana na mizuka wengine kwa njia ya kiajabu (uk.29-33). Ya kustaajabisha ni kwamba kama mhusika K katika kitabu cha SA. Mohamed, Olali naye anamsawiri mhusika Eks akifa kupitia kujiua na kisha kufufuka baadaye. Ni ajabu zaidi wakati Eks anasawiriwa kuwa na nafsi kadhaa na kuwa uwezo wa kubadilikabadilika kuchukuwa nafsi tofautitofauti baada ya kifo chake. Amesawiriwa kujipangia kifo chake, ajipangie maombolezi juu ya kifo chake na hata apange na kutekeleza mazishi yake mwenywe (uk 36-40).

Umazingaombwe uliendelea kufanyika baada ya miaka kadhaa wakati ya Eks kwa njia ya kiajabu anaamuriwa kujito. Eks alionekana akifanya hivyo kisha kujifufua na kujipata akiketi jukwaani kwenye jumba la kifahari huku umati wa watu wakimtazama. Katika mandhari haya pia, matukio ya kimazingaombwe yanafanyika Eks anapoamrishwa kujigeuza kijana chipikizi kwa kubadilisha jina lake na umri wake upunguzwe kutoka miaka sabini hadi miaka ishirini na tatu, (uk. 48).

Ni tukio la kimazingaombwe pia wakati mhusika Mkuu kupea Eks amri ambazo lazima azifuate ili apate umaarufu fulani na atekeleze umazingaombwe zaidi. Maagizo aliyopewa Eks yalikuwa ni pamoja na kuchomoka na kufyatuka huku akififia angani. Anarudi kutoka angani kama amejipamba na maarifa chungu nzima maarubu yake yakiwa ni kuwashirikisha binadamu wote maagizo maarufu kweli kweli ambayo yatawafurahisha na kuwafanya wamuabudu Eks. Tunashuhudia hotuba ya kiajabu ambapo Mkuu ambaye amegeuka mabruki aliyeneemeka na kufanikiwa kutambua na kujua matatizo ya aina yote ulimwenguni kote yakiwemo matatizo ya kiafya. Anaambia umati wa watu anaowazungumzia kuwa ni changamoto zaidi kila pahali duniani kwa wanaougua magonjwa mabaya yasiyo na tiba ya kawaida na isitishe ni watu maskini..

Mtunzi amewapa baadhi ya wahusika majina kwa njia ya kiajabu kama vile mhusika kwa jina Sikujua aliyepata jina lake kutokana na neno 'sikujua' na hata matendo yake yanaashiria yeye kutojua mengi kwa yale yaliyomtokezea. Sikujua ni rafiki mkubwa wa mhusika Baya na anafunga safari kwenda kumuona kwani alikuwa na mpango wa kumuoa binti huyo lakini jinsi jina linavyoashiria, Sikujua hakuwa akijua Baya ni msichana wa aina gani.

Vilevile, Sikujua anapokutana na binti mmoja aliyejirembesha na wa kumezewa mate kwa jina Takosani binti Inatesh ambaye jina lake *Inatesh* pia linatokana na jina '*Shetani*'. Sikujua hakujua kuwa hapo ndio ilikuwa mwanzo wa kufuga chui. Baada ya kuwazawaza, mara moja mawazoni mwake anakumbuka kuwa kwa kweli hamjui Baya vizuri na bila kuchukua muda, akili zake zote zinamwedea Takosoni binti Inatesh. Kumbe ilikuwa kuruka kutoka kanga ndani ya moto. Sikujua alijipata jela na akaamua kuwa ilikuwa wakati bora kujipatia jiko bila kumkagua na kutafuta njia ya kujua mienendo ya binti huyo na kusahau kuwa *'mtaka nyingi nasaba hupata mingi misiba!*. Walipokuwa wakijadiliana ajabu ni kwamba, binti huyu wa kifantasia ana mambo ya kimazingaombwe chungu nzima. Binti Inatesh alimshangaza sana Sikujua alipompasulia waziwazi kwamba, anapenda kutembelea mizuka huku makaburini na akamwomba waandamane naye ili aweze kuombea mamaye aliyeaga dunia miaka kadhaa iliyopita. Sikujua hakuwa na la kufanya ila kumtii. Walipofika kaburini, Takosani anajiangusha chini na kulialia kwa sauti kubwa sana hadi jioni huku akitoa majonzi ya mamba na kumwomba Sikujua amchukue baharini hata kama ni wakati wa usiku ili aweze kuogelea. Sikujua akamtii lakini wakati huo alikuwa amepata kujua kuwa mambo yake hayachukuliki (uk.41-44).

Sikujua kupatana na umazingaomwe huu, anapasuka moyo anavyosikia haya lakini kwa sababu ya mahaba ya njiwa na mvuto wa msichana huyu wa kiajabu ambaye tayari amekwishamgusa fahamu, anamchukua hoteli na kukodisha vyumba nambari kumi na tano na kumi na nane, yaani kila mmojawao chumba chake. Takosani anaomba chumba nambari kumi na nane kibadilishwe ili wachukue chumba nambari kumi na tatu. Kuambiwa na mwenye hoteli kuwa hamna nafasi, Inatesh aliyekuwa akitaka chumba chenye nambari hiyo kwa hamu na ghamu aliamua kutumia miujiza yake. Akajigeza mbu mara moja kisha kutoweka kwa muda. Sikujua anajua kuwa nambari kumi na tatu kwa kawaida inahusishwa na nuksi fulani lakini la kushangaza ni kuwa Inatesh amekwamilia akitaka kupewa chumba chenye nambari hiyo. Alipokuwa akishangaa ni nini kinachofanyika tukio lililomstaajabisha likatokea. Alijipata ndani ya ndege na kwa ghafla wakatua kwenye hoteli kubwa ya kifahari na muda si muda wakajipata kwenye chumba nambari kumi na tatu huku wakishiriki ngono kwa furaha tele.

Katika mandhari haya ya kiajabu, Sikujua akiwa macho alimuona Inatesh akiondoka kupitia ukutani kwa njia ya kimazingaombwe. Anaporudi na kumuona Sikujua akiona kero, Inatesh anamwamuru Sikujua afunge macho na mara tu anapofunga macho yake anapoteza fahamu na kupatwa na usingizi mzito wa pono. Anapoamka na kupata fahamu, anajikuta kwenye mandhari ya kiajabu akiwa amezungukwa na majitu yanaofanana na watu lakini wao si watu wa kawaida. Inatesh alionekana akimkamata Sikujua mkono akitaka wafunge ndoa papo hapo. Sikujua anashindwa kuelewa kama anaota ndoto au ni nini anachokiona. Anajaribu kumhoji Inatesh akimwabia kuwa anaona kama yeye ni jini lakini wapi! Inatesh anaiva macho huku akiwa amejaa bughudha na mara moja anampotezea akili Sikujua jambo ambalo ni la kukefyakefya kwani Sikujua alikuwa akijifanyia mawele. Baada ya kukaa kiungani kwa

muda, Inatesh akakabilisha moyo kisha akamjibu akisema yeye ni mwanadamu halisi. Sikujua anamwuliza amuelezee ni wapi walikokuwa. Takosani anamfahamisha bila kumficha kuwa walikuwa kwenye ulimwengu wao maalum chini ya bahari.

Sikujua anajipata tena chumbani mwake. Inatesh anapanga sherehe kubwa mawazoni mwa Sikujua. Anamwamuru Sikujua amwekee wimbo wa kimashetani lakini anamueleza Inatesh kuwa hana santuri yenye muziki wa aina hiyo. Hapohapo, Inatesh anatoa santuri iliyoandikwa jina lake *Inatesh* (shetani) kwa rangi nyekundu. La kushangaza zaidi ni kwamba Sikujua anashindwa kunata ujumbe kutoka kwa wimbo huo. Ni jambo la kifantasia kuwa wimbo unaopaswa kuimbwa kuanzia mwanzo ikawa wimbo unaoimbwa kuanzia nyuma ama mwisho wa wimbo huku maneno yakitamkwa kinyumenyume ili iwakoseshea watu mwelekeo na wasiweze kupata ujumbe wenyewe vilivyo. Ya ajabu pia ni kwamba walipokuwa wakiendelea na sherehe hiyo, wanyama wa aina yote duniani walikuwa wamejibana kila mahali pembeni mwa uwanja kila kikundi kikicheza kwa mtindo wa kimazingaombwe viungo vyote vya miili yao vikitetemeshwa. Sikujua akiwa amepigwa na butwaa, Inatesh akimshika kwa sikio akimninginisha huku akichezacheza (uk.48-53).

Mtunzi wa kazi hii anajaribu kuleta funzo katika jamii kutokana na uwasilishaji huu kwamba tunaelewa wazi jinsi vijana wetu katika maisha ya kisasa wanavyojipata wakishiriki katika mambo ya kuogopesha na hata kunaswa na kutoswa baharini kwenye mambo yanayowapandisha shetani bila kujua. Mambo haya yanafanyika kwa mfano wanafunzi wengi hasa katika vyuo vikuu wanajipata tayari wamechochewa na kutiwa hamu kisha kunaswa katika matumizi ya dawa za kulevya.

Tunapata pia kuwa katika jamii zetu hapo awali, nyimbo zilikuwa zikitumika kama vyombo vya kuelimisha, kuonya na kueneza ujumbe. Kinachostaajabisha katika ulimwengu wa kisasa ni kuwa nyimbo nyingi za vijana ni za kukera na wanapozisikiliza hupandwa na jazba huku wakipata mshawasha wa kufanya maovu. Nyimbo za hukosa urajua na hamna chochote kinachosikika wala kueleweka katika nyimbo hizo. Ya ajabu pia ni kwamba nyimbo hizi zina beba lugha ya vikundi fulani vya watu katika jamii ya kisasa. Sawa na hulka ya Inatesh, vijana hawa ndio wanaoelewa kinyume mbele kilichomo ndani ya nyimbo hizi na wana uwezo wa kuelewana wao kwa wao. Zinapoimbwa nyimbo hizo walengwa hao wanavutiwa na ngoma hadi kupandwa na jazba kisha kupatwa na hisia au taathira ya kujisahau nafsi na mwishowe wanajipata wakipanda mbegu za kutenda maovu. Matukio ya aina hii ni ya kimazingaombwe yanapofikia masikioni mwa wazee na hivyo, mwandishi amejaribu kutumia fursa hii kumulika visa vya aina hii na kutahadharisha jamii yote kwa jumla kupitia wasomaji wao lengwa.

Tom Olali, mwandishi wa riwaya ya *Watu wa Gehenna*, kwa kutumia mbinu za kimiujiza katika uwasilishaji wa ujumbe na kwa usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe, amefanikiwa kuafikia malengo yake katika kazi yake ya kimajaribio kwa kuenda kinyume cha sheria za sanaa za kijadi. Ameweza pia kutumia fursa hii kuelimisha jamii kisiasa. Hii ni kwa sababu wanauhalisiajabu wako huru kujadili na kushughulikia mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla katika kazi zao bila kufungwa na mbinu za awali za sanaa za kijadi (uk 53-56).

Umazingaombwe unajitokeza wakati Van, mhusika ambaye amejitopolea elimu kutoka chuo kikuu cha *End of This World* nchini Taznania (Tanzania). Kupitia nguvu za kiajabu Van

anafanywa aning'inie kwenye mlingoti wa bendera huku akitishwa kusulubiwa kama Yesu kwa sababu yeye alikuwa mmoja wa wale waliokuwa wakipinga uongozi mbaya huko Taznania (uk. 54).

Akiwa na nia ya kuziba ufa, Van anasimulia matukio ya kimazingaombwe yanayotokea akisema kuwa viongozi wengi wa kisiasa wana tabia ya kuamini mambo ya ramli na uchawi na wanashirikisha mambo hayo ya ushirikina na siasa katika jamii. Anasema kwamba viongozi hao hulenga kuyashikamanisha mambo hayo kwa pamoja huku kila mmoja wao akitamani kutajirika upesi sana.

Van anaona kwamba hamna tofauti kwa wenyeji kwani ni kama wanasiasa wana tumia mateka na ngumi kunyayasa wananchi walio maskini katika jamii. Wanaamini mambo ya kinyago yanayohusisha uganga wa kiasili wa kuponya au kudhuru si hoja kwao. Lililo hoja ni kwamba matendo haya yote ni yale yanaojumulisha siri ya mizungu mwishowe. Van akifafanua zaidi anaeleza kuwa mazingaombwe hayo ni kiinimacho ambacho kinahusu mafunzo ya hekima hususan katika kumbi za uganga yanoyotolewa kwa siri kwa lengo la viongozi hao wa kichawi kujipatia uongozi kwa kutumia nguvu za kichawi kupata ushindi katika uchaguzi huko Taznania. Wanafanya hivyo kwa kusababisha matendo ya kudanganya macho ya wananchi. Mambo ambayo huwafanya waone au wafahamu mambo kinyume na jinsi yalivyo. (uk. 53-56).

Mhusika Siyawezi akichangia kuhusu umazingaombwe katika uwasilishaji, anatoa maelezo yake kuwa katika Kisiwa cha Pate kumekuwa na wataalamu hodari wenye ujuzi wa juu wa sayansi ya kimazingaombwe. Akitoa maelezo yake zaidi, anasimulia uchawi wenye mateso

makali yanayofanyiwa wapinzani walio na nia nzuri kisiasa. Umazingaombwe ni kuwa wanageuzwa viumbe waliochakalika, wenye maumbo ya kiajabu ya mnyama mwitu na wasioonekana kama wakaaji wa dunia hii (uk. 54-57). Wanasiasa, hasa wabunge na mawaziri katika mazingira haya, hufanyishwa madhambi na waganga na kupitishwa kwenye kiapo cha kuwapiga zii na kujipata wakifanyiwa umazingaombwe kama vile kutakiwa kuruka na hata kukunywa damu za wanyama wenye maumbo ya kutisha. Maajabu haya yote yanafanywa usiku wa manane na wanaoshuhudia matukio haya ni majitu manene, kila moja likiwa na jicho kubwa usoni mwake. Macho hayo yanatoa mwangaza tele. Mbuzi anazikwa akiwa hai huku mdomo, macho, na masikio yake yakiwa yameshonwa kisha kubandikwa jina lenye herufi *demokrasia*. Lengo likiwa kumaliza nguvu za wapinzani wao wa kisiasa. Ya kustaajabisha ni kwamba, keshoye viongozi hao wanachukuliwa na chechele na kuingiwa na sahau wakionekana wakitema cheche bungeni wakijifanya viongozi waliochaguliwa na wananchi (uk. 56-58).

Umazingaombwe unazidi kufanyika huku Pate, tunapoelezwa kuwa wanasiasa hutumia nguvu za popo kuwadhulumu na kuwahangaisha wapinzani wao wa kisiasa. Yanayostaajabisha ni kuwa wanasiasa hao waovu wanashiriki matendo ya kishetani yasioaminika. Tunayowasilishiwa na wahusika wa kimazingaombwe ni mambo ambayo katika hali halisi ni vigumu kufanyika. Tunaambiwa kuwa wanasiasa wanaotumia nguvu za kichawi kupata ushindi katika uchaguzi huko Taznania wanashiriki ukahaba na popo usiku ili wapate nguvu za kuwawezesha washinde wanasiasa wenzao wanaopingana nao. Wanapofanya hivyo, wanahakikisha kuwa wamekaa macho kwa muda huwo wote wasije wakashikwa na usingizi na kisha kuzuzua mambo. Hii ni kwa sababu inaaminika kuwa mwanasiasa yeyote akilala akiwa katika hali hiyo ya ukahaba na popo atashambuliwa na

malengo yake kuzidi kudidimia. Ya ajabu pia ni kwamba wakikosa kuwa na moyo kwa hali na mali kukaa ange hadi popo hao wafikie tamati shughuli zao, watapigwa kipaipai, kwani wakisumbuliwa wakiwa wangali katika hali hii, watapatwa na hasira kisha kudhoofisha hali ya wanasiasa hao ya kiafya. Aidha, inaaminika kuwa wataangamiza umaarufu wa chama chao cha kisiasa kinachowashughulikia na kutathmini kufaulu kwao kisiasa. Ni lazima basi, wakae chonjo ama watumbukie kwenye jungu la matuta ya moto wakilala kabla popo kukamilisha shughuli zao za ukahaba na kuyoyomea mbali.

Matukio zaidi ya kimazingaombwe yanafanyika wakati Siyawezi katika uwasilishaji wa ujumbe anasababisha matukio ya kimazingaombwe hivi kwamba wananchi wananyanyaswa na kutumiwa vibaya. Wanaondolewa majumbani mwao usiku kwa njia ya kimiujiza bila wenyewe kujua na kwenda kufanyishwa kazi ya kupigapiga mawe usiku kucha na wengine kuchimba kisima kisha wanarudishwa alfajiri wakiwa wamechoka huku wakiwa wamefanya kazi bila malipo yeyote (uk.57-60). Ingawa kuna baadhi ya watu katika jamii zetu wanaoamini mambo ya aina hii, jambo la kumaanika ni kuwa mtu kwa hiari yake mwenyewe hushiriki kwa kuona anachotaka na kusikiza anachotaka kusikia na kwamba imani za kimazingaombwe za majini humuathiri tu, yule anayeamini imani hizo.

Tunapatana na matendo ya wahusika wa kimazingaombwe ambapo Sikujua aligwaywa moyo akiwa ndani ya gari wakisafiri. Aliona gari lao walimokuwa wakiabiri likizama baharini. Punde si punde anajikuta mahakamani. Hapo alijipata katika njia panda lakini hakutaka kuamini tayari amepigwa tinge na anajiambia, akijaribu kujishikilia kwenye shingo ngumu kuwa anachopitia ni ndoto tu. Kisha anajihurumia akihisi kwamba amechanganyikiwa na

kujiambia hayo yaweza kuwa si mambo yaliyo kweli ama yawe ni mambo ya ukweli hakatai, bali yote mawili kwa pamoja ni sawa (uk.59-60).

Ni ajabu Sikujua anapoletewa chakula akiwa kwake na wafanyi kazi wanaomhudumia Inatesh. Kabla hata kula chakula hicho anashikwa na fadhaa anapopata kuwa kwa ghafla mahali pale panageuka kuwa mahakama na wale watumishi wa Inatesh wakageuka wakawa mahakimu wa kumshtaki Sikujua. Kwa ukali, wanamuorodeshea makosa yake yote aliyoyatenda pamoja na watu ambao wengi wao aliwatesa wakiwa hai na ambao sasa ni mizuka. Sikujua pia anashtakiwa kuwa alipokuwa akitafuta kura na wakati alikuwa mamlakani kama mbunge, alishiriki katika vita vya kikabila na kusababisha umwagikaji wa damu wakati wa kampeni na baada ya uchaguzi. Vilevile, yeye anashtakiwa kuwa alipata cheo chake cha ubunge kupitia matendo ya kichawi na madhambi mengineyo. Mwishowe, watumishi hao wanachukua jukumu la kumwadhibu kwa kumpa kichapo cha mbwa bila kumhurumia (uk.60-63).

Kupitia matukio ya kimazingaombwe, mwandishi ametumia fursa hii katika uhusika wa kazi yake kutoa onyo kwa watu wengine wakiwemo viongozi ambao hushiriki katika utekelezaji wa mambo mabaya yanayo- sababisha mateso kwa wananchi katika jamii. Mtunzi pia katika usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe anadhihirisha kuwa kuna wakati maovu haya yote yatafichuka na mwishowe adhabu kali kutolewa kwao.

Tunapata pia matukio ya kifantasia wakati wahusika wa kimazingaombwe waliposawiriwa katika mandhari ambapo mchezo wa kiajabu unachezewa kwa malengo ya kudalilisha wananchi na kuhatarisha maisha yao kwa njia ya kajabu bila idhini yao. Mchezo huu unasemekana kuwa ni mchezo unaochezwa kwa kuwakusanya watu mia sita sitini na sita

kwa safari moja na kisha kuwaweka kwenye shuka linaloshikwa kila kipembe na Mashetani sita sita wanaozungusha watu hao mara sita na kisha kuwatumbukiza kwenye shimo linalowaka moto na baadaye kila mmoja wao anajipata uso wake ukichomelewa alama ya kushangaza. Wanaporudishwa kutoka katika shimo lile, wanalazimishwa kusimama foleni wakiwa wamevishwa taji lenye herufi '666.' Kila mmoja wao analazimika kuapa mara 666 bila kupumua kisha wanawachiliwa (uk 63-65.

Usawirishaji wa wahusika wa kimazingaombwe unapatikana pia katika mandhari ya makaburini tunapompata Sikujua na Inatesh wakikutana na mhusika mwingine wa kiajabu kwa jina Sshamy ambaye anawapeleka kwenye shimo la kuhifadhi miili ya albino. Sikujua anaamuriwa wabadilishane na Sshamy na kugeuzwa kuwa mlinzi wa chumba hicho (uk.66-71).

Tumepata pia katika mandhari haya ya mahakama, magari yanayosafirisha watu kwa azma ya kuwanyonga. Lengo kuu la wenye magari hayo ni kuwalaghai watu ambao wanatumiwa kufanya biashara haramu ya kuwaua wenzao na kisha kutoa sehemu nyeti za mili yao na kuziuza (uk. 81- 97). Mtunzi pia anasawiri wahusika wa kimazingaombwe kwa kusababisha mabishano na wananchi kisha kuwashawishi washiriki katika hii biashara duni ya kuwatafuta maalbino vijijini huku wenyewe wakitumia dawa za kulevya na mwishowe wanashtakiwa na kuhukumiwa vilivyo. Kulingana na mashtaka haya, mtunzi anajaribu kuleta wazi dhihirisho la jinsi watu wanavyohadaiwa na kupelekwa nchi za ng'ambo kwa minajili ya kupata kuajiriwa kazi lakini wafikapo huko, waajiri wanawageuka na kutowalipa mshahara.

Katika mandhari ya safarini au tuseme mazingira yanayohusiana na usafirishaji, tunapata uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe wakitekeleza matukio ya kimazingaombwe

yanayoshtua. Haya yalifanyika wakati mhusika Baya aliposimamishwa na kuombwa lifti na Mishi. Walipokuwa wakiendelea na safari yao wakiwa katika vokswageni ya Sikujua, gari la moshi lilijitokeza kwa ghafla huku likipiga honi kwa fujo kuashiria kuwa liko karibu kuwafikia. Mwalimu Baya aliyekuwa akiendesha gari akaamua kuongeza mwendo ili aweze kupita kabla ya gari la moshi kuwafika huku moyo ukimpapa. Lakini kwa ghafla, matukio ya kustaajabisha yanatokezea wakati gari lake linakata mafuta kisha kusimamishwa kimiujiza katikati ya njia ya gari la moshi. Baya anashikwa na kihoro kwani aling'ang'ana akijaribu kuwakisha lile gari bila kufaulu, kwani betri ya gari ilikuwa imekwisha kawi. Kutazama huku na huku anashindwa kuona chochote kutokana na mwangaza mkali uliotokana na taa ya gari hilo la moshi lililomfanya asione chochote. Mara moja akiwa na nia ya kumwokoa abiria wake, anamwamuru Mishi afungue mlango na atoke nje huku naye akijaribu kufungua lango lake lakini wapi! Walishangaa kupata kuwa milango wala madirisha hayafunguki. Kumtazama Mishi, anampata akiendelea kukaa kama amepigwa na bumbuazi huku akiwa ametulia tuli kama mtungi wa maji na kukaa ndii bila kuonyesha dalili yeyote ya kudhihirisha kuwa anahisi hatari iliyokuwa ikiwakabili. Kujaribu tena kufungua mlango wake atoke, bado ulikataa. Alijaribu njia zote kujitoa kutoka gari lile lakini hakuna kilichoweza kufua dafu na hapo akajua ametiwa mtegoni jambo lililomfanya ajilaumu kwa nini alimpa lifti binti huyo mwenye mkosi (uk.101-106).

Baya akiwa karibu kukata tamaa, alijiambia kuwa na liwe liwalo na akaamua atazame tena Mishi akitaka kujua ni nini alichokuwa akiwaza. Ya kustaabisha ni kuwa nguvu fulani za kimiujiza zilimshika alipokuwa akijaribu kusonga. Kabla tu wagongwe na gari la moshi, sauti ya kiajabu ikasikika kutoka kwa kinywa cha Mishi na hapo hapo gari la moshi likaligonga gari lao kwa nguvu na Baya akafikiria wamefikia mwisho wa maisha yao hapa duniani. Kwa muda wa sekunde chache, kila mahali kukanyamaza.

Yanayostaajabisha ni kwamba kwa njia ya kimazingaombwe, Baya anajipata na uwezo wa kutazama kila kitu na akaona mabehewa ya gari la moshi yakipita kwa kasi yakipasua katikati ya mili yao. Akaona ndani ya gari hilo la moshi mkiwa na viti viliviyokaliwa na mizuka na pia watu walio hai lakini wenye maumbo ya kutoeleweka. Kwa ghafla, kila kitu kikatulia na gari lao nao likiwa bado shwari. Baya akiwa katika hali ya kushagaa na kutoamin jinsi gari la moshi zima lingeweza kujipata likikata katikati yao bila kuwaua wala kukanyaga gari lao, anashindwa kufahamu kama alikuwa ndotoni au matukio hayo ya kimazingaombwe yamefanyika kweli, (uk. 107-108).

Muda si muda umazingaombwe unatokea tena Mishi anapotoka kwa ghafla kutoka ndani ya gari wakati gari likiendeshwa. La ajabu ni kuwa wakati alipokuwa akitoka nje ya gari Baya anasikia mlio wenye sauti ‘Kakro Kok Kakro’. Baya anajiambia kuwa Mishi alikuwa amevaa viatu vilivyokuwa wazi visivyostahili kutoa mlio huo. Anapotazama miguu ya Mishi ili aone ni viatu vipi vilivyokua vikitoa mlio ungedhani chuma kinagongeshwa gongeshwa sakafuni, moyo ukampasuka kwani alishangaa kumuona Mishi akiwa na miguu minne. Kuangalia vizuri, Baya hakuamini, miguu ya mwanamke yule imegeuka kwato za mnyama kama punda. Na mara moja Baya hakuhitaji ushahidi zaidi. Lo! Kusema ukweli, Mishi alikuwa jini (uk. 108-110).

Mbinu alizozitumia mtunzi katika uhusika umesababisha umazingaombwe katika usawiri wa mhusika Mishi kama mfano wa wahusika wa kimazingaombwe wanao patikana wakitekeleza matukio ya kifantasia wakiwa katika mazingira ya kiajabu.

Uwasilishaji wa kimazingaombwe ulizidi kutokezea tunapompata Baya akiendelea na safari yake huku akiendesha gari akijua kuwa yuko peke yake mara akasikia sauti fulani sikioni mwake ikimnong'onezea kimyakimya. Hapo akaaza kuwa na moyo wa bua na akawa na mwao kuwa ameingia katika mashaka tena. Akaamua kuendesha gari fulifuli lakini la kustaajabisha ni kwamba alipopinduka kutazama nyuma ya gari lake alimuona Mishi akitabasamu na kisha kujigeuza kuwa mdogo sana akawa kijitoto tu. Mara akatoweka tena. Mara sauti ndogo ya kike ikamwita na hapo nywele zake zikamsimama na mara moja akajua kuna tatizo bado. Pole pole akapinduka na kutazama kiti cha nyuma, alishangaa kumuona Mishi yule yule ameketi vizuri kana kwamba hamna lolote la kimazingaombwe lililokua limefanyika hapo awali. Baya kwa mara ya kwanza akaanza kujihisi kuwa huenda ikawa ameanza kurukwa na akili (uk. 112-114).

Kuna uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe kwenye mazingira ya kiajabu tunaposhuhudia tena Mishi na Baya wakijikuta baharini, wakiwa wamekumbatiana kimapenzi kwenye kitanda cha sufi kilichokalishwa juu ya maji. Baada ya kushiriki ngono, Baya anajaribu kujinyosha kitandani lakini akawa hawezi hata kusonga. Kutazama akashangaa kuwa Mishi tayari ametoweka. Kwa ghafla kitanda kile kikageuka kikaanza kupumua na Baya kujaribu kutoroka akajipata amefungiwa kwenye kitanda hicho jambo ambalo lilimtia shaka na kumzungusha kichwa. Wakati Baya anapojaribu kufikiria ndipo anaposhikwa na usingizi hapo hapo na kulala fofofo. Anaamka tena kutoka usingizini pale Mishi alipotamka jina fulani. Kilichomfanya Baya kushikwa na machugachuga ni alipojipata chini ya bahari huku amezungukwa na viumbe wenye maumbo ya kutatanisha na vilivyokuwa vikijaribu kumng'ang;ania kumfikia akiwa bado amefugwa kwenya kitanda kile kile. Baya alipokuwa akiwaza na kuwazua, Mishi akajitokeza kwa ghafla lakini la ajabu zaidi

ni kwamba, alimwona Mishi machoni mwake akijigeuza na kuwa jitu lenye macho matatu kwenye paji la uso wake likiwa limesimama kama twiga na kwato zake nne na papo hapo, Baya akajikuta roho inamtoka kisha akashikwa na usingizi tena (uk. 117-118).

Baya alipozinduka usingizini na kupata fahamu, akapata amepelekwa mahali ambapo hapajui kwenye nchi kavu akiwa amefungwa miguu na kuninginizwa juu ya mti mrefu kichwa chake kikielekea chini. Anapotazama vizuri, anagundua nguo zake zilikuwa zikininginia kwenye matawi ya mti uliokuwa mbele yake. Kujitazama, akashituka kujikuta akiwa uchi wa nyama (uk.116-118). Baada ya muda mrefu wasamaria wema wakamsikia akiomba msaada aokolewe. Wakamsaidia kuteremka na wakampa shuka ili aweze kujisitiri. Waokolewaji hao wakamchukuwa apate hifadhi kwa mzee wa kijiji aliyemwomba amuelezee kisa chake chote kutoka mwanzo hadi mwisho. Mzee yule akamushauri kuwa njia ya pekee iliosalia ni kwenda kwa mzee ajulikanaye kama Sheikh ili aweze kusikia kisa hicho na kujua yatakayomtokezea kisha kumuagua. Baya akiwa na hamu ya kujiondoa kutokana na mambo haya, akashika njia kwenda kumtafuta bwana yule akiwa na imani kuwa mashaka yake yote yatatatuliwa mwishowe. Lakini cha kushangaza ni kuwa Baya baada ya kupitishwa kwa mambo hayo yote wa kimazingaombwe, anaamka kutoka usingizini akiwa amerudishwa kwake. Baya hakugundua ama alikosa kuamini kuwa mambo hayo yote ya kimazingaombwe yaliyokuwa yakimfanyikia yalikuwa mawazoni mwake tu jambo lililomkera sana (uk.112-121).

Mtunzi amesawiri pia wahusika wenye matukio ya kimazingaombwe yanayofanyika katika vyuo vikuu na hata katika shule za upili. Anatumia fursa hii kusababisha uwasilishaji unaohusu mambo yanayoweza kutokea katika jamii yetu ili kuwawezesha wahusika wake kuelimisha jamii hasa wanafunzi wasije wakajihusisha na mambo yatakayoharibu mielekeo

yao ya kimasomo na hata kimaisha kwa jumla. Anawashauri wanafunzi kwamba kukiwa na jambo la lazima linalowalazimisha wafanye maandamano, basi wafanye kwa uagalifu mno. Mtunzi akifanya usawiri wa aina hii pia akilenga kuleta funzo kupitia wasomaji utakao enea kindanindani na mwishowe kuwekea kikomo tabia zinazohusu mipango ya maandamano katika vyuo mbalimbali hasa vya nchi za kiafrika, jambo ambalo lingali likifanyika hata wakati wa leo (uk.121-123).

Tumepata kuona umuhimu wa uwasilishaji wa aina hii pia katika kuelimisha jamii nzima hasa kuhusu migomo inayofanyika mara kwa mara katika viwanda mbalibali. Kitendo hiki ambacho wakati mwingine husababisha wafanyikazi hasa katika makampuni, mashirika au vikundi fulani vya kibinafsi kupoteza ajira. Makampuni kama hayo kwa mfano ni kama makampuni barani Afrika yanohusishwa na wachuma majani chai na pia makampuni yanayohusisha uzalishaji wa zao la kahawa na makampuni mengine mengi. Migomo hiyo husababisha kusambaratika makapuni hayo, moja baada ya nyingine bila mpangilio.

Uwasilishaji wa ujumbe wa wahusika wa kimazingaombwe unafanyika wakati mhusika Yunasi alipokuwa akifanya kazi katika nchi za ng’ambo. Ni tukio la kustaajabisha wakati Yunani anapatikana akizungumziwa na sauti inayotoka kutani na haoni mtu yeyote na akashindwa kuelewa kama yeye anaota mchana au amepatwa na kichaa bila kujua. Sauti hiyo inamkumbusha kuwa ataadhibiwa kutokana na tabia yake mbaya na wizi wa pesa za kanisa na kuhusisha wasichana wadogo mambo ya uzinzi wakati alipokuwa kasisi katika kanisa fulani. Ni umazingaombwe pia anapojaribu kusoma Biblia Takatifu pale anapohisi uwepo wa mtu anayesimama nyuma yake kisha kukiweka kitambaa cheusi mbele ya macho yake na hivyo kumzuia asisome Biblia. Yunasi akiwa na akili zake timamu na kama mhusika mkristo

halisi ana imani kuwa kuna nguvu za kiajabu katika jina la Mungu Mumbaji na wote wanaloliita jina lake wanaokolewa. Yunani anachukua hatua ya ujasiri, anapiga magoti chini ili apate kuomba. Lakini anapojaribu kufunga macho kuomba anashangaa kusikia mlio wa watoto wengi wachanga. Kutazama, anaona amezungukwa na maiti za akina mama na kila mmoja wao akiwa ameshika mtoto mkononi. Kwa ghafla maiti zile zinafufuka na kila mmoja kumtupia mtoto akitamka *'shika, ni wako!* Yunani hata hivyo akakazana kuomba, (uk.149-154).

Umazingaombwe unaotokea mawazoni mwa mhusika Hikmat. Hikmat ambaye anajihusisha na mambo ya utangazaji na uigizaji wa michezo kadhaa katika runinga, amesawiriwa kutekeleza matukio ya kimazingaombwe. Hikmat amesawiriwa kuwa mhisika mwenye nafsi kadhaa. Anapopanga wahusika katika mchezo wowote ule, yeye mwenyewe anajigeuza na kujitekelezea matukio akiwa wahusika wote wanaohitajika katika igizo hilo. Akiwa runingani, anachukua nafsi ya kila mchezaji na kutekeleza matendo ya kimazingaombwe bila watazamaji kugundua kuwa wahusika hao wote ni nafsi ya mhusika mmoja anayebadilikabadilika. La ajabu zaidi ni kuwa muda si muda watazamaji walipokuwa wakijiburudisha, kitendo cha kimiujiza kinatokea ghafla wakati Hikmat anapoamuru nafsi hizo zote zake zijibadilishe na mara zinageuka na kuwa wanyama mwitu runingani na watazamaji wakashikwa na bumbuazi. Isitoshe wanyama wale moja kwa moja wakajitokeza nje ya runinga na kuanza kufukuza watazamaji huku wakitishia kuwala. Baada ya kutawanyika kwa muda, mara mambo yanarudi kuwa sawa tena na watazamaji hao wanajipata wakirudi na kuendelea kama kawaida. Watazamaji hao wanapotezewa akili kila mmoja wao akishangaa asijue ni nini nini kilichotokea (uk.170-171).

Tumepata uwasilishaji wa kiuhalisiajabu pia wakati wahusika wa kimazingaombwe wanasawiriwa kuashiria hali katika jamii inayowapa wananchi mateso na kuwakosesha

amani. Mhusika Ikmat amesawiriwa kuchukua nafsi ya mhusika mwenye huruma na anayefafanua jinsi wananchi walivyojawa na huzuni wakiona jinsi wanavyothakilishwa na kudharauliwa na kwa kunyimwa matunda ya uhuru. Wananung'unika wakilazimika kudhihaki uwepo na uwezo wa Mungu wakishangaa jinsi anawawacha watu waliofanikiwa kuwa na mali wawe kupe. Wanasahau kuwa wao pia ni wanadamu hata ingawa wameumbwa wawe na ngozi nyeupe. Hawakupenda jinsi Wazungu na Wahindi wanawadalilisha na kuwaita barnyani yani nusu nyani nusu mtu eti kwa sababu ya ngozi nyeusi ya Mwafrika (uk.171-172).

Mtunzi katika usawiri na uhusika anabandika taswira ya kifantasia katika mawazo ya msomaji. Mwandishi anafanya hivo kwa kusawiri uwasilishaji utekelezwe na wahusika wa kimazingaombwe na kuwawezesha wafanye matukio ya kimiujiza yanayosababisha wasiwasi na hata kutia wayowayo kwa wasomaji kwani uwasilishaji unabeba ujumbe wenye matukio yasiyowezekana wala kuaminika katika muktadha wa jamii ya kawaida.

Tumepata pia matukio ya kimazingaombwe yanayofanyika kutokana na uwasilishaji wa ujumbe wa mhusika Lakeisha. Ya ajabu ni kuwa Lakeisha anashuhudia matendo ya kimiujiza anapopita katika kijiji kimoja ambapo wanawake wanakatakata mikono ya watoto wao kisha kuining'inisha kwenye viingilio vya nyumba zao. Aliposonga kutazama vizuri, anawaona viumbe wenye sura za kutatanisha wakiingia ndani ya chumba kimoja kilichofanywa kiwanda cha kugeuzia watoto wale wawe wanyama wenye maumbo ya kutisha. Viumbe hao wakishageuka maumbo wanageuzwa tena na kuwa maingatinga kisha kupelekwa na kuamuriwa kulima mashamba ya wazungu huku wakitumia damu badala ya petroli. Ajabu pia ni kwamba akina mama waliowazaa watoto wale wanakubali kushiriki mambo ya

kishetani kisha tena kushtaki hali huku wakijitokeza na kupiga mayowe, wakivua nguo zao na kutembea uchi. Baada ya muda si mrefu, watoto wao wanafufuliwa tena kisha kurudishwa katika hali zao za kawaida na huu kweli ni umazingaombwe kwani jambo hili hufanyika tena kila mara wanapohitajika kukiwa na kazi ya ukulima.

*Watu wa Gehenna*, pia inawapa wahusika wa kimazingaombwe jukumu la kulinda gereza na kusimamia mahitaji yote ya kiajabu yanayohusu wanadamu. Jambo la kimiujiza ni kuwa wahusika hao wamesawiriwa kuwa na uwezo wa kubadilikabadilika vilivyo kuligana na jinsi wanavyotakikana wawe ndio waweze kushughulikia mambo fulani. Wakiwa na shughuli ya kufanya huko angani mara moja wanageuza wawe na mabawa na wawe pia na uwezo wa kuruka na hata kuishi huko hewani kwa muda wote wanapotakikana kuwa huko. Wakiwa na shughuli ya kufanya baharini wanajigeuza wawe meli, nyangumi ama mnyama yeyote ya baharini. Wahusika hawa vilevile wana uwezo wa kumulika kila mahali ulimwenguni wakitafuta watu wanaomcha Mungu. Wanapowapata, wanawapangia vifo. Wanafanya hivyo kupitia ajali za barabarani, za ndege au wafe kutokana na mizozo ya kikabila katika jamii. Mahakamani wahusika hao aidha wamepewa vyeo mbalimbali na kila kikundi kina jukumu lake na wanasawiriwa kuwa na uwezo wa kutatua mahitaji yao yote kulingana na mpangilio wa jaji wao mkuu (uk.187-189).

Katika mazingira ya mahakama hii pia, Bi. Saeeda na Bi. Balira wanasukumwa kwa nguvu pembeni mwa rusu au mstari wa vitu vya kimazingaombwe ambavyo vimepangwa kimoja juu ya kingine huku maandishi yaliyoandikwa kwa moto mkali yenye maneno ‘mwanzo wa jehamanu,’ mahali walipokuwa wametesewa hapo awali wakiwa wafanyikazi wa nyumbani pamoja. Wanaendelea kuchapwa kisha wanawachiliwa kupiga soga kana kwamba wako pahali pa starehe. Mara Baingama anasikia sauti ya mamake Lakeisha ikimwita na anashtuka

anapogundua hayo yote yalikuwa ndoto tu na kumbe alikuwa amelala usingizi mzito ulioambatana na jinamizi kali.

Mtunzi ametumia umazingaombwe huu kwa kumshirikisha msomaji na kututurisha moyo na kujipata akijiuliza na hata kufikiri kama labda alichosomo kilikuwa ni ndoto ama kweli si ndoto, (uk.189). Mwandishi pia kwa kuwasilisha ujumbe wa uhalisiajabu katika ndoto ya aina hii anamulika jinsi hali mbaya unavyotekelezwa na viongozi katika jamii huku wakifanya maovu kwa njia ya kimazingaombwe. Kwa mfano tumepata kuwa wanasiasa, wafanyi biashara na watu wasio na utu wanatumia viwiliwili vya zeruzeru kupigia ramli ili wajitajirishe huku wakipuuza haki za zeruzeru na kuwaona hao si chochote si lolote na hata kufikiria kwamba hao sio binadamu kamili. Katika mahakama hii, mavazi mekundumekundu yanayovaliwa na mahakimu na machozi ya damu yanayotiririka machoni mwa washukiwa yanadhihirisha kuwa kuna majuto na mashaka ya kiajabu mle gehenna (jahanamu).

Tukio jingine la kimazingaombwe linafanyika katika mazingira ya hospitali wakati madaktari, wachungaji na wahudumu wa chumba cha kuhifadhia maiti wanashirikiana na wafanyibiashara haramu wawe wakikata viwiliwili vya maiti bila idhini yao. Wanaelewa wazi kuwa wanadamu wanaogopa binadamu wenzao wanapokufa na hivyo wanapozichukua maiti zao wanajawa na huzuni na hawana nafasi ya kuangalia vizuri sehemu zote za mwili kabla ya maiti kuwekwa kwenye jeneza.

Ni umazingaombwe pia wakati mhusika kasisi Taabu anayedhaniwa kuwa yeye ndiye wa kuokoa watu kutokana na maovu ikawa yeye kumbe ni ibilisi. Yeye anapanga ajali mbaya ifanyike ili watu wengi wafariki na waweze kupata miili itakayowafanikisha kibiashara.

Baada ya ajali kufanyika, anakimbia huko mara moja kuwahubiria watu ambao wamenusurika kutokana na ajali hiyo na hata kupanga kuhudhuria mazishi ili ajifanye mnyenyekevu huku akitoa rambirambi zake akiwaambia waombolezaji wasitie shaka ‘kwani yote ni mipango ya Mungu (uk.199). Wanabiashara hao waovu wanatoa ndimi, masikio, macho na sehemu nyeti na kuweka katika friji na baadaye kuuzia wateja wao kwa bei ya juu. Mara magazetini tunapata vichwa vya habari vikiwa na jumbe za kutatanisha kuhusu wizi wa viungo vya sehemu nyeti za miili ya watu kutoka vyumba vya kuhifadhia maiti na wahubiri wakiombwa kuendelea kuombea jambo hili. Ajabu ni kuwa zeruzeru wanauawa bila huruma ili viongozi wafanikishe biashara za viungo vya mwili na kujitajirisha. Wanasiasa hao wakitaka kujipatia kura kwa wingi lakini hawana habari kuwa wamemaliza zeruzeru ambao wangewapigia kura (uk 200).

Umazingaombwe zaidi ni kuwa vifo vingine vinafanyika wakati umati wa watu umekusanyika kuhudhuria mikutano ya kisiasa kwa azma ya kusikiza sera za viongozi wao. Viongozi hao huwa wakiandamana na watu wanaojifanya kuwa waganga sugu, kumbe ni wachawi wanaojihusisha na nguvu za giza (uk.208). Mwandishi anatambulisha kuwa tabia ya kuamini mambo ya uchawi ni ushirikina tu, uwe ni wa utabiri wa nyota, matumizi ya damu na viungo vya albino, kupiga ramli na kadhalika yote ni ushirikina. Tukiendelea kutazama uwasilishaji wa kimazingaombwe wa Baingama, tunapata kuwa nafsi yake inawaomba wananchi wote wapuuze ushirikina lakini kinyume ni kwamba anasema kuwa ni sawa kuamini katika biashara ya uuzaji wa sehemu za mili ya wafu na hasa mili ya albino. Anageuka kuwa mhubiri akiendelea kusema kuwa kifo ni jukumu lake Mungu na ndiye aliye na uwezo kumpaa uhai kwa binadamu. Anaendelea kujifanya mhubiri akisema kwamba ni jukumu la aliyeumba mwanadamu atakayeamua ni lini ataruhusu uhai huo utolewe na kwamba kifo ni siri ya Mungu (uk.210).

Katika mandhari ya mahakamani, umazingaombwe unatokea wakati Takosani na Sikujua wanashtakiwa kwamba wamesababisha kifo cha mwenazao Yunasi pamoja na vifo vya kila mtu katika familia yake. Takosani anajitetea na anakiri kuwa yeye ni mfanya kazi wa Shetani na kwamba amekuwa akiwasiliana naye tangu akiwa mtoto mdogo na kwamba yeye pia anatawaliwa na nguvu za giza za ajabu na kuwa ameweka imani yake kwa msingi wa kitabu kimoja fulani cha Shetani. Katika mazingira haya, tunaona wakili wake akimtetea kwa sheria zinazowalinda wenye matatizo ya kiakili lakini kwake Takosani anasisitiza kuwa yeye si mwendawazimu lakini kweli ni kwamba yeye ni mwenye imani ya dini ya kishetani (uk.212-218). Hapa, tunaona kuwa mtunzi anatoa mwanga kuonyesha wazi kuwa mawakili hutetea washukiwa au wateja wao hata kama wamefanya makosa bora tu wapewe hongo na wajinufaishe.

Umazingaombwe umejengeka zaidi wakati tunapopata mahakama ya Gehenna inapozidi kutoa amri kwamba watu wote waliotenda dhambi duniani kwa njia yeyote ile wahukumiwe vikali kwa njia ya kutisha. Kuna ujeuri fulani baina ya wahusika wawili wakuu, Munkari na Nyamaume pamoja na wahusika wengine wa Gehenna. Khan amesawiriwa kama mhusika hewa asiyeonekana kwa macho. Jukumu lake kubwa ni kuwa katika mchezo unaochezewa mawazoni mwake. Kwa kutumia umazingaombwe wake anapuliza baragumu na kuwaita watu wa Gehenna waje mkutanoni wapewe ujumbe maalum.

Mhusika Munkari anahutubia umati wa watu akiwa amebeba nguruwe mnono kwelikweli na mkoba mkubwa wenye mafuvu ya vichwa vya watu. Wanaohutubiwa wanalia na kutoa sauti kama za popo, lakini ni wakati wa kupewa mhadhara kwa dhambi walizotenda wakati walipokuwa duniani (uk.221). Munkari anawaambia kuwa wako pale kwa hiari yao kwani

hawakuletwa na yeyote lakini anahojiwa kwa sababu, ingawa wamekwishakata roho wao ni *'The living dead,'* yaani wafu wanaoishi (uk.221). Anatoa maelezo kuwa shughuli zao ni kutekeleza uongozi mbaya unaosababisha nchi hususan za Kiafrika kuyumbayumba. Pia alisisitiza uharibifu wa mali ukomeshwe katika taifa akieleza kuwa mambo yasiyokuwa ya uadilifu hayana ustawi wala maendeleo katika jamii (uk.222). Mhusika huyu wa kiajabu amechukua nafasi kueleza kuhusu athari za utandawazi ambapo mafisadi huhamisha utajiri wa Kiafrika kwenda kutajirisha nchi nyingine (uk. 224).

Mchezo uitwao *'corruption'* ambao unafanyika katika fikra au mawazoni mwa Bi. Saeda nao unawasilisha ncha nyingine ya umazingaombwe wa *Watu wa Gehenna*. Mwandishi, akiangazia maovu yanayotendeka katika nchi za Kiafrika, anatumia mhusika huyu wa kiajabu kutekeleza matendo ajabuajabu huku wananchi wakifanyishwa matukio ya kimazingaombwe na kuwapitisha katika majuto makali. Viongozi wanaoshiriki ufisadi wanapanga mkutano kisha wanawahutubiwa wananchi hao na wakati huo huo, wanafanyishwa umazingaombwe na kupotoshwa kiakili ili waweze kukubaliana kuwa wamefanyiwa kazi inaogarimu pesa nyingi ilihali si kweli. Wanaamuriwa wasiwe na uwoga kama nyamaume ama wavuviwe motoni (uk. 242). Kila mmoja katika umati ule anatulia akifikiria wamepewa ushauri wa mabomba lakini wapi, hali ni kwamba wanaandaliwa majuto ajabuajabu. Nyamaume anajitokeza mara moja kisha anavuvia moto maradufu na kilio kikali, mayowe na sokomoko zinaongezeka kutoka kwa wanaohutubiwa. Viongozi hao waovu wanafanya hivi ili waweze kupata ushahidi wa kutumia katika kulaghai wizara ya fedha kuwapa pesa hizo kisha wagawane. Mchezo huu wote unafanyika mawazoni mwa Bi Saeda Khan ambaye ni mmojawapo wa watu wa Gehenna.

Kuna safari ya kimazingaombwe ya kuelekea Naigerai. Abiria wamejazwa gari kupita kiasi. Dereva naye anaendesha gari kwa kasi zaidi, kilomita 666 kwa saa moja. Gari linaingia kwenye shimo barabarani na dereva anashindwa kulidhibiti, mafuta yanavuja na moto kuwaka na kwa ghafla mlipuko mkubwa kusikika huku moto ukisambaa haraka na kuteketeza abiria. Ni hali ya umazingaombwe kuwa abiria mmoja kwa jina Angamizamtuwewe hakuchomeka hata kidogo. Tukio hili linafanyika huko NdaRwa na mara moja watu wa Gehenna wanafika penye ajali huku wakisherekea na kuihesabu mifupa na kisha kupanga kutoa hukumu kwa wateja wao wapya (uk. 243-250). Matukio mengi yanafanyika katika mandhari ya ndotoni hata ingawa mambo mengine katika hali halisi yanaonekana kuwa kuna uwezekano kuwa yaliwahi kutendeka.

Kuna umazingaombwe naye Faki Nahodha anapozindushwa na mlio wa arafa ya ujumbe fulani unaotoka kanisa analohudumu kasisi Taabu akitakiwa huko mara moja kwa mipango ya mazishi.Kasisi Taabu alipatikana akiwa amekufa kanisani akiwa amejitoa uhai yeye mwenyewe. Anapofika huko kanisani, anashindwa kuamini alichokiona. Badala ya maiti ya kasisi huyo kuzikwa, la kushangaza tena ni kwamba kasisi huyo mfu anapatikana akinywa chai, huku akisoma gazeti la *The Tombstone Epitaph.* Muda si muda, kasisi Taabu anajaribu kuwasiliana na Nahodha papo hapo anazinduka na kukosa kufahamu ni nini kinachofanyika. Faki anashangaa kwani kadhia hiyo yote inafanyika mawazoni mwake (uk.253-257).

Ni umazingaombwe pia wakati nafsi ya Hikmat inapochipuka tena na kujizungumzia yenyewe na hata kujiuliza maswali kisha kujijibu. Ni hali ya kimazingaombwe kupata mhusika huyu akijadiliana na nafsi yake na hata kutoa maamuzi.

Mara binti Abadalla mkewe Takosani, anamwamsha Eks. Eks naye anaamka akishituka huku akionekana kama alikuwa kwenye ndoto ya kutisha. Na kweli yeye alikuwa katika dunia nyingine na anapoamka, anajipata akiwa amerudi katika dunia halisi lakini bado anakakaa akiwa na taaradhi. Ni tukio la kimazingaombwe jinsi mhusika huyu anavyobadilika kwa ghafla na kuchukua maumbile au umbo la wahusika wengi tofauti tofauti. Alichokuwa akitamani kujua au kufichuliwa nini kilichotokea hasa na ni kwa sababu gani. Mara anaingiwa na wasiwasi huku akiwaza mara anagundua kumbe matukio yale yote yaliyotokea ni dhahania tu. Alichokuwa akikumbuka ni kuwa kabla ya kupatwa na usingizi ule mzito uliomzamisha katika ndoto hii ya kutisha, alikuwa amemaliza tu kusoma kuhusu watu waliopatwa na maafa kisha kutumbukizwa kwenye bahari kubwa ya moto mkali wakiwaka kama kuni zinazowaka daima wakijuta bila mwisho wa adhabu zao.

**4.2 Uwasilishaji wa Wahusika Wakuu wa Kimazingaombwe**

Uwasilishaji wa wahusika wakuu huchukuwa nafasi kubwa katika utendekaji wa kazi katika shughuli za kisanaa. Wahusika wakuu ni viumbe wanaosawiriwa kutekeleza majukumu makubwamakubwa wakisaidiwa na wahusika wadogo kukamilisha au kusisitiza wajibu wao. Wakieleza kuhusu uwasilishaji wa wahusika wakuu, Njogu na Chimerah (1999) wanasisitiza kuwa ni jambo la kimsingi kulingana na kanuni za kisanii. Wataalamu hawa wanasema kuwa wahusika wakuu ndio viumbe watenda kazi katika sanaa na ni wao ambao wanasababisha matukio makuu. Azimio kuu la watunzi katika uwasilishaji wa ujumbe wao huwa ni wajibu wa wahusika wakuu. Malengo yaliyomo katika mpangilio akilini mwa waandishi huwekwa wazi kupitia mbinu za uhusika na katika mbinu za usawiri wa wahusika wakuu wakiwa na mwingiliano unaofaa kati yao na wahusika wadogo ambao lazima wakweko ili wakamilishe kazi zao.

Kutokana na mawazo haya, mhusika mkuu huumbwa na kusawiriwa kimakusudi kutekeleza majukumu fulani anayodhamria mtunzi katika fasihi. Matendo au matukio ya mhusika mkuu au tuseme hisia zake zozote zile zinatolewa na kunadhibitiwa kwa kiasi kikubwa na dhamira ya mwandishi mwenyewe katika kazi zake za kifasihi. Kuna wahusika kadhaa, wahusika wakuu na wahusika wasaidizi wanaojitokeza katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Mhusika K

Mhusika K ni mmojawapo wa wahusika wakuu aliyesawiriwa na mtunzi Mohamed katika riwaya yake ya *Babu Alipofufuka.* Achukue sehemu kubwa ya shughuli za uwasilishaji wa ujumbe katika kazi yake. Mzuka, ambaye ni mzuka wa babu yake K, ametumiwa ili amwezeshe mhusika K kutekeleza matukio ya kimazingaombwe ambayo yanadhihirika riwayani kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi.

K ni mhusika wa kimazingaombwe na mambo ya kifantasia yalianza kumtokelezea kupitia kwa matendo ya kimiujiza kutoka kwa Mzuka, babuye aliyefariki kitambo lakini roho yake imesalia ikimsubuasumbua mjukuu wake. Uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe ulisawiriwa kwa kutumia mbinu za kimiujiza katika uhusika. Uwasilishaji wa ujumbe katika hadithi nzima inasimuliwa na wahusika wa kimazingaombwe kwa njia ajabuajabu na yenye matukio ya kustaajabisha.

Huyo Babu wa K ambaye ni mzuka aliyekufa zamani kisha akafufuka, anajitokeza kwa umbo la ajabuajabu mawazoni mwa mjukuu wake. Nia ya Mzuka ni kumwandama mjukuu wake kwa kumtatiza na kumfanyisha vituko vya kutatanisha na kumsababisha akose mwelekeo. K mwenyewe ni mhusika ambaye amesawiriwa kama sehemu ya viongozi wabaya ambao uongozi wao haufurahishi wananchi. Kwa ustadi wa hali ya juu, msanii Ahamed amesawiri

babu wa K kwa kumpa jina Mzuka kwa sababu yeye kweli ni mzuka kisha kumpa nguvu za kimiujiza ambazo anazitumia kwa kusababisha uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe.

Mtunzi anatumia fursa hii ya uwasilishaji wa kimazingaombwe kuonyesha hali katika ulimwengu ambao maisha ya watu inaongozwa na kuelekezwa na aina mbili za imani. Ya kwanza ni imani unaoashiria mambo yanayofanyika katika jamii kubainisha ukweli wa mambo na nyingine ni imani inoashiria hali ya kimazingaombwe ambapo mambo yanayotokeleza katika jamii ni ya kimiujiza na hayaeleweki wala kuaminika. Hali hii katika uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe ndipo msomaji katika sanaa anaweza kupata ujumbe kwa kupitiziwa picha au vitu inayomjia mwazoni mwake yakiwemo maono na jazanda au taswira. Mambo ya kiajabu yanayoleta wasiwasi na hali ya kificho waliyonayo wahusika wa kimazingaombwe yanafanyika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* wanapotekeleza uwasilishaji wao.

Umazingaombwe katika uwasilishaji wa wahusika wa kifantasia unajitokeza mara ya kwanza kabisa katika ukurasa wa 13 hadi 16 katika riwaya ya *Babu Alipofufuka.* Hapa tunakutana na maelezo kuhusu mhusika K ambayo yanawasilisha majivuno yake ya kujitakia makuu na kupandishwa kwa cheo hivyo tu bila kanuni ama kufuata taratibu za uajiri kama ilivyo kawaida ya viongozi wenzake wasio na utu.

K katika maisha yake hapo mwanzoni, alikuwa na nia nzuri ya kufanyia wananchi katika jami kazi ya maana kwa azma ya kuwa kiongozi siku za usoni. Alipokuwa mdogo K aliwahi kuota na kujipata akiwa ameajiriwa na serikali na akapewa gari kubwa la kifahari na kwamba alikuwa akiwaheshimu watu wote katika jamii na kila mtu alikuwa akimpenda katika eneo lake la uwakilishi. Anageuka baadaye na kuwa msahaulifu mno kwani alipopata kazi na

kupandishwa cheo, alisahau ahadi yake ya kukumbuka wanyonge na maskini na ya kuweza kumfaa kila mtu katika jamii.

K anajiona kuwa yeye ni tofauti, hajioni kuwa yeye ni mwanadamu wa kawaida na anachotaka sio kukwea miti kwa utaratibu bali ni yeye kutaka kuruka juu na kugusa mbingu hata bila ubawa. K pia anajigamba kuwa yeye si kama mhusika Protectus ambaye daima anashinda akishughulikia masihahi ya watu wengine.

Tumepata kuona kuwa mhusika K ni mhusika wa kimazingaombwe anayejiona mawazoni mwake kama ni mweza yote katika jamii na kuwa yeye ni mtegemewa kwa kila kitu na kila mtu katika jamii kana kwamba asipokuwako maisha yanaweza kusimama. Mawazoni mwake pia anajihisi hawezi kufa na anashangaa watu wanaomtegemea wangeishi vipi baada ya kifo chake.

Umazingaombwe wa K pia unadhihirishwa kwa kule kubadilika mara tu anapoingiliwa na Mzuka, babu yake na kugeuza mwelekeo wa maisha yake. Anastuka anapojipata akipitizwa na mzuka wa babu yake katika mambo mengi ya kimiujiza ambayo yeye anajihisi kuwa hana uwezo wa kijiokoa kutokana na mtego huu. Anajisumbua kuona kuwa amepokonywa hata uwezo wa yeye kumwamuru dereva wake kwani babu huyu wake K amechukua mamlaka yote. Mzuka anahangaisha K na kumbadilishabadilisha apendavyo hata kumgeuza mnyama na kusababishwa kutishikatishika huku mwili wake ukiwa kama upongoo kwenye kuti la mnazi.

K ameendelea kufanyishwa umazingaombwe mara kufanyiwa mambo ya kumfurahisha kwa muda kisha mambo yanamgeuka tena na kufanyiwa mambo ya kumshtua. Anazungushwa

kiakili huku akiwaona watu wenye maumbo ya kutatanisha wanaomtisha kuchukua maisha yake kudhihirisha ghadhabu wao. K anaonyeshwa nyuso za watu wengi zinazotoa ishara kuwa wameuthika. Hawa ni pepo wake wanaopinga uongozi wake mbaya katika jamii na ni onyo kwa K na wenziwe kuwa hawawezi kamwe kuukimbia ukweli. Mtunzi anamsawiriri K pia ajionee umazingaombwe wa dereva wake akijibadilisha sura kwa njia ya kiajabu na kupewa nguvu aweze kumbeba popote kwa mkono na wakati mwingine kumfanya kiti chake.

Mhusika K pia anasawiriwa kuendeleza umazingaombwe wake huku akistuka kwani mawazoni mwake anahisi kuongeleshwa na kusikia sauti inayofanana na yake ikimwitamwita kisha kujipata akitumbukizwa kwenye shimo lenye maji ya barafu. Anajaribu kuwaita walinzi wake wamsaidie atoke shimoni lakini kila mmoja wao akimtazama tu na kumcheka - jambo ambalo lilimfanya afoke maneno huku akiwa amechukizwa lakini walinzi wake hao wakamtia biri. Mara K anatambua kuwa anaandamwa na mahasimu wake wengi wanaotaka kulipiza kisasi kutokana na mambo mabaya aliyowatendea akiwa uongozini na hapo akatia hasira kujua kuwa ametiliwa dhiki ya roho (uk.22-28).

Mhusika K amesawiriwa pia kama kiongozi anayewapenda wageni kuliko wenyeji. K kwa muda anasawiriwa kama mhusika tajiri mwenye hoteli ya kifahari ambapo anafurahi kuwapokea wageni wanaotoka nchi za ng’ambo na wakati huo wote hakujali kuwatambua raia kutoka jamii waliokuwa wakija na kusimama langoni siku kutwa kila siku wakijaribu kujipatia nafasi nao wawaone wageni hao na labda mahitaji yao yaangaliwe.

Kwa ghafla matukio ya kimazingaombwe yanamtokelezea K tena anaposawiriwa kuingiliwa na mzuka wa babu wake ambaye amejigeuza mnyama mwenye sura ya kutisha na ambaye

kwa sauti ya kutisha anamwambia K kwamba ni yeye (K) aliyepuuza watu wake na kujileta mwenyewe kwenye makao yake ya maficho na hivyo ataona cha mtema kuni na kilichosalia ni yeye kuomba utajamali. K kutokana na jambo hili amepitizwa kwenye mateso mbalimbali na yule mnyama mbaya tena mkali wa kupindukia. Hapa tunapata kuwa mtunzi alikuwa amemsawiri K kama mhusika wa kimazingaombwe ambaye amejisahau na hata kusahau mambo muhimu yanayopaswa kufuatiliwa kulingana na mahitaji ya kimila na tunavyofahamu, mwacha mila ni mtumwa (uk. 35-39).

Mtunzi amesawiri mhusika K pia kama kiongozi mbadhirifu wa mali ya umma na kama kiongozi anayeongozwa na wageni wakora kutoka ng'ambo. Anadanganywa na kupotoshwa kutoa mali ya serekali kwa minajili ya kuanzisha miradi mbali mbali isiyo na manufaa kwa raia katika jamii. Kwa njia ya udanganyifu wageni hao wanachukua pesa wakijifanya kuwa wamechukua kandarasi na kwamba wameifanyia serikali kazi ya maana ilhali ni uwongo. Majukumu ya wageni hao walaghai ni kuanzisha tu hoteli ambapo watu wanapiga mtindi huku wakijishughulisha na matendo ya uasherati na mambo mengine mabaya yasiyokubalika katika jamii. K alipounga mkono mradi huu, hakuweza kufikiri kuwa watoto wake nao wanaweza kunaswa hapa na kutoka bila kujiingiza mtegoni. Tayari mabinti wa viongozi wengi wanaonekana wakiingizwa katika mambo machafu ya uasherati katika klabu hii - jambo ambalo lilimfanya Mzuka kuwaonya kuwa kutokana na maovu wanayoyafanya, lawama litawafikia na hata hadi kufikia wajukuu na vitukuu wao lazima hukumu itawaangukia wapende wasipende (uk 42-45).

Mtunzi anasawiri Mhusika K pia kuhisi mawazoni mwake kwamba muda wote wamekuwa na babu wake ni muda mrefu sana na huenda kwamba hautakuwa na mwisho. Hali hii katika uwasilishaji wa kimazingaombwe unaashiria mvunjiko wa mahali na wakati (uk. 93-95).

K vilevile amesawiriwa kama mhusika wa kutekeleza umazingaombwe kutokana na uwezo wake wa kuwa na nafsi zaidi ya moja. K ana uwezo wa kubadilika na kuchukua nafsi ya mhusika anayeshughulikia mambo ya kawaida katika jamii kisha kugeuzwa na kusababishwa ashiriki katika mambo ya kimazingaombwe. Mara, kwa mfano, twapata mtunzi akimfanya K akubali kulazimishwa kutumia kinyago cha kuvalia usoni kisha anaamrishwa kujiua kwa kujikaba koo na ajiangushe chini kama amekata roho tayani. Anasawiriwa pia kuitikia amri za babu yake anayemfufua na kumgeuza awe na umbo la mchwa kisha kufanywa kuwa na uwezo wa kuingia ulimwengu wa kimashetani kwa njia ya kiajabu (uk. 81- 87).

Umazingaombwe wa mhusika K pia akiwa kiongozi katili unaonyesha uwezo wake wa kufanyisha watu mambo ya kifantasia kama vile kuwageuza watu buku wenye matukio ya kimazingaombwe yanayosababisha uharibifu wa nyumba za watu vijijini ili wenyeji watoroke nao wapate ardhi ya kuuzia wageni kutoka nchi za ng’ambo.

Mtunzi anakamilisha hadithi yake kwa kumsawiri mhusika K kudhihirisha majuto makali wanayopata wote walioshinda kukimbilia roho hata baada ya kupata onyo. Riwaya inamalizika pia kwa kumuonyesha kuwa K mwishowe aligusa manda na akapoteza kila kitu katika maisha hadi kupoteza maana ya kuishi, akiwa na kichwa bupu huku akilalia mate - jambo ambalo mwishowe lilimsababisha ajitie kitanzi kwa kukosa kuona maana ya maisha tena. Hivyo ndivyo umma unavyomhukumu na kuzungusha kichwa mkosaji wake (uk.164-166).

### 4.2.2 Mzuka

Huyu ni babu wa K ambaye, kama jina lake linavyoakisi, alifariki zamani na kisha akafufuka. Mzuka ni mhusika wa kimazingaombwe aliyesawiriwa kuwa na nafsi yake daima kama pepo, kiumbe asiyeweza kuonekana kwa macho ya watu ila tu kwa sauti yake. Mtunzi amesawiri mzuka huyu atangulie katika hadithi kwa kuzungumzia mjukuu wake K akimwambia kuwa nafasi ilioko kati yake na yeye si kubwa huku akimaanisha uhusiano walionao ni wa damu na kwamba ingawa aliaga dunia kitambo bado yu karibu naye na kuwa yuko na uwezo wa kumfikia kila hali. Jambo hili linawekea msomaji kikwazo ambacho ni kitendawili lakini mwishowe watafumbua fumbo hili baadaye kwamba sauti hii ni ya babu yake K.

Mtunzi katika hii hali ya umazingaombwe, amesawiri Mzuka aweze kuwasilisha ujumbe wake akinuia kutoa onyo kuhusu hali ya mabadiliko ya mambo mbalimbali katika jamii. Mambo hayo yanahusishwa na kule kuingia kwa wageni kutoka nchi za ngambo, watu weupe wenye tabia ambazo kwetu ni za kimazingaombwe. Anajaribu kuwasihi wenyeji wakae kando na mambo yanayohusu Wazungu hao na kuwaomba wakae ange na kukata shauri kwamba watakaa wakishirikiana kama wenyeji kwani mambo kikoa, (uk.77-80).

Mwandishi amesawiri Mzuka kama mhusika wa kimazingaombwe anayemtumia mjukuu wa K kudokeza ufantasia ulioko ulimwengini. Mtunzi anatumia fursa hii pia kujisifu kwamba hatimaye azimio lake na yale ya wasanii wenzake yameafikiwa. Wasanii hao wa kimajaribio wanaona kwamba wako na mbinu huru sasa katika sanaa za kuwawezesha kuonyesha umakini wao katika uhusika na katika usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe ambao wataweza kutekeleza uwasilishaji wa ujumbe kulingana na mahitaji yaliyoko katika jamii ya kisasa. Mwandishi amechukua fursa yake pia kupitia usawiri wa aina hii kuonyesha jinsi matukio ya kimazingaombwe ni mambo ambayo yanafasiriwa na kueleweka kwa njia

tofautitofauti katika jamii mbalimbali. Hii ni kwa sababu mambo yanayochukuliwa kama mambo ya kifantasia katika jumuiya fulani yanaweza kuchukuliwa kama mambo ya kawaida katika jumuiya nyingine, (uk.18-22).

Umazingaombwe unaendelea kuonekana wakati Mzuka ambaye ni mhusika mkuu na wa kiajabu, amesawiriwa awe na hali ya kuwa na nguvu ya kuingia katika mawazo ya K na kumwongoza kulingana na mapenzi yake. Ametawala mienendo ya K hadi yeye kukula hasara ingawa amejitahidi sana kujitawanya kwa mapana na marefu huku akijitia ujuzi bala kujua kuwa kuiga tabia za Kizungu ndio kujipalia makaa.

Mzuka anatumia nguvu za kimiujiza kujaribu kufanya K asiwe na moyo wa kigeugeu bali awe na hamu ya kujihusisha na matukio mazuri katika jamii hasa akiwa kiongozi. Mzuka anajaribu kumkosoa K ili aweze kurekebisha mienendo yake na arudie hali yake ya zamani kabla kupata cheo uongozini, wakati alikuwa mtu mwema katika jamii. Mzuka anakataa kata kata mambo anayoyaona yakitekelezwa na viongozi kama K (uk.119-121). Mzuka ni sauti ya usawa na fikra za kiutu katika jamii.

Wakati huo huo, mwandishi anaendelea kumsawiri Mzuka kama mhusika anayeweza kutumia nguvu za kiajabu kutekeleza mambo mengi ya kifantasia huko na huko akisababisha K kuzunguka vuruvuru akiwa hana mpango wala mwelekeo. Mzuka anamfanya K aone ni kama ameingiwa na kichaa kwani kila kitu kinachomfanyikia humpa jipu la moyo (uk.18-20).

Mwandishi amemsawiri Mzuka pia awe na uwezo wa kumsababisha K azongwe na mambo huku akimwacha akabiliane na majaribio mengi. Ni jambo la kustaajabisha huku nyumbani mwa K anakumbushwa na Mzuka wakati mbwa wake alipokua akipelekewa chakula na

chakula hicho kutoweka kwa njia ya kimiujiza. Baada ya muda mrefu Mzuka anatobolea waziwazi K kwa kumwambia kuwa ni yeye ambaye alikuwa akiondoa chakula cha mbwa wake mara kwa mara na kukiwapa watu kijijini. Anamuelezea kuwa kwake kufanya hivyo wakati huo ni kwa sababu yeye (K), alikua akifanya kitendo kisichokubalika, kutojali watu katika jamii. Anamwambia K kuwa hangeweza kukubali aone mbwa akila chakula kizuri vile ilhali watu kijijini wanalala njaa.

Mzuka kwa njia ya kimazingaombwe anasababisha K akohoe vibaya sana huku akisikia sauti za watu wanaomchekelea. Isitoshe mtunzi anasawiri Mzuka kumfanya K asokotwe na tumbo na hapo basi hali yake kiafya ukazidi mashimo. Wakati huo tena, Mzuka anasawiriwa kusababisha K asikie akijicheka mwenyewe na kwa ghafla anawaona Mashetani wakimjia na kujaribu kutoroka anapata kuwa amefugwa kwa kamba. Kutazama vizuri, akashituka na kushikwa na bumbuazi kuona kuwa si kamba bali ni nyoka mrefu ambaye amemzukuka, (uk 7- 9).

Mzuka amesawiriwa pia awe na uwezo wa kutoweka na kujigeuza kuwa muye kisha anaongea na K huku wafanyikazi wa K wakishangaa kusikia anayesemezana na K, K akimjibu pia lakini hawamuoni mtu mwenyewe. Wanaambiana mwajiri wao amepatwa na kichaa, wengine wanasisitiza, kuwa si hivyo kwani nao walisikia mtu akiongea. Umazingaombwe ulioko pia ni kuwa ana uwezo wa kujibadilisha kiajabu ajabu, mara anageuka na kuwa popo, mara nyoka (uk.48-50).

Mwandishi Mohamed amemsawiri Mzuka pia awe mhusika mwenye akili na ujasiri kuzidi viongozi wanaoiga kila kitu hata vyakula kutoka kwa wakoloni. Kila mara wakiwa mkutanoni anasababisha zogo wa zahama kisha anawafanya wakoloni wao zuzuku zuzu huku

akiwakosesha fahamu ili kusababisha mipango yao na kuwaweka katika ukucha wake. Anaelewa kuwa maovu yanayotendwa na viongozi lazima yatakuwa na hukumu kali na kwamba hata vizazi vyao havitakosa mtego pia bila mtanabahisho, (uk.50).

Mwishowe mwandishi anamfanya Mzuka abadilike awe hakimu kisha kumpa jukumu la kumhukumu K huku akimtajia makosa yake yote moja baada ya jingine wakati mzuka huyo akiwa tayari amejigeuza kuwa mkuu wa gereza. Bila kusitasita, anampasulia K ukweli na katika hali hiyo hiyo akamwambia K waziwazi kuwa wakati wake wa kupashwa adhabu umewadia. K akabakia pekee akiwaza na kuwazua kwani yeye mwenyewe aliweza kupata taswira ya makosa yake yote na akawezeshwa kujionea maovu aliyoyatenda na hapo anajiuliza kama ni heri ajinyonge huku akilia kilio cha mbwa mdomo juu.

### 4.2.3 Eks

Mhusika Eks ni mhusika wa kimazingaombwe ambaye mwandishi, Tom Olali, amemsawiri kama mhusika mwenye nafsi zaidi ya moja. Mtunzi amemsawiri Eks na kuchukua fursa yake kuonyesha umaarufu wake wa usawirishaji wa wahusika wa kimazingaombwe kwa kutumia mbinu zake kwa njia ya kifantasia katika uhusika. Amemsawiri mhusika huyu awe na nafsi mbili na kumsababisha aweze kuwasiliana kwa njia ya kimazingaombwe na nafsi hizo kana kwamba ni watu wawili. Ni hali ya kustaajabisha wakati Eks anajigeuza pepo kisha kujizungumzia huku nafsi yake ikiwa pepo pia inamjibu na watu wanaosikia maongezi yao wanashangaa kwani kujaribu kutazama, hawaoni watu wenyewe wanaozungumza. Ni ajabu pia kuwa amesawiriwa kuwa na uwezo wa kuchukua umbo wa mhusika mwingine kisha kutekeleza shughuli za mhusika huyo bila kujulikana kuwa ni yeye na si yule.

Umazingaombwe wa wahusika umesawiriwa pia na mwandishi kudhihirisha kuwepo kwa uwasilishaji wa kimazingaombwe unaosawiriwa kufanyika kwenye mandhari ya kimiujiza

ambayo yamebuniwa na mwandishi kuambatana na malengo yake ya kisanii. Mwandishi amechukua fursa hii pia kuweka wazi uongozi mpaya unaosababishwa na wakoloni ambao wamekucha kuendeleza uongozi mbaya ya kuwadhulumu wananchi katika jamii, (uk 9-18).

Mwandishi amemsawiri mhusika Eks aweze kudhirisha shida wanazoweza kukumbana nazo watu wakikosa kuwajibika katika kukataa mambo ya kuwaiga wageni. Kwa mfano, vyakula vya kigeni anavyokula Eks vinamfanya anone kama nguruwe huku kitambi chake kukiwa kubwa hata kikawa kizuizi kwake kuvaa nguo anazozitamani kuvaa. Ikawa ni shida kwake kutembea, kuendesha gari na hata kuinama. Kitambi hicho pia kikawa kizingiti kinachomzuia kutekeleza shughuli muhimu kama vile kutekeleza kitendo kinachofaa cha ndoa (uk.17-21).

Eks anapatikana akikalia kiti cha jeuri huku akisawiriwa na mwandishi kama mhusika wa kimazingaombwe na kupewa uwezo wa kuwasiliana na pepo wa watu waliokufa zamani. Anawaomba wamruhusu ashiriki ngono na mizuka hiyo. Ni umazingaombwe zaidi kwake Eks wakati anaporuhusiwa kutekeleza matukio hayo ya ukahaba na mizuka, yeye pia akaanza kuandamwa kila mahali na wale pepo - jambo ambalo lilimkera sana na hapo akajua tayari amewekwa hatarini jambo ambalo lilimfanya kuingia jakamoyo. Alipokuwa akijaribu kukuna kichwa, ghafla lilitokezea jitu lenye umbo la mnyama asiyeweza kueleweka na kumchukua kwa mkono wake huku akimwambia kwamba sasa anasa kwake zimefika ukingoni na kwamba wakati wa mashtaka umefika.

Matukio ya kimazingaombwe ya kustaajabisha yanafanyika tena wakati Eks anapowasiliana tena na nafsi yake ya pili kwamba ni heri kifo cha kujifanyia kuliko kifo kinachotekelezwa na majitu. Eks mara moja anajitia kitanzi lakini ya ajabu ni kuwa nafsi yake ya pili inamzuia asife. Lile jitu harakaharaka likaja likamchukua na kumlazimisha ajitoe uhai. Eks akashindwa na la kufanya ila kutapatapa kama mfa maji huku akipanda Shetani (uk.265-269).

### 4.2.4 Binti Abdalla

Mhusika Binti Abdalla pia ni mhusika wa kimazingaombwe na amesawiriwa kama mhusika mwenye nguvu za kiungu. Amesawiriwa aweze kujigeuzageuza na kujifanya pepo na kutekeleza matukio ya kimazingaombwe na ya kutatanisha. Binti Abdalla anashika njia wakati wa usiku wa manane na kuzunguka kijijini kote akitafuta akina mama ambao wananyonyesha watoto wadogo kisha kuwafanyia kitendo ambacho akiwezi kuaminika. Anawashika watoto wale na kuwasukuma kwa lazima warudi matumboni mwa mama wao. Jambo la kutatiza zaidi ni kuwa watoto hao wanapofika tumboni, kila mmoja wao anageuzwa na kuwa mdudu mkubwa mwenye mabawa anayeshinda akijaribu kuruka nje. Wanapofanya hivyo, mama anawekwa katika majuto ya uzalishaji huku akijaribu kumsukuma mtoto atoke tumboni lakini wapi! Walisalia wakisonga ndani huku wakikosa kutambua lango liko wapi.

### 4.2.5 Inatesh

Inatesh pia ni mhusika wa kimazingaombwe na amesawiriwa kuwa na uwezo wa kugeukageuka na kuchukuwa umbo tofautitofauti akitekeleza matukio ya kimazingaombwe yenye ugaidi mwingi sana kwani yeye mwenyewe ni mkaidi kama mkia wa nguruwe. Amesawiriwa kuwa na tabia mbaya ya kuwatembelea watu wanapokula na kujigeuza nzi. Anaudhi sana mtu anapojaribu kuchukua chakula kwa mkono na kumega, papo hapo anaruka na kutangulia kinywani kisha kutoweka tumboni na kuvuruga kita kitu huku akimfanya kila mtu kukimbia msalani bila haja yenyewe kukamilika (uk.40-43).

Umazingaombwe wa mhusika Inatesh pia unaonekana wakati anajaribu kuwa msiri lakini ulaghai wake haufichiki. Alijifanya msichana mdogo huku akililia akisema eti yeye ni yatima na anahitaji kusaidiwa. Watu wengi walimzunguka wakimhurumia huku wakikosa kujua kuwa yale yalikuwa ni majonzi ya mamba tu. Amesawiriwa na mwandishi afanye matendo ya

kupiga moyo beni na ya kuogofya lakini kwa sababu sura yake ni ya kuvutia, wanaume wengi walishindwa kudhibiti majaribu ya kushiriki mambo ya kimapenzi na huyu msichana basi kuingia mtegoni, (uk.41-44).

Matukio ya kimazingaombwe yanafanyika hotelini wakati binti huyu alikuwa wamekodisha chumba cha kulala na mhusika Sikujua. Kwa gafla alitoweka chumbani huku Sikujua akiwa na uhakika kwamba Inatesh hakupitia langoni. Amesawiriwa akiwa mhusika wa kimazingaombwe na amepewa uwezo wa kutoweka hata kwa kupenya kuta kisha kutoka huku akiwashangaza waonalo tukio hilo, (uk. 43-46).

Binti huyu wa kimazingaombwe amesawiriwa pia awe na uwezo wa kumfanya kila mume anayekubali kufanya mambo ya kimapenzi naye apoteze fahamu na kisha kufanyishwa matukio ya kutatanisha ambayo yanaharibu hali yao ya maisha kabisa.

Umazingaombwe anaoutekeleza msichana huyu kulingana na usawiri wa mwandishi, umeweza kusababisha dhihirisho kuwa mwanadamu ingawa amepewa akili ya kutosha kujikinga na kujiepusha na mambo mabaya ulimwenguni, bado kuna nguvu za kimiujiza ambazo zinamsukuma hadi ajiweke motoni huku wakifa kwa mitutuo yao wenyewe (uk. 47-53).

### 4.3 Umazingaombwe katika Uwasilishaji wa Wahusika Wadogo

Wahusika wadogo ni wahusika wa maana sana katika kazi ya kifasihi hata igawa wamepewa jina linaloashiria udogo. Hawachukui nafasi kubwa katika kazi za kisanaa, bali huwa watendaji muhimu ambao shughuli zao ni kutekeleza uwasilishaji wa ujumbe katika ujenzi wa wahusika wakuu. Wahusika wadogo pia wanajulikana kama wahusika wasaidizi wanaosaidia wahusika wakuu kukamilisha shughuli zao kikamilifu. Kwa mujibu wa

Wamitila (2003:125), mhusika mdogo hutumiwa na mtunzi kujenga au kukuza dhamira kuu lakini nafsi yao inabaki kuwa ndogo. Wahusika wasaidizi pia hutumiwa kumsaidia msomaji apate kuelewe vyema matukio ya mhusika mkuu. Kupitia maingiliano baina ya mhusika mkuu na mhusika msaidizi, tumepata mwanga zaidi kuhusu hulka na wasifu wa mhusika mkuu kulingana na lengo la mwandishi (Njogu na Kimerah1999:41-42).

Yafuatao ni mifano ya wahusika wadogo wa kimazingaombwe wanaoshughulishwa katika kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kifantasia katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.*

### 4.3.1 Delpiero

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, Delpiero ni mhusika mmojawapo wa wahusika wadogo. Yeye alianza urafiki na K mara tu K alipopata mamlaka. Umazingaombwe wake ulipatikana wakati wavuvi waliposema kuwa walimuona baharini akijigeuza na kutoa mabawa kwa ghafla na kupaa juu angani na kupotelea huko. Amesawiriwa kuchukuwa nafsi ya mhusika anayeshughulikia uuzaji wa bidhaa za kimagendo kama vile sehemu nyeti ya albino. Amesawiriwa kujibadilisha sura kuwa albino na hata kuwa kijani kibichi badala ya rangi yake ya kawaida ya zeruzeru (uk.12-14).

### 4.3.2 Von Heim

Shughuli zake hasa ni kushinda makaburini akiwafufua watu waliokufa. Amesawiriwa kama mtu aliyevaa ngozi ya kondoo kwani anawadharau watu weusi na kuwaona waafrika kama mazumbukuku na wasio wa maana hapa duniani. Anachukulia mtu mweusi kama chombo cha kufanyia utafiti wa kisayansi kama vile kutoa mate ya panya kutathmini uzuri wa dawa kabla kutumika kwa matibabu. (uk 14).

### 4.3.3 Dilivio

Dilivio anayependa mcheza kamari ni mhusika wa kimazingaombwe kutoka nchi ya Italia. Umazingaombwe wake ni kuwa anajulikana kutokuwa na usingizi iwe usiku au mchana kwani yumo mbioni daima akijishughulisha na matendo machafu ya kimazingaombwe. Anapenda uasherati zaidi ya kiasi kana kwamba akikosa msichana au mwanamke yeye hutafuta ngombe, mbuzi au mnyama yeyote wa kike kisha anajigeuza kwa njia ya kimiujiza kuwa mnyama huyo kusudi atimeze haja yake vilivyo. Mitalino huyo anapenda anasa, kwa hivyo anamshawishi K wafuje mali ya umma kisha wajenge hoteli ambapo watu watakuwa wakijistarehesha kwa kucheza, kula, kuogelea, na hata kujianika juani. Anasema kuwa lazima wateja watakaokubalika hotelini, wote lazima wawe wanavua nguo zao zote kabla ya kiugia ndani (uk.42-44).

### 4.3.4 Mzula

Mtunzi amesawiri mhusika Mzula kama mhusika wa kiajabu. Yeye ni dereva mwaminifu na mtiifu kwa mkubwa wake K. Umazingaombwe wake unatokana na kusawiriwa kama mtu wa mkono wa mhusika Mzuka katika kazi yake ya kumtatiza K kwa hivyo anabadilikabadilika kila mara ili aweza kuchukua nafsi mpya kulingana na anachotakiwa kumfanyia K (uk. 17-28).

### 4.3.5 Maajuza

Maajuza naye ni mhusika wa kimazingaombwe aliyesawiriwa kama mkewe babu Mzuka na kama nyanya wa K. Umazingaombwe wake ni kuwa ana uwezo wa kuwasiliana na mumewe mzuka aliyefariki kitambo. Maajuza ana uwezo pia wa kutazama ndani ya vichwa vya watu na kutambua kilicho mawazoni mwa wajukuu na vitukuu wake kuhusu kutoamini kwao juu ya uwepo wa mizuka wanaoweza kuwasiliana na watu. Ana imani kuwa mizuka inaweza

kuwasiliana na walio hai katika njozi ama katika ruiya.Tunaarifiwa pia kwamba yeye ana uwezo wa kuwaona mizuka katika maumbo mengi kama vile nyani, chura, konono au kipepeo.

Maajuza ni mwenye busara nyingi na mara nyingi hushughulika kwa kufundisha wengine katika jamii. Alimuheshimu mumewe na kufuata maagizo yake ya busara hadi sasa hata ingawa aliaga dunia. Anaambia watoto wake kwamba, makungu wapo na ndio wanaopanga mielekeo yao katika maisha, na wakiwa na hasira, husababisha hali ya kutokuwa na utulivu au umakini miongoni mwao (uk.119).

### 4.3.6 Mahasimu wa K

Mahasimu wa K ni wahusika wa kimazingaombwe wanaopatikana mawazoni mwa K. Jukumu la wahusika hawa ni kuandamana na K kila mahali na wanaongezeka kuwa wengi kila mara shida za K zinapozidi kuongezeka. Inaaminika kuwa hao ni watu ambao hapo awali walikuwa wamegombana ama kufarakana na K kwa ajili ya ugomvi walio nao juu ya kutoelewana kisiasa. Hii ni kwa sababu ya K kuwa na tabia nzito daima na kutojali masilahi ya wananchi na kwa hivyo lengo lao ni kulipiza kisasi.

### 4.3.7 Mahakimu Wakati

Mahakimu Wakati ni wahusika wa kimazingaombwe wanaoishi mahakamani. Wao ni wazee wenye matamshi makali ya kutisha na sura isio ya kawaida. Wanamfanya K ale kiapo kisha kumhukumu kwa makosa aliyoyatenda. K anakumbushwa kuwa hata kujitoa uhai ni makosa tayari ya kutosha ahukumiwe. K pia anaambiwa kuwa akishafikishwa kwa Mahakimu Wakati basi hakuna lingine la heri ila yeye kushika moyo mkononi tu.

### 4.3.8 Mishi

Mishi ni mhusika wa kimazingaombwe anayepatikana ijapokuwa mara kwa mara anapotea kiajabuajabu kutoka jamii bila kujulikana anaenda wapi na anatoweka kwenda kufanya nini? Ni mhusika wa maana sana sana katika kuendeleza riwaya na kudhihirisha umazingaombwe katika hadithi. Umazingaombwe wa Mishi umeanza kuonekana wakati anajipatia jukumu jipya la kumtatiza Mwalimu Baya kwa kumharibia gari lake kila mara anapotaka kutoka jambo ambalo linamfurahisha sana.

Mishi aliye mhusika wa kimazingaombwe amesawiriwa kuwa na uwezo wa kusababisha matukio ya kimazingaombwe kokote akiwa na uchu wa kumuona akitaabika. Mfano ni kuwa siku moja alisababisha motokaa ya Baya kusimika katikati ya njia kwenye reli wakati gari la moshi ilipokuwa ikikuja kwa mwendo wa kasi lakini kwa ghafla, gari hilo la moshi lilipita juu ya gari la Baya kimiujiza bila kuwadhuru.

Umazingaombwe wa mhusika Mishi pia hutokea anapojibadilisha badilisha kiajabu. Mara mwalimu Baya anampata Mishi akiwa amevivalia viatu vyake vya kawaida na lakini kwa ghafla miguu yake inageuka na kuwa kwato za mnyama kama nyati. Mishi pia anadhihirisha umazingaobwe wake kupitia popote hata kwenye kuta na hata kuona na kutambua kilicho upande mwingine wa ukuta. Umazigaobwe wake zaidi ni kuwa ana uwezo wa kutawala nafsi ya mwanadamu yeyote kwa kumfanya apate usingizi nzito ili kumfanyisha mambo mabaya ya kimazingaombwe huku akilala torotoro.

Umazingaombwe pia unafanyika wakati mwili wake Mishi unapotoa mwanga yenye rangi mbalimbali na kutojulikana yeye ni nini. Watu kwa wanyama wanakuja kumtazama lakini umazingaombwe ni kwamba wanaomkaribia, anabanua mdomo yake kubwa zaidi kama

shimo kisha kuwavuta kwa nguvu na kuwameza. Wakati mwingine mwili wake unabadilika na kuwa jini mwenye vichwa viwili.

### 4.3.9 Shamsa (Baadayadhiki)

Mtunzi amesawiri mhusika Shamsa ambalo jina lake pia ni Baadayadhiki kama mhusika wa kimazingaombwe ambaye mahali pake ni makaburini. Umazingaombwe wake ni kule kuishi maisha ya upweke chakula chake kikiwa maini ya mizuka. Mtunzi anamsawiri mhusika huyu kufichua siri za wanao fanya mambo mabaya katika jamii. Baada ya kuwatambua anawapangia mashtaka wahukumiwe kifo kisha anawasubiri mle kaburini.

### 4.3.10 Mkuu

Mkuu ni mhusika wa kimazingaombwe anayepatikana mawazoni mwa mhusika Eks. Umazingaombwe wake ni kuwa na uwezo wa kutawala mienendo ya Eks. Anachukuwa nafsi ya Eks na kumuamuru afe. Eks ana aga dunia na baada ya miaka saba anaamuriwa afufuke kisha kuendelea na shughuli zake za hapo awali. Umazingaombwe pia ni kuwa Mhusika Shamsa mbaye yeye pia amesawiriwa kama mhusika wa kimazingaombwe, amepewa uwezo wa kuendelea kuwasiliana na mzuka wa Eks muda huo wote Eks akiwa kwa walio kwisha kata roho.

Mtunzi amemsawiri mhusika Mkuu ambaye ni mhusika msaidizi awe simba mwenye uwezo wa kutazama na kuweza kufahamu hali ya mambo jinsi yalivyokuwa yakitendeka ulimwenguni kote. Yeye akiwa na uwezo pia ya kuwakagua watu wanaostahili kuadhibiwa kisha anawapangia kifo. Mkuu amesawiriwa awe na uwezo wa kumwandama Eks kama vile Mzuka alikuwa akimkalia kitako mhusika K.

Mkuu amesawiriwa pia kama mhusika maarufu kimaarifa na amepewa uwezo wakujuza watu wake mambo muhimu na kuwataatharisha kutokana na matukio yoyote yanayoweza kusababisha hatari katika jamii. Jukumu lao hasa ni kukuzia njugu maganda ili aweze kuzuia watu katika jamii ambao ni wa manufaa kwao kama albino wasije wakafa kutokana na hali yoyote ile kabla waweze kuwa wamekomaa kutoshelesha mahitaji yao.

Mtunzi amesawiri mhusika Mkuu pia kama mhusika mwenye hekima na tena daktari hodari mwenye uwezo wa kushughulikia aina yote ya magonjwa na kuwaponya watu. Mtunzi anapendekeza kuwa mhusika Mkuu huyu ni mtafiti wa dawa na watafiti aina yake wangeendelea kuishi katika dunia ya leo, kungepatikana dawa ya ukimwi na kwa hivyo ni nafasi nzuri kushughulikia utafiti huo huo kwani nani asema eti watafiti hao hawako!

Mkuu ni mhusika wa kimazingaombwe ambaye amesawiriwa pia awe na uwezo wa kuweza kusawazishwa na uwezo wa Mungu na kusababisha matukio ambayo yamaonekana kutokweko mtu mwenye ujasiri kama yake ulimwenguni ila Mwenyezi Mungu tu.

Mtunzi anamtumia mhusika Mkuu kudhihirisha kuwa kuna nguvu za kiungu ambazo tunafaa kuweka imani yetu. Mhusika Mkuu analeta ufahamu kuwa watu weusi wanadhani kuwa wameumbwa na upungufu fulani kana kwamba wanafikiria kuwa watu weupe ni viumbe bora kuwashinda na kwamba uwezo wao unakaribiana na ya Mungu. Mkuu amesawiriwa awe na uwezo wa kutahadharisha watu weusi kuwa maendeleo ya utandawazi na ya kiuchumi usije yakawa chanzo kwao cha kuzipuuza mbibu za kiasili na ilhali kuwafanya waende kinyume wanapoaja utamaduni uliobora kwao. Anatoa mfano kuwa binadamu anapotengeneza ndege, yeye hajawahi kuona kuwa anahitaji utaalamu wa kutengeneza pia mahali pa kuegesha ndege hewanii na awe na uwezo wa kuirekebisha inapoharibika huku angani. Mungu amempa binadamu uhuru na uwezo wa kufanya atakavyo na kwa hivyo akitengeneza vitu ambavyo

vitamdhuru basi asimlaumu Mungu. Umeme ni mfano nzuri kwani mwanadamu aliutengeneza halafu umeme huo unaweza kumkatisha maisha wakati wowote asipoutumia vizuri.

### 4.3.11 Munkari

Mtunzi amesawiri mhusika Munkari awe mhusika wa kimazingaombwe na ambaye ni hakimu wa Gereza. Ni mlinzi mkali na tunamuona akiwazuia wahusika wasio viumbe au wateja wa Gehenna wanaojaribu kutoa usaidizi kwa wafungwa au mfungwa fulani kwani sio shughuli zao kufanya hivyo hata kama ni bibi yake au mtoto wake, (uk.219).

Mtunzi amesawiri mhusika Munkari awe na roho wa kufurahishwa na mateso yanayopewa watu huku gerezani na amejitosa cheo na kujipatia jukumu la kusimamia na kuwakaribisha watu huku gerezani (uk. 248-252).

Mtunzi anazidi kumsawiri mhusika huyu kutekeleza umazingaobwe wake kwa kuwa ana uwezo wa kujipwatuka ardhini kwa njia ya kimazingaombwe huku akiwa amevaa sare kama askari jela huku akitoa onyo kali kuwa ni lazima wafanya dhambi wote wahukumiwa na kupewa kichapo cha mbwa kabla kuwawacha wateseke kwenyenye jahanamu wakilia na wakisaga meno milele na milele, (uk.254-256).

### 4.3.12 Hikmat

Mtunzi amesawiri mhusika Hikmat ambaye pia ni mhusika wa kimazingaombwe awe mhusika mwenye maarifa tosha ya kisiasa (uk. 154-156). Amesawiriwa pia kama mhusika mwenye nafsi mbili na aliye na uwezo wa kujigeuza kwa ghafla na kuchukua umbo

kuambatana na malengo ya mtunzi. Mtunzi amesawiri Ikmat pia kama wakili wa wale wote wanaopitia changamoto katika jamii, (uk. 263-276).

### 4.3.13 Watu wa Gehenna

Mbinu alizozitumia mtunzi katika uhusika na katika usawiri wa wahusika wanaojulikana kama Watu wa Gehenna ni za kustaajabisha kwani wao wenyewe ni wahusika wa kimazingaombwe walioambatanishwa na matendo maovu yanayostahili adhabu ya milele gerezani. Mtunzi amesawiri makao yao yawe huku Gehenna kwenyewe. Wakazi hao wa gereza wana tabia za ajabu ajabu na matukio ya kimazingaombwe. Hawa ni viumbe wanaojuta daima kwa sababu walishiriki kwa njia moja au jingine katika utekelezaji wa mambo yanayosababisha matukio mabaya zaidi katika jamii. Wamesawiriwa kuishi wakisubiri kwa hamu na gamu vifo vijitokeze hapa na pale ili waongezeke huku jahanamu. Hao ni viumbe wa kustaajabisha kwani wanaofurahia wakati kuna matukio katika jamii ambayo yatasababisha vifo vya watu wengi ili wapate wateja wao, (uk. 7-9).

Tumebainisha pia katika sura hii kwamba uhusika katika riwaya hizi ulijengeka kutokana na hadhithi za kawaida katika jamii zetu. Watunzi wanaosawiri wahusika kwa kutumia mbinu za kimazingaombwe wanafanya hivyo kwa kuiga mbinu za fasihi simulizi zilizokuwa zikitolewa na kusambazwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kusimuliwa ama kwa kupitia mazungumzo katika jamii. Ni simulizi ambapo wahusika kama vile majitu, mizimu na hata wanyama waliaminika kuwa walikuwa na uwezo wa kutangamana na wanadamu katika ulimwengu halisi.

Katika kuangazia kipengele cha uwasilishaji wa wahusika hao wa kimazingaombwe, tumetazama matukio yao yanayojitokeza kulingana na mawazo ambayo yanabuniwa na watunzi kwa kujaribu kuambatisha vilivyo matendo ya wahusika hao na mahali

wanapotekelezea matendo hayo. Kupitia uchunguzi huu, tumebainisha kuwa waandishi S. A. Mohamed na Tom Olali wametumia kwa njia moja au nyingine mawazo ya wahusika wao kama mandhari ya kimazingaombwe.

Katika uchunguzi wetu kuhusu mandhari, tumefanikiwa kufahamu kuwa ndoto pia ni aina mojawapo wa mandhari ambayo yanachukua nafasi kubwa katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna*. Akieleza kuhusu ndoto, Malcolm (1959) anasema kuwa ndoto katika uwasilishaji wa ujumbe ni mtiririko wa mawazo yanayobebwa akilini mwa mtunzi. Matukio haya yote yanayotekelezwa na wahusika katika fasihi ni mambo katika mawazoni mwa watunzi ambayo yanasawiriwa yaambatane na maono, taswira na matukio yanayodhihirisha umazingaombwe wa wahusika. Hivyo basi ndoto ni chombo kinachotumiwa kusafirisha hisia na sifa za wahusika wanaosawiriwa na mtunzi na zinazojengeka katika mandhari husika.

Mtunzi wa riwaya ya *Babu Alipofufuka,* S. A. Mohamed katika uteuzi wake wa mbinu za uhusika na za usawiri wenye matukio ya kimazingaombwe ametumia fursa yake kumulika mashaka kadha wa kadha yanayohusu hali ya maisha ya wananchi katika jamii zetu za kiafrika. Zaidi ya hayo, msanii huyu anadhihirisha uwepo wa shida mbalimbali za kihistoria na za kisiasa ambazo viongozi wameshindwa kutatua. Udhoofu wa uwezo wao ukisababisha hali tata katika jamii na kutowezekana kuwepo na viongozi wenye ujasiri kama wa wafalme wa zamani ambao walikuwa na uwezo wa kushikamanisha watu katika jamii na kuleta umoja katika makubaliano ya pamoja katika ujenzi wa taifa.

Msanii Tom Olali naye ametumia mbinu za kimazingaombwe katika shughuli zake za uhusika na za usawiri wa wahusika wake wa kifantasia. Yeye pia ameweza kushughulikia kwa ustadi zaidi mambo mengi ajabuajabu katika uwasilishaji unaotekelezwa na wahusika

wa kimazingaombwe. Umazingaombwe huu umeonekana wazi kudhihirisha baadhi ya mambo katika uwasilishaji wa ujumbe katika riwaya za kimajaribio ambayo hayangeweza kuelezwa kwa kutumia mtindo wa kawaida wa kimapokeo katika sanaa za kisasa.

Watunzi wa riwaya hizi mbili wamekiuka sheria za uandishi wa kijadi na kuamua kutumia mbinu zao za kipekee katika uhusika na katika usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe. Uchunguzi wetu ulianisha kuwa nia ya watunzi hao wa kimapokeo kwa kukiukia mtindo mpya ya utunzi katika fasihi ni kuwawezesha kutekeleza uwasilishaji wa kimazingaombwe bila kuzuiliwa na sheria za kijadi za fasihi za kimajaribio.

Mbinu za utunzi wa fasihi za kimazingaobwe husababisha uwezekano wa mwingiliano unaowafaa watunzi katika ubunifu wao wa wahusika na mandhari yanayoambatana vilivyo na matukio ya wahusika katika kazi zao. Imebainika kuwa lengo la watunzi katika fasihi za kimapokeo pia ni kuwa huru kuwasilisha yale waliyo nayo mawazoni mwao na kuhakikisha kuwa hali halisi katika jamii umeonyeshwa wazi jinsi ilivyo. Hivi ni kumaanisha kuwa mambo yanayofanyika katika jamii hasa yaliyo mabaya yanahitajika kuvumbuliwa ili hali halisi ijulikane na labdha pingamizi kuondolewa na kwa njia moja ama nyingine marekebisho yafanyike.

Katika kutamatisha, tumebaini kuwa watunzi wa riwaya zilizoteuliwa wamebuni masimulizi yanayowasilishwa na wahusika wa kimazingaombwe kwa kuteua na kutumia mbinu za kifantasia bila kufuata kanuni za uaandishi jinsi ilivyo katika fasihi za kimajaribio. Wamitila (2003) anaeleza katika ufafanuzi wake anasema kuwa uteuzi wa mbinu katika uhusika na usawiri wa wahusika ni jambo muhimu zaidi katika sanaa. Anasema kuwa uteuzi wenyewe unahusu sifa ambazo zinayaeleza wazi matukio ya kimazingaombwe ambayo yanatekelezwa kuambatana na ubunifu wa masimulizi na uteuzi bora ya mandhari au mazingira. Akifafanua

zaidi, Wamitila anasema kuwa matukio katika riwaya za kimazingaombwe yanatekelezwa kwa kuashiria umazingaombwe unaopatikana katika jamii husika. Katika hali hii wahusika wanabuniwa kutekeleza masimulizi ambayo yanawezesha uwelewaji wa hali ya watu katika jamii hiyo. Lengo la watunzi katika fasihi za kimajaribio ni kuweka wazi mambo yanayotendeka katika jamii husika na uchochole kudhihirika na kuafikia vilivyo mahitaji ya wote katika jamii bila ubaguzi wowote.

Maelezo haya ya Wamitila yameweza kudhibitisha hekima za waandishi S.A. Mohamed na Tom Olali kwa kujitoa kwa ujasiri kubuni mwelekeo mpya ulio bora zaidi katika fasihi za kisasa inayokabiliana na mabadiliko ya aina mbalimbali ambayo yangezidi kukosa utatuzi kama hali katika fasihi ingebaki kuzingatia mbizu za sanaa za kimapokeo.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii tumechanganua na kujadili dhima na sifa mbalimbali za wahusika wa kimazingaombwe pamoja na kuchunguza matendo yao yanayowafanya wahusika hao waonekane viumbe wasio wa kawaida jambo ambalo linathibitisha umazingaombwe wao. Tumebaini kuwa wahusika huwa nguzo kuu katika kuleta wazi mawazo ya mtunzi na kusababisha mawasiliano katika kazi ya kisanaa. Kupitia kwa mshikamano wa wahusika hao wanapotangusana na kuvunja kanuni au maafikiano mbalimbali na wahusika wengine, tumebainisha upekee na umuhimu wa kila mmoja wao katika kuendeleza ama kuonyesha sifa bainifu za kimazingaombwe kama zinavyojitokeza katika riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna*. Sura inayofuata inaangazia muhtasari, mahitimisho na mapendekezo ya tasnifu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii ya tano imefafanua muhtasari wa tasnifu, matokeo ya utafiti pamoja na mahitimisho ya uchunguzi wetu. Hatimaye, utafiti umetoa mapendekezo yetu kuhusu utafiti wa baadaye.

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na umechunguza uwasilishaji wa wahusika na uhusika wa kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* (2001) ya Tom Olali na *Babu Alipofufuka* (2012) ya S. A. Mohamed. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni matatu mahsusi. Madhumuni ya kwanza yalikuwa ni kubainisha jinsi vipengele vya uwasilishaji wa wahusika vinavyodhihirisha masimulizi ya kimazingaombwe. Pili ni kuchunguza jinsi mbinu za uhusika zinavyomithilisha matukio na uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe katika riwaya zilizoteuliwa. Madhumuni ya tatu yalikuwa ni kuchanganua uwasilishaji wa wahusika ili kuainisha matukio na mandhari ya kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka*. Kwa kuangazia umuhimu wa malengo hayo ya utafiti, tumefanikiwa kubaini kuwa maazimio ya utafiti wetu yameafikiwa vilivyo.

Utafiti ulikuwa na jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ilihusu misingi ya utafiti na utangulizi wa jumla pamoja na kuchanganua nadharia ya uhalisiamazingaombwe unaodhihirisha na kubainisha uwepo wa uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe katika riwaya zilizoteuliwa kutumika katika uchanganuzi wa data za utafiti.

Sura ya pili ilihusu mapitio ya kazi za waandishi tangulizi ambazo zilitaliiwa baada ya kupatikana zikiwa na uhusiano na mada ya utafiti huu. Maandishi kuhusu umazingaombwe yalifafanuliwa pamoja na nudhumu nzima ya swala la wahusika na uhusika. Utafiti ulibainisha waziwazi pengo la utafiti. Umazingaombwe katika uwasilishaji wa wahusika na uhusika wao ni kipengele adimu katika riwaya za kisasa na ambazo hazijatafitiwa kwa kina. Aidha, nadharia ya utafiti ya uhalisiamazingaombwe ilifafanuliwa huku ufaafu wake ukibainishwa waziwazi.

Sura ya tatu imeshugulikia mbinu za utafiti ambapo sura iliweka bayana jumuiya pamoja na sampuli ya utafiti. *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* ziliteuliwa kimaksudi kama sampuli za utafiti kutokana na sifa za umaratokezi mwingi wa hulka za umazingaombwe wa wahusika na uhusika. Vipengele vya ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data vilevile vilizingatiwa. Utafiti huu ulikuwa wa kithamano ambapo mbinu ya maelezo,kama ilivyo katika fasihi, ilitumiwa.

Shughuli kuu katika sura ya nne ilihusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na kuchanganua usuhuba uliopo wa wahusika na uhusika wao hususan katika mandhari mbalimbali zilizomo ndani ya riwaya teule. Wahusika na uhusika wao katika mandhari mbalimbali riwayani na zenye umazingaombwe zimebainishwa na kisha kueleza namna zinavyokuwa msingi wa maana kwa hadhira. Riwaya, kwa mfano, zinatumia mandhari za kifahari sambamba na zile za kichochole ili kueleza matukio ya wenyenavyo kwa upande mmoja na wasionavyo kwa upande wa pili.Katika mandhari za kifahari ndimo mnamopatikana wahusika hao wa kimazingaombwe. Pia, kuna miktadha mingi inayohusu safari za kimaajabu ambayo imetumiwa kukoleza

wahusika na uhusika wa kimaajabu katika riwaya hizi, Sura hii pia imejadili wahusika wa kimazingaombwe, hulka zao na michango yao maalum katika riwaya teule. Wahusika mahsusi wakiwemo K, Mzuka, Eks, Inatesh,Maajuza na wengineo wa kimazingaombwe wamefafanuliwa.

Sura ya tano inahusu muhtasari wa tasnifu, mahitimisho na mapendekezo ya tasnifu. Maswala muhimu yaliyojitokeza yameelezwa kwa muhtasari. Aidha, sura hii imetoa dira ya tafiti za baadaye kwa watafiti wajao.

## 5.2 Matokeo na Mahitimisho ya Utafiti

Utafiti huu ulizingatia mada inayohusu namna riwaya zilivyowasilisha swala la wahusika na uhusika wa kimazingaombwe katika riwaya mbili teule za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.*

Kulingana na maelezo ya msanii Wamitila (2003:123), mhusika ni kiumbe anayesawiriwa na mtunzi ili aweze kutimilisha kazi zake za kisanaa kwa kumfanya amtekelezee matendo ambayo ameyabuni mawazoni mwake. Mhusika anasawiriwa kulingana na mbinu za uhusika ambazo mtunzi ameweka katika mpangilio wake. Anaposawiri wahusika wake, mtunzi lazima awe na mawazo akilini mwake na awe na mpangilio ya jinsi ya kuwaweka wahusika wake katika aina fulani ya mandhari. Kwa hivyo, mhusika ni kiumbe ambaye anasababishwa kutekeleza shughuli zote zinazohusu masimulizi na matukio katika kazi ya fasihi kwa jumla. Wahusika pia ni viumbe wanaosawiriwa wawe na maumbile yanayoambatana na shughuli walizopangiwa kutekeleza kulingana na mbinu za aina ya fasihi husika. Kihisia, mhusika anasawiriwa aweze kufanana na mwanadamu kwa kiwango kikubwa. Mienendo ya mhusika

pia husawiriwa kulingana na mbinu za uhusika zinazoambatanishwa na hali katika jamii inaohusu maendeleo ya kiuchumi, kielimu ama kiutandawazi kwa jumla.

Imebainika katika utafiti huu kuwa riwaya zote mbili zinahusu uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe. Katika kutekeleza hilo, riwaya hizi zimekiuka pakubwa sheria za kijadi za uandishi wa kama ilivyo katika fasihi za kimapokeo. Hivi ni kusema kuwa mtunzi katika fasihi za kimajaribio zikiwemo hizi za kimazingaombwe yuko huru kuiegemeza kazi yake kwenye mitazamo yake na mbinu anazozinuia kutumia katika uhusika, usawiri na uteuzi wa mandhari ambako matukio ya kimazingaombwe yatafanyika. Hivi ndivyo zilivyowasilishwa riwaya zetu za utafiti. Hakuna sheria zozote maalum zilizopendekezwa na waasisi wa jadi wa fasihi, yaani kina Aristotle na Plato ambazo zimezingatiwa hapa.

Shughuli kuu ya mhusika katika kazi ya kisanaa ni kuwasilisha ujumbe kulingana na malengo ya mtunzi. Matendo yanayotekelezwa na wahusika lazima yasawiriwe yaambatane vilivyo na yale yaliyo katika fikira za mtunzi. Wahusika huwezesha dhihirisho kuwa viumbe wanaosawiriwa kuonekana kuwa na maisha ya kawaida katika ulimwengu wa kawaida huwakilishwa na wahusika walio na hisia za kawaida na vile vile wahusika wa kifantasia wanasawiriwa wawe na hisia za kimiujiza na wanawezeshwa kuzalisha matukio ya kimazingaombwe. Wahusika basi huwa viumbe wenye jukumu kubwa katika kuendeleza hadithi katika kazi za kifasihi lengo lao likuwa kuwasilisha ujumbe kwa wasomaji lengwa kupitia kwa shughuli zao mbalimbali za kisanii wanapotagusana na wahusika wenzao. Imebainika katika utafiti huu kuwa wahusika wa kuu wa riwaya hizi ni viumbe wanaofafanuliwa zaidi na uwezo wao mkubwa wa hata kuingia ndani ya nafsi za wahusika wenza na kuwasababisha kuona yasiyoonekana na kufanyishwa mambo yasiyowezekana.

Wahusika hawa wana ukia maumbile kwa kuwa wanafanya mambo ambayo si rahisi kueleweka.

Kulingana na Wamitila (2003) mhusika ni dhana unaotumiwa kuelezea mbinu au njia anayochukua mtunzi katika kusawiri wahusika katika kazi yake. Matendo ya viumbe hao husawiriwa na kusababishwa kuingiliana na malengo au mawazo yaliyobuniwa na mtunzi. Hivi ni kusema kuwa vitendo vya wahusika huwa vinafanywa kuwepo na maafikiano baina yao wao wenyewe na mazingira au mandhari wanamopatikana wahusika hao. Ufafanuzi huu unatiliwa shaka na riwaya zetu za utafiti. Ili kuelewa uhusika katika usawiri wa wahusika wa riwaya hizi, tumeegemea usimulizi wenyewe riwayani. Riwaya zimechanganya na kuwatangamanisha wahusika wote kwa pamoja. Humu mna wahusika halisi na pia wale wa kimazingaombwe katika kazi hizi. Riwaya zimesawiri wahusika wengine wawe na uwezo wa kubadilika badilika kutoka wahusika halisi na kisha kuweza kurudi kuwa wahusika wa kimazingaombwe. Matukio mengi ya kifantasia yamesawiriwa yatendeke wakati wahusika wanapolala aula wakiwa wamo ndotoni na wakati mwingine matukio hufanyika wakati wahusika wakiwa macho lakini matendo au matukio yanayojitokeza ni ya kinjozi.

Uchunguzi wetu umebainisha kuwa nadharia ya uhalisiamazingaombwe imewezesha kuelewa na kuyathamini matukio mengi ya riwayani. Imetuwezesha kuelewa, kwa mfano, usorajua uliokithiri ambapo tunashuhudia mhusika akiwa mara labda anaota, pengine ndipo yupo katika hali halisi na wakati yupo uhalisini huenda ikawa ndipo yumo ndotoni katika mtazamo wa kimazingaombwe.

Katika uchunguzi huu, tumeweza kubainisha kuwa sifa za wahusika wa kimazingaombwe zinalingana na mawazo ya mtunzi na pia matukio yao huambatana na njia au mbinu

zilizotumiwa kuwasawiri wahusika. Watenda kazi katika fasihi za kinjozi wanaumbwa kwa lengo la kuwafanya wawe na masimulizi yenye mwambatano wa kina na matendo yao yanayotekelezwa vilivyo ili watambulike wazi kama wahusika wa kimazingaombwe.

Uchuguzi wetu kuhusu uwasilishaji wa ujumbe umetubainishia umuhimu wa usawiri wa wahusika unaotekelezwa kulingana malengo na mbinu za mtunzi katika kuendeleza riwaya zetu teule za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* ambazo zimefaulu kutekeleza kazi zao za kimazingaombwe bila vikwazo vyovyote vya kifasihi.

Imebainika pia kuwa fasihi hii ya kimazingaombwe hutumia wahusika na uhusika wa kutisha ili kuathiri fikra za wasomaji kuhusu hali nah alia duni za jumuiya ya riwaya. Tunapata kwa mfano usawiri wa wahusika hawa wa kimazingaombwe wakiishi katika maisha yenye mashaka tipitipi. Hali za kimaisha za watu hao zinatatanisha kwani hao ni watu damu moja katika hali yao ya umaskini na ambao wanalazimika kutumia vyakula visivyo vya wanadamu (kama vile kula kinyezi chao) kwa kuwa hawana namna nyengine wa kujilisha. Chakula hiki kinawadhuru na kuwafanya wawe wagonjwa jambo ambalo linasababisha shida zaidi kwa sababu hawana pesa ya kutumia kwa matibabu (Uk.120-223).

Utafiti huu umeonyesha pia kwamba usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe katika riwaya teule umetambulisha uwezekano wa matumizi wa mbinu mpya katika mtindo wa utekelezaji wa uhusika unaoakisi taratibu za utunzi katika sanaa za kimapokeo na kuegemea usawiri katika sanaa inayohusisha mambo ya kimazingaombwe katika jamii. Umazingaombwe wa mhusika Babu Mzuka, kwa mfano, unahusu kule kufufuka na kumjia mjukuu wake K kwenye maisha yake ya kindanindani na kumdhalilisha hadi akadhoofika

katika hali yake yote maishiani mwake. Ni jambo hili ambalo lilitia mkazo mtunzi aweze kutoa wasaa kwa msomaji na kuwatia katika ngoma si zao kwa kuwasababisha kupitia mbinu zake za usawiri. Mtunzi anawafanya wasomaji wake washiriki kimawazo hali ya kuwafanya wakazane katika kujaribu kutatua shida mbalimbali wanazosiona zikiwakabili watu katika jamii.

Jambo lingine ni kuwa usawiri wa aina huu umefanya msomaji kulazimika kuhitimisha kuwa viongozi kila wanapoishi huwa wanastahili kuandamwa au kufuatwafuatwa na pepo wa watu hao wenye hasira na kuwa wakati wowote wanaweza kulipiziwa kisasi hata kama hawana uhakika kama wamewahi kufanya kosa lolote lile (Uk.23-26). Usawiri wa aina hii wa wahusika kwa hakika ni shime kwa wasomaji na jumuiya kwa ujumla kuhakikisha kuwa mienendo na hulka ya viongozi ipigwe darubini ili kuhakikisha kuwepo kwa maadili katika swala zima la uongozi. Hii ndiyo kauli mbiu kuu inayopendekezwa na waandishi ili kuepuka mienendo mibaya ya kina K, Eks na wahusika wengine wenye na mienendo sawa na hiyo.

Riwaya pia zinaelekea kuidhinisha kuwa ni sawa kwa watu kutiwa hofu hizi za watawala waovu na kuwa zina uhalali wake na ni za haki. Ni kweli kuwa wananchi walioonewa na kudhulumiwa kwa muda ya miaka mingi hufikisha uvumilifu wao ukingoni na kukataa uwongozi huo duni katika jami kisha kuitikia mwangwi wa wale waliokuwa tayari kupindua serekali.

Katika kutamatisha maelezo haya ya uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe, Wamitila (2003) anaeleza katika ufafanuzi wake kuwa uteuzi wa mbinu katika uhusika na usawiri wa wahusika ni jambo muhimu zaidi katika sanaa. Anasema kuwa uteuzi wenyewe unahusu sifa ambazo zinayaeleza wazi matukio ya kifantasia ambayo yanatekelezwa

kuambatana na uteuzi bora ya mandhari au mazingira. Akifafanua zaidi, Wamitila anasema kuwa matukio katika riwaya za kimazingaombwe yanatekelezwa kwa ufantasia na yawe yanayowezesha uwelewaji wa hali ya watu katika jamii kudhihirika vilivyo na kuafikia mahitaji ya wote katika jamii bila ubaguzi wowote. Maelezo haya ya Wamitila yawafiki vizuri mahitimisho ya utafiti huu.

Kwa kuagazia matokeo ya utafiti wetu, tumefanikiwa kubainisha kuwa maazimio ya utafiti wetu yameafikiwa vilivyo. Mafanikio pia kwetu ni kwamba watunzi wa riwaya hizi mbili za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* wamebuni matukio na masimulizi ya kimazingaombwe yainayoingiliana na kuchangiana kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa uhusika wa kiajabu na katika mbinu zao za usawiri wa wahusika wa kifantasia na tumebainisha kwamba uwasilishaji wa kimazingaombwe unajibainisha wazi kwa kiwango kikubwa katika riwaya zetu teule.

**5.3 Kuafikiwa kwa Nadharia Tete**

Katika kukagua upimishaji wa nadharia chukulizi katika utafiti wetu, mwega wa uchunguzi wetu umeweza kuthibitisha mawazo yetu kulingana na haipothesia tulioweka ituongoze. Uwasilishaji wa ujumbe wa wahusika wa kimazingaombwe umechukua nafasi kubwa katika riwaya zote mbili za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka.* Umazingaombwe wa wahusika wao wa kifantasia umefanyika kuambatana na malengo ya waandishi wa riwaya zilizoteuliwa. Wahusika wametekeleza uwasilishaji wao vilivyo kuambatana na mazingira ya matukio hayo ya kimazingaombwe. Uchunguzi huu umebaini kuwa wasanii hao ambao wameegemea mbinu za kifantasia katika uwasilishaji walikabiliana na hali ngeni katika jamii uliosababishwa na mabadiliko ya kiutandawazi. Ni sababu mojawapo ya waandishi S.A.

Mohamed na Olali Tom kukumbatia mawazo yao mageni kwenye uandishi wa kimazingaombwe katika kazi zao ili waweze kuafiki uwasilishaji unaoambatana na mahitaji ya sanaa za kisasa na uchunguzi wa maswala ya kijamii kwa mtazamo wa Kiafrika.

Kumebainika pia kuwa mbinu za uhusika katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka* zinamithilisha matukio na uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe. Uchunguzi katika utafiti huu umeainisha kuwa watunzi katika kazi za kimazingaombwe hutumia mbinu katika uhusika ambazo ni za ubinafsi fulani kutegemea ubunifu wa kila msanii wa kimapokeo. Lengo moja walilo nalo wasanii hao wa kimazingaombwe ni kusababisha uwasilishaji wa ujumbe wao unaoweza kushughulisha matakwa ya kila mtu katika jamii kwa kupitia matumizi ya mbinu za usawiri ambazo hazina mpangilio unaowakilishwa kwenye sheria za sanaa za kimapokeo. Watunzi hao wa kimajaribio wametumia mbinu katika uhusika ambazo zimewawezesha kubuni wahusika na kuwapa uwezo wa kuwasilisha ujumbe walio nao mawazoni mwao kwa kufunganishwa vilivyo na mihimili ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Wasanii hao wamefaulu katika kutatua mambo ya kifantasia ambayo hayangeweza kutatuliwa kwa kuzingatia mipangilio katika sanaa za kijadi zisizo huru.

Utafiti huu pia umebaini kuwa uwasilishaji wa wahusika unaainisha matukio na mandhari ya kimazingaombwe katika riwaya za *Watu wa Gehenna* na *Babu Alipofufuka*. Uchunguzi katika kazi hii umetufahamisha kuwa mandhari, au mazingira ya kinjozi katika riwaya zetu teule yamesawiriwa kwa kutumia mbinu za kimazingaombwe. Katika uchuguzi wetu tumeweza kufahamu kuwa ingawa uhusika na usawiri wa wahusika katika riwaya hizi ulifanyika nyakati tofauti (2001 na 2012), mbinu za uandishi zinaashiria nia iliyo sawa kulingana na mawazo walio nayo watunzi hao. Jambo hili lamaanisha kwamba tofauti za wanda wa utunzi

sio kizingizio cha uelewano wa wasanii wa fasihi za kimajaribio ambao lengo lao ni kuafiki mahitaji ya sanaa za kisasa za kimazingaombwe katika jamii. Hili ni jambo ambalo linaleta wazi kuwa utengano uliokuwa ukisababishwa na hali ya kifasihi za kimapokeo hapo awali sasa umewekwa kando. Hapa ni kwamba hamna tena sababu ya kuwa na vizuizi katika uwasilishaji wa ujumbe kwani wasanii wa kisasa wako huru kubuni na kusawiri wahusika wa kimazingaombwe kisha kuwaweka katika mandhari yanayoambatana na matukio katika kazi zao bila kufungwa na vikwazo vyovyote vya taratibu za kifasihi.

## 5.4 Mapendekezo

Katika kuunga mkono na kuitikia mwangwi wa wasanii tangulizi wa kimazingombwe, tunadhamiria kuwa utafiti wetu utanufaisha wasomaji lengwa wa watunzi wa riwaya tulizoziteua za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.* Wataokapata manufaa pia ni pamoja na wasanii na wasomaji wa riwaya nyingine ambazo zinagawa madhumuni zao katika uwasilishaji wa ujumbe kupitia usawiri wa wahusika wa kimazingaombwe. Tunatumai pia kuwa utafiti wetu utakuwa msingi bora wa kutoa mwelekeo zaidi kwa watunzi wa kimajaribio kupitia utafiti wa dhati wa uwalisilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe katika riwaya za aina hii.

Ijapokuwa kazi yetu ya utafiti imeshughulikia uwasilishaji wa ujumbe wa wahusika wa kimazingaombwe kama inavyopatikana katika mandhari ajabuajabu katika riwaya za kimajaribio, wakati haujawadia wa kutamatisha utafiti zaidi na ubunilizi zaidi wa mbinu mbalimbali za uhusika na za usawiri katika riwaya aina hii. Ni jambo hili lililotusukuma kupendekeza kuwa wasanii wengine waweze kutumia nadharia nyingine kutafitia maswala tofatutitofauti katika nyanda pana za kisanaa za kisasa kwa kuwa kazi zetu zimekitwa tu

katika uhusika na uwasilishaji wa wahusika waliosawiriwa kwa njia ya kimazingaombwe katika riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna*.

## MAREJELEO


Adam J., na Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies.* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Alexander M. (1990). *Flights from Realism.* Lonss`don, Edward Anold, Allende I. (1985).

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Nairobi: Oxford University Press.

Baldic C. (2001). *The Concise Oxford Dictionary of Literary Terms.* Oxford University Press.

Babbie, E. (1999). *Basics of Social The Research.* Belmont: Wads worth Publishing Company.

D'haen T. L. (1995). *Magical realism and postmodernism: Decentering privileged centers*.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia uwanja wa fujo.* Nairobi: Vide – Muwa Publishers Limited

Kombo D. na Tromp, L. (2006) *Proposal and Thesis Writing*: Paulins Publishers.

Kothari C. K. (2008). *Research Methods and Technique*. New Delhi: Age International (P) Limited.

Malcolm N. (1959*). Dreaming U.S.A.* London. Routledge and Kegan Paul Ltd.

Njogu K. & Chimera, R.(1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Ponera A.S. (2014).*Utangulizi wa nadharia ya Fasihi Linganishi.*Dodoma: Karljamer Print Technology.

Roh Franz. (1925) Nach-Expressionismus-Magischer Realismus. Leipzig. Krinkhardt & Biermann.

Strecher, M. C (1999). Magical Realism and the Search for Identity in the Fiction of Murakami Haruki, Journal of Japanese Studies.

Thiong'o N. (2004). *Murogi wa Kagogo.* Nairobi. East African Educational

TUKI (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Toleo la Tatu: Dar essalaam. Institute of Kiswahili Research.

Wafula R.M., & Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi.

Wamitila, K.W. (2004). *Musaleo!* Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

Wamitila K.W. (2001). *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Warnes C. (2006). *Magic Realism and German Idealism*. *Modern Language Review*.

Williams, R. (1995). *The Postmodern Novel in Latin America*: *Politics, Culture, and the Crisis of Truth*. New York: St. Martin's.

Zamora P.L. & Faris B.W. (1995). *Margical Realism*: *Theory, History and Community.* London.